# Nipashe

Jumatatu Desemba 5, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581150

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US








**Mwili** wa askofu uliokutwa ziwani kuzikwa Mwanza

UKURASA 3




UKURASA 13



Choo kinachotumiwa na walimu na wanafunzi wa Shule ya Msingi Usari, Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro. **NA MPIGAPICHA WETU**

## RIPOTI MAALUM

# Utata wa kiafya walimu, wanafunzi wanapochangia vyoo vya shule

• **Watawa** wajitosa kusitiri walimu wa kike...*Ukurasa 26*



Mwenyekiti wa Bodi ya KCB Group, Andrew Kairu, Mkurugenzi Mkuu, Paul Russo, Mwenyekiti wa Bodi ya Tanzania, John Ulanga, Mkurugenzi Mtendaji KCB Tanzania, Cosmas Kimario na Mkuu wa Masoko, Mawasiliano na Uhusiano, Christine Manyenye wakiwa kwenye mazungumzo na Rais Samia Suluhu Hassan katika kikao kilichofanyika Ikulu Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## ‘Inawezekana Bandari Dar kuwa kinara Afrika’

UKURASA 4

## Mbowe atinga Marekani na ajenda nne za kisiasa

UKURASA 2


KIBO POULTRY PRODUCTS LTD

CHRISTMAS Sale

Pata Kifaranga bora wa nyama

Tsh 1,500/=



NI KILA JUMATATU NA ALHAMISI TUNASAMBAZA MIKOA YOTE

MAWASILIANO PIGA

Violet: 0762 645027

Tungi: 0624 019103



MICHEZO MEXIME: YANGA IMEIPONZA IHEFU UK.31 KATUNI UK.6

# Mbowe atinga Marekani na ajenda nne za kisiasa

Na Elizabeth Zaya

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, anatarajiwa kufanya ziara ya kikazi ya siku sita Marekani kuanzia jana.

Safari hiyo ya Mbowe nje ya nchi kikazi ni ya kwanza tangu aachiwe huru na Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi Machi 4, mwaka huu, ambako yeye na wenzake watatu walikuwa wanakabiliwa na tuhuma mbalimbali ikiwamo kupanga njama za kufanya vitendo vya kigaidi.

Kwa mujibu wa taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Mawasiliano Itifaki na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema, akiwa Marekani, Mbowe atahudhuria kongamano la kimataifa la Umoja wa Kidemokrasia (IDU) litakalofanyika kwa siku tatu mfululizo.

Katika taarifa yake hiyo, Mrema alisema: "Kongamano hili litakalohudhuriwa na vyama wanachama wa IDU, viongozi wa serikali, wabunge na maseneta pamoja na taasisi za kimataifa, litahitimishwa na kikao cha Baraza la Uongozi la umoja huo, Desemba 9, mwaka huu".

Mrema alisema kuwa Mbowe, akiwa Marekani, pia atahudhuria kongamano na Mkutano wa Baraza la Uongozi la IDU, akiwa kama Mwenyekiti Mwenza wa Umoja wa Kidemokrasia Afrika (DUA) na mmoja wa makamu wenyeviti wenza wa IDU.

Pia alisema akiwa nchini humo, Mbowe atafanya mfululizo wa vikao na viongozi mbalimbali duniani pamoja na taasisi na mashirika ya kimataifa.

"Mbowe atakutana na mashirika na viongozi mbalimbali kujadili demokrasia, utawala wa sheria na maendeleo ya kiuchumi barani Afrika kama Mwenyekiti Mwenza wa DUA.

"Mbowe anatarajiwa kuhitimisha ziara yake kwa kuzungumza na Watanzania waishio Marekani kwenye mkutano utakaofanyika Desemba 10, mwaka huu," alisema.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Amon Mpanju (katikati), akizungumza na Mkuu wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Dk. Joyce Nyoni (kulia) na Mkurugenzi wa Rasilimali Watu wa wizara hiyo, Vesensia Kagombora, katika ziara yake ya kukagua miundombinu mbalimbali ya kampasi ya Kisanagara wilayani Mwanga mkoani Kilimanjaro juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mipango kuwezesha WAVIU yaandaliwa

Na Mwandishi Wetu

SERIKALI imesema itatoa maelekezo kwa halmashauri kuweka mipango maalum kuziwezesha ofisi za vikundi vya watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi (Konga) katika maeneo ya usimamizi, ruzuku na mikopo.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene, alitangaza kusudio hilo jana alipozindua magari manane ya mradi wa 'Hebu Tuyajenge' uliofanyika katika Ofisi za (NACOPHA) jijini Dar es Salaam.

Alisema lengo ni kuwa imara na endelevu na kuwa na mchango mkubwa katika kufikia malengo ya kitaifa na dunia kuhusu Ukimwi.

Alisema Rais Samia alitoa maelekezo mahususi kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS), Wizara ya Afya na wadau wengine kuweka jitihada na mikakati madhubuti katika kuzuia maambukizi mapya ikiwa ni pamoja na kuimarisha huduma za upimaji wa VVU na matumizi ya dawa za kupunguza makali ya VVU (ARV).

Naibu Katibu Mkuu wa ofisi hiyo, Kaspar Mmuya aliwapongeza Baraza la Watu Wanaoishi na VVU (NACOPHA) kwa kazi nzuri katika kupambana na maambukizi ya VVU.

Akitoa taarifa, Mwenyekiti wa NACOPHA, Leticia Kapela, alisema baraza limepata neema kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu kwa upande wa vijana, wanawake na WAVIU kwa ujumla.

**Alisema lengo ni kuwa imara na endelevu na kuwa na mchango mkubwa katika kufikia malengo ya kitaifa na dunia kuhusu Ukimwi.**

# Serikali yamulika uzalishaji mazao Jeshi la Magereza

Na Mwandishi Wetu, IRINGA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, amelitaka Shirika la Uzalishaji Mali la Magereza (SHIMA) kutumia ardhi ya Gereza la Isupilo wilayani Mufindi mkoani Iringa pamoja na magereza mengine nchini kuongeza kasi ya uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara.

Akizungumza wakati wa ziara yake katika Gereza la Isupilo jana, Masauni alisema kuwa mbali na kuanza kazi kwa SHIMA, pia amefarijika na mapokeo makubwa ya mabadiliko ndani ya Jeshi la Magereza, hasa katika Mkoa wa Iringa.

Alisema kuwapo kwa SHIMA ni fursa kubwa kwa magereza kutimiza majukumu yao, pia kunufaika zaidi na shirika hilo kiuchumi kama gereza na wafungwa wanaomaliza muda wao.

Masauni alisema jukumu kubwa la shirika ni kusimamia shughuli za kibiashara zitakazotokana na kilimo huku magereza wakifanya shughuli za kusimamia wafungwa kwa kuripoti kwa Kamishna wa Magereza.

Alisema makubaliano kati ya shirika na Jeshi la Magereza kwa wafungwa yatakuwa ya kibiashara kati ya pande hizo mbili na itasaidia magereza na wafungwa kupata faida ya nguvu wanazotumia.

"Sioni ubaya wowote kwa Jeshi la Magereza kuwalipa wafungwa watakaomaliza vifungo vyao kwa nguvu watakayoitumia," alisema.

Waziri Masauni aliizindua Bodi ya SHIMA Novemba 3, mwaka huu, akisisitiza iwe na maono ya kibiashara na utekelezaji wa azma ya Rais Samia Suluhu Hassan ambaye moja ya vipaumbele vyake ni kuliboresha jeshi hilo na mifumo yake.

Masauni alisema katika kutekeleza mipango hiyo, Rais aliongeza bajeti ya jeshi hilo ili watekeleze majukumu yao ipasavyo kwa ufanisi na weledi.

Alisema kutoka na wajumbe wa bodi hiyo aliowateua kwa sifa na weledi wao, serikali ina matumaini makubwa kuwa watatekeleza majukumu yao kwa uzalendo wa kusaidia taifa.

"Lengo kuu la SHIMA ni kusaidia Jeshi la Magereza kutenganisha majukumu ya kijeshi na biashara bila mwingiliano wowote, ili kuwapo kwa mafanikio makubwa ya kujiendesha na kuchangia Pato la Taifa, hivyo ni matumaini yangu makubwa kuwa bodi hii itasaidia shirika hili kutimiza malengo hayo na kusonga mbele zaidi," alisema Masauni.

Masauni alifanya ziara ya siku moja moja katika mikoa ya Ruvuma, Njombe na Iringa akiwa na lengo ya kukagua utendaji kazi wa taasisi zake zilizoko katika mikoa hiyo.

HABARI KITAIFA

## Uzimaji moto kwenye mabehewa wakamilika

**Na Idda Mushi,** MLIMBA

UZIMAJI moto uliosababishwa na kumwagika kwa kemikali aina ya sulphur iliyokuwa ikisafirishwa kwenye mabehewa 22 ya gari moshi kutoka Dar es Salaam kwenda Zambia umekamilika.

Ajali hiyo ilitokea mwishoni mwa wiki katika Halmashauri ya Mlimba wilayani Kilombero mkoani Morogoro, Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ikiwahimiza wasafirishaji wa kemikali hatarishi kuchukua tahadhari zote wakati wa usafirishaji.

Akizungumza eneo la tukio hilo, Meneja wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Kanda ya Kati Dodoma, Gerald Meliyo alisema kemikali hiyo ni miongoni mwa kemikali hatarishi zilizoainishwa na Umoja wa Mataifa (UN).

"Ni kemikali inayoweza kuwaka moto haraka sana ikitokea msuguano wowote kama ilivyojitokeza hapa, na ikiwaka moto inatoa sumu gesi mbalimbali zinazosababisha athari za mabadiliko ya tabianchi.

"Ndiyo maana tunatoa angalizo kwa wote wanaosafilisha kemikali, hasa kemikali hatarishi, kuwa makini kwa kuchukua taadhari, pia kufuata taratibu zote zilizowekwa kwa mujibu wa sheria ya kemikali nchini," alisema Meliyo.

Aliwahimiza kuzingatia mafunzo ambayo yamekuwa yakitolewa na Ofisi ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ili kuhakikisha kemikali zinasafirishwa kwa usalama.

Meneja wa Utekelezaji wa Sheria kutoka Baraza la Taifa la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC), Jamal Baruti, alisema baraza hilo limeendelea kuangalia athari zinazoweza kusababishwa na kemikali hiyo hasa kwa upande wa mazingira ili kudhibiti.

"Sisi kama baraza kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali tutahakikisha kemikali yote iliyomwagika katika eneo hili inaondolewa na kusimamia mazingira ya eneo hili kurejeshwa katika hali ya kawaida ili kuyalinda mazingira na afya ya binadamu," alisema Baruti.

Meneja wa Usalama wa Shirika la Reli ya TAZARA, Sadick Anthony, alieleza mipango waliyonayo kuondoa mabehewa yaliyoanguka ili kufungua njia na kuruhusu usafirishaji kuendelea.

"Tutafanya mpango wa kutoa mabehewa yanayozuia njia ya reli na baada ya hapo tutaanza kutengeneza njia ya reli na safari za kupitia reli ya TAZARA zitaanza, na tutaendelea kuondoa mabehewa yote yaliyopo eneo hili," alifafanua.

Meliyo pia aliwahimiza wakazi wote wa vijiji vinavyozunguka eneo hilo la ajali kuwa watulivu mpaka pale utoaji wa kemikali hiyo utakapokamilika na kutangaziwa kuendelea kutumia eneo hilo kwa shughuli za kibinadamu.

# Askofu Kwangu kuzikwa leo

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MWILI wa Askofu mstaafu wa Kanisa la Anglikana Tanzania Dayosisi ya Victoria Nyanza (DVN), Boniphace Kwangu, unatarajiwa kupumzishwa leo katika makaburi yaliyoko kwenye dayosisi hiyo, jijini hapo.

Akizungumza na gazeti hili kwa njia ya simu, Mchungaji wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Victoria Nyanza (DVN), Kefa Mlugu, alisema kabla ya maziko atafanyiwa ibada ya mwisho katika kanisa kuu la Anglikana la Mt. Nicolao, jijini hapo itakayoendeshwa na Askofu Mkuu wa kanisa hilo nchini, Maimbo Mndolwa kuanzia saa tatu asubuhi.

Alisema wameruhusiwa na Jeshi la Polisi kufanya shughuli za mazishi na kumpumzisha kama familia ya kiroho leo kwenye makaburi ya dayosisi hiyo na baada ya maziko mambo mengine yataendelea.

"Naomba ufike katika ibada ya mwisho itakayofanyika katika kanisa kuu la hapa mjini na baada ya mazishi ndipo taratibu zingine zitaendelea, lakini kwa sasa tumeshakabidhiwa mwili na upo Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Bugando," alisema Mlugu.

Boniphace William Kwangu (61), Askofu mstaafu Dayosisi ya Victoria Nyanza, mwili wake ulikutwa juzi ukielea katika Ziwa Victoria baada ya kupotea kwa muda wa siku nne.

Inadaiwa kuwa askofu huyo aliyekuwa mkazi wa Shibula, wilayani Ilemela, aliaga nyumbani kwake Novemba 28, mwaka huu asubuhi akielekea wilayani Sengerema kupokea malipo yake ya mwisho ya Sh. milioni 2.5 baada ya kuwa ameuza eneo lake pamoja na nyumba yake kwa Kanisa la KKKT Sengerema.

Iliendelea kudaiwa baada ya kufika kwa wanunuzi wake hakufanikiwa kupewa fedha hizo kutokana na kilichoelezwa kuwa hakuwa na nyaraka za umiliki wa eneo hilo na akaamuliwa kurudi Mwanza ili kuleta nyaraka hizo.

Familia yake ilianza kupata wasiwasi baada ya kutorudi nyumbani kutopatikana kwenye simu yake ya mkononi.

Imeelezwa kwa kushirikiana na viongozi wa kanisa, walitoa taarifa Kituo cha Polisi Kirumba na kuzunguka katika baadhi ya vyombo vya habari ili kusambaza taarifa hizo bila mafanikio.

Taarifa ya Jeshi la Polisi iliyotolewa na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, ASCP Willbroad Mutafungwa, ilithibitisha kupatikana kwa mwili wake uliokuwa ukielea katika Ziwa Victoria karibu na linapojengwa daraja la Kigongo-Busisi maarufu kama daraja la JPM.



Wahitimu wa Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki (HKMU), wakila kiapo katika mahafali ya 20 ya chuo hicho yaliyofanyika chuoni hapo mwishoni mwa wiki, wahitimu 294 walikabidhiwa shahada mbalimbali na Mkuu wa Chuo, Spika Mstaafu, Anne Makinda. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Jela miaka 15 kwa kumuua mkewe kwa kumchoma kisu

**Na Said Hamdani,** LINDI

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Mtwara imemhukumu kifungo cha miaka 15 gerezani mkazi wa Kata ya Chikonji, Manispaa ya Lindi, Omari Hamisi (21), baada ya kukutwa na hatia ya kumuua mke wake, Nasra Selemani (20).

Hukumu hiyo ilitolewa na Jaji wa Mahakama hiyo, Dk. Eliamini Laitaika baada ya kuridhishwa na ushahidi uliotolewa huku mshtakiwa akikiri kutenda kosa hilo. Baada ya kutiwa hatiani, Wakili aliyekuwa anamtetea mshtakiwa huyo, Happynes Sabatho aliiomba mahakama kumpa adhabu iliyo nafuu mteja wake ikizingatiwa ni kijana mdogo anayehitaji kulitumikia taifa lake na amekaa mahabusu kwa muda mrefu, hivyo amejutia kosa.

"Mheshimiwa Jaji, ninaiomba mahakama yako tukufu kumpa mteja wangu adhabu iliyo nafuu kwani bado kijana na amekaa ndani kwa kipindi kirefu," aliomba wakili huyo.

Jaji Laitaika alimuuliza Mwanasheria wa Serikali, Yahaya Gumbo, iwapo ana kumbukumbu za makosa ya zamani kwa mshtakiwa, akidai hana huku akiiomba mahakama kumpa adhabu kali ili iwe fundisho kwake na wengine wenye tabia ya kuua binadamu wenzao ili kupunguza vitendo hivyo.

Akitoa hukumu katika kesi hiyo namba 41/2020, Jaji Dk. Laitaika alisema amesikiliza maombi ya pande zote mbili za utetesi na mashtaka, hivyo anamhukumu Hamisi kutumikia kifungo cha miaka 15 gerezani.

Awali ilidaiwa na Mwanasheria wa Serikali Yahaya Gumbo, kuwa mshtakiwa alifanya mauaji hayo Septemba 3, 2020, usiku huko Kijiji na Kata ya Chikonji, Manispaa ya Lindi kwa kumchoma kisu tumboni mkewe Nasra Selemani aliyemkuta akiwa na mwanamume mwingine.

Gumbo alidai kitendo kile alikifanya mshtakiwa baada ya kutomkuta nyumbani mke wake huyo na alipofuatilia alimkuta na mwanamume huyo aliyekimbia baada ya kuwakaribia na alipomhoji mke aliyekuwa naye, alishindwa kujitetea ndipo ugomvi ulipoanza na kumchoma kisu tumboni na kusababisha kifo.

HABARI KITAIFA



Mwonekano wa Bandari ya Jebel Ali nchini Dubai. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ‘Inawezekana Bandari Dar kuwa kinara Afrika’

**Na Beatrice Bandawe**

UFANISI kuanzia upokeaji na utunzaji wa makasha katika Bandari ya Dubai maarufu Dubai Port World (DP World) ni elimu tosha ya kuleta mageuzi ndani ya Mamlaka ya Bandari Nchini (TPA) na kuwa kitovu kikubwa cha biashara barani Afrika.

DP World kutoka Umoja wa Falme za Kiarabu inajumuisha bandari za Jebel Ali, Mina Rashid na Mina Al Hamriya imeleta mageuzi makubwa ya kichumi na kuchangia asilimia 30 ya Pato la Taifa (GDP).

Umoja wa Nchi za Falme za Kiarabu (UAE), kabla ya kuingia katika teknolojia ya kisasa ya upokeaji na usafirishaji wa mizigo, ilikuwa ikitumia ngamia kama njia kuu ya usafirishaji.

"Licha ya kuwa jangwa, sasa ni tegemeo kubwa kwa nchi mbalimbali duniani katika usafirishaji wa makasha kutoka kwa wazalishaji wakubwa mpaka kuwafikia wateja wadogo," anasema Abdulaziz Al Marzooqi, Ofisa anayehusika na Maendeleo ya Biashara Afrika na Meneja Uhusiano wa Kimataifa, alipokuwa akiongea na wahariri waliotembelea bandari hizo, Dubai, mwishoni mwa mwezi Novemba, 2022.

Anasema kutokana na teknolojia ya kisasa bandari hizo zina uwezo wa kuhudumia makasha milioni 13.5 kwa mwaka na kuifanya iwe bandari ya ufanisi zaidi duniani.

"Viongozi wa mataifa haya mawili wanaweza kufanyakazi pamoja na kuwezesha bandari kukua, kama UAE ilivyoweza kukua na kuwa lango kuu ya kupokea mizigo," anasema Almarzooqi.

Tanzania imejaliwa kuwa na bandari kubwa zinazotegemewa kuhudumia meli na shehena zikiwamo za Tanga na Mtwara hasa ikizingatiwa kuwa imezungukwa na nchi nyingi ambazo hazina bahari na kuwa tegemeo kubwa kwa nchi hizo.

TPA imekaa kimkakati kuhudumia nchi za Afrika ikiwamo Jamhuri ya Kidemorasia ya Congo (DRC), Malawi, Zambia, Rwanda, Burundi na Uganda.

Alipokutana na wahariri wa habari mapema mwezi Oktoba, mwaka huu mjini Bagamoyo, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Bandari Nchini (TPA), Plasduce Mbossa, alisema mamlaka hiyo ina uwezo wa kuhudumia makasha 700,000 pekee kwa mwaka.

Akisema mageuzi ya kiuchumi yanaweza kufanikiwa kama bandari za Tanzania zitaimarishwa kwa kuboreshwa kutoka zilipo sasa kwenye daraja la tatu na kwenda katika daraja la pili.

DP World ina uwezo wa kuhudumia makasha milioni 70 yanayopokewa kutoka meli 70,000 kwa mwaka kutokana na miundombinu na teknolojia inayorahisisha utoaji huduma.

DP World, inahudumia nchi kadhaa barani Afrika zikiwamo Somalia, Rwanda, Senegal ambazo baadhi yake mbali ya kutumia bandari hizo kusafirisha mizigo yao, lakini zimetumia fursa ya kufanya biashara ya chakula Dubai.

DP World, katika kuonesha kuwajali wananchi wake, moja ya bandari yake ya Mina Al Hamriya, wafanyakazi wanaendelea kutumia njia ya kitamaduni ya ushushaji mizigo (vyakula na mifugo) wakati wakiendelea kuelimishwa kuingia kwenye teknolojia ya kisasa.

Almarzooqi, anasema wanaamini Mamlaka ya Bandari Tanzania ina fursa kubwa ya kukua na kufikia hatua iliyofikiwa na DP World kama ina nia thabiti ya kuleta mageuzi ya uchumi.

"Tanzania inaweza kuwa kitovu cha uchumi Afrika Mashariki na Kati kupitia Bandari yake ya Dar es Salaam," anasisitiza Almarzooqi.

Nchi zingine zilizofanikiwa katika biashara ya bandari duniani ni Singapore, ambayo imebadilika kiuchumi kutokana na ujenzi wa miundombinu ya bandari inayofanyakazi kwa kufanisi mkubwa.

Kwasasa, bandari nchini humo inapokea meli 130,000 kwa mwaka huku sekta ya majini ikitegemea asilimia saba ya pato la nchi na ajira 170,000 kwa mwaka.

Hivi karibuni, Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumzia mageuzi ya bandari nchini alisema, lengo ni kuifanya Dar es Salaam kuwa kitovu kikubwa cha biashara ndani ya Afrika.

Mwezi Julai, mwaka huu, akizungumzia mageuzi ya sekta ya bandari, Rais Samia alisema lengo la serikali ni kuifanya Dar es Salaam kuwa kitovu kikubwa cha biashara ndani ya Afrika kama itaungwa vizuri.

"Tukiweza kuunganishwa vizuri, Dar es Salaam inakwenda kukua. Ni lango muhimu la maeneo barani Afrika."

Akawakumbusha waliokabidhiwa kufanyakazi bandari wafanyekazi kwa kasi kubwa kuendana na mabadiliko hayo.

Mkurugenzi Mkuu TPA, Mbossa anasema kuwa utekelezaji wa miradi mbalimbali katika bandari utasaidia ufanisi katika utendaji na uboreshaji wa kuhudumia makasha.

Akizungumzia dira ya mamlaka hiyo, Mbossa alisema nia ni kuwa kinara, kuongoza, kuwa lango la biashara ya kitaifa na kimataifa na kufikia uchumi wa daraja la pili kutoka la tatu lilipo sasa.

Anasema mageuzi makubwa ya kiuchumi yanaweza kufanikiwa kama bandari za Tanzania zitaimarishwa lengo kubwa ni kuongeza ufanisi.

Mradi wa Bandari ya Bagamoyo, mkoani Pwani, aliutaja kuwa moja ya chachu ya kuboresha huduma za bandari nchini, pia Chongoleani mkoani Tanga na Kisiwa-Mgao, mkoani Mtwara.

Akizungumza na Televisheni ya Taifa (TBC), Kaimu Mkurugenzi wa PTA, Mrisho Mrisho, anasema Bandari ya Dar es Salaam inaimarika kutokana na kuongezeka kwa ufanisi wa kuhudumia meli kutoka siku saba hadi tatu kwa sasa.

Vile vile, anasema imeongeza huduma ya kuhudumia hadi kuelekea meli 89 kwa mwezi badala ya 50 zilizokuwa zikihudumwa mwanzo.

**"Tanzania inaweza kuwa kitovu cha uchumi Afrika Mashariki na Kati kupitia Bandari yake ya Dar es Salaam," anasisitiza Almarzooqi.**

## Serikali yazitambua teknolojia mpya 90

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amesema serikali imetambua teknolojia mpya 90 zilizozalishwa nchini na hivyo kufanya jumla ya teknolojia zilizotambuliwa hadi sasa kufikia 479.

Amesema lengo ni kuwa na kanzidata ya kitaifa itakayorahisisha upatikanaji wa taarifa muhimu kuhusu teknolojia na bunifu nchini.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa Mahafali ya 16 ya Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) yaliyofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam.

Alisema wizara itaendelea kusimamia uendelezaji wa masuala ya sayansi, teknolojia na ubunifu ili kutoa fursa kwa wabunifu na wagunduzi mbalimbali kuonesha ubunifu wao.

Profesa Mkenda alisema wizara itaendelea kusimamia uendelezaji wa masuala ya sayansi, teknolojia na ubunifu ili kutoa fursa kwa wabunifu na wagunduzi mbalimbali kujitokeza, kuonesha bunifu na gunduzi zao.

Alisema katika kuboresha utendaji kwa vyuo vya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi nchini serikali imefanya mambo mbalimbali ikiwamo kujengea uwezo rasilimali watu kwa lengo la kuwezesha usimamizi wa utoaji wa elimu na kukamilishwa kwa taarifa za tafiti za soko la ajira katika umeme, madini na uchapishaji.

Kuhusu tatizo la mafunzo kwa njia ya vitendo Prof. Mkenda alisema serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia itafanya juhudi za kuwasiliana na sekta binafsi kupitia Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) ili watoe fursa ya mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi na wafanyakazi wa taasisi za ufundi.

"Ninamshauri kila mhitimu awe na dhamira ya kujiajiri na kuwa tayari kuvuka vikwazo vitavyojitokeza ili kufikia malengo yake. Aidha, napenda kuwakumbusha wahitimu wote kwamba jamii ina matarajio makubwa kutoka kwa mafundi sanifu na wahandisi walisoma katika taasisi hii," alisema Mkenda.

Prof. Mkenda alisema serikali imeimarisha ushirikiano na mataifa mengine katika uendelezaji wa elimu ya juu nchini kwa lengo la kuhakikisha wataalamu wanapata uzoefu na ujuzi wenye kuendana na mahitaji ya kikanda na kimataifa. "Nilipata fursa ya kutembelea kule Uingereza katika Chuo Kikuu cha Northampton na kukutana na watumishi wawili wa DIT wanaosoma kule, kwenye hili nawapongeza sana na kuwasihi inapotokea fursa ya kupeleka watumishi nje ya nchi basi iwe ni katika vyuo vikubwa vya aina hiyo ili kuendana na azma ya serikali kuwapatia Watanzania elimu itakayotuwezesha kukidhi mahitaji ya kikanda na kimataifa," alisema Mkenda.

Mwenyekiti wa Baraza la Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Dk. Richard Joseph, alisema katika mwaka huu wa fedha serikali imeipatia taasisi hiyo Sh. bilioni 2.7 ambazo ni za awamu ya kwanza ya utekelezwaji wa miradi ya ukarabati inayokadiriwa kugharimu Sh. bilioni 11 hadi kukamilika.

# Wizara na taasisi zabanwa matumizi takwimu za sensa

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

SERIKALI kwa kushirikiana na wadau imeandaa mwongozo wa matumizi ya takwimu za sensa ambao utazilazimu wizara na taasisi za serikali kutumia takwimu hizo katika kupanga mipango ya maendeleo nchini.

Mtakwimu kutoka Ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS), Philbert Gerald, aliyasema hayo juzi wakati wa mafunzo ya siku mbili kwa waandishi wa habari kuhusu matokeo ya mwanzo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 yaliyofanyika mjini hapo.

Alisema dhamira ya kuandaliwa kwa mwongozo huo kuiwezesha Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), wananchi na wadau wengine kutumia matokeo ya sensa kupanga mipango jumuishi kuhuisha sera zilizopita.

"Lengo la mwongozo ni kuongeza uelewa, uwazi na kupanga wigo wa matumizi ya matokeo ya sensa ya mwaka 2022 katika kuweka mipango ya maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi," alisema.

Gerald alisema mwongozo huo utatekelezwa katika kipindi cha miaka 10 kuanzia Novemba 2022 hadi Oktoba 2032 wakati sensa nyingine ya watu na makazi itakapofanyika.

Aliongeza kuwa mwongozo unatekelezwa kwa kuzingatia sera, sheria, kanuni na taratibu za serikali zinazohusu matumizi ya matokeo ya sensa katika kufuatilia na kutathmini mipango ya maendeleo inayotekelezwa kwa wananchi kupitia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Mpango wa Maendeleo ya Zanzibar.

Mratibu wa Sensa Zanzibar, Abdulmajid Jecha Ramadhani, alisema mwongozo huo utakuwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar ambazo zitakuwa zinafuatilia kuona kama wizara na taasisi zinatumia takwimu za sensa katika kupanga mipango ya maendeleo.

Ramadhani alisema matumizi ya takwimu bado yapo chini nchini, hivyo kuandaliwa kwa mwongozo huo kutazibana wizara kuhakikisha zinatumia takwimu za sensa katika mipango ya maendeleo.

Washiriki wa mafunzo hayo waliitaka serikali kutumia takwimu za sensa za mwaka 2022 ili zilete matokeo chanya katika maendeleo badala ya kuziweka kabatini.



Mkurugenzi wa Shirika la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), Janeth Mawinza (katikati), akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Msingi Mivumoni, Wazo jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki, alipokwenda kutoa elimu kuhusu madhara ya vitendo vya ukatili, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bilioni 2.5 wahitaji vifaa saidizi

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO) limesema watu zaidi ya bilioni 2.5 wanahitaji kupatiwa vifaa saidizi ili kutekeleza majukumu yao kutokana na kuwa na aina fulani ya ulemavu.

Pia limesema Tanzania ikikadiriwa kuwa na asilimia 9.3 ya watu wenye umri kuanzia miaka saba wakiwa na tatizo hilo.

Hayo yalibainishwa na Mwakilishi wa WHO kutoka Genneva- Uswis, Kylie Shae, wakati wa uzinduzi wa mradi wa mafunzo kwa watoa huduma za vifaa saidizi ngazi ya jamii, zahanati na hospitali katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro na Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero mkoani hapo.

Kylie alisema kati ya watu hao kundi la wazee ndiyo linaonekana kuwa na mahitaji makubwa ya vifaa hivyo huku idadi ya wanaopata ikiwa ni kidogo. Aidha, aliwapongeza wadau wanaojitolea kuwasaidia watu wenye mahitaji ya vifaa saidizi, huku akiitaka Serikali ya Tanzania kuangalia namna ya kutoa vifaa hivyo katika hospitali kwa utaratibu wa kawaida.

Meneja Programu ya Afya kutoka Shirika la Help Age International, Dk. Edwin Mung'ong'o, alisema lengo ni kuboresha upatikanaji wa huduma ya vifaa visaidizi.

Dk. Mung'ong'o alisema mradi huo umeshatoa aina 64 ya vifaa saidizi ikiwamo miwani, magongo ya kutembelea na viti vya kuogea pamoja na vifaa vingine ambavyo vitatolewa kwenye Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro na Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero.

Alisema katika Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro Manispaa vifaa hivyo vitatolewa katika zahanati 10, vituo vya afya vinne na hospitali moja, katika Halmashauri ya Mvomero vitatolewa katika zahanati 10, vituo vya afya vitano na hospitali moja.

Alisema Shirika la HelpAge International ni mdau mkubwa wa serikali katika kushughulikia masuala ya wazee kitaifa ikishirikiana na Shirika la MOREPEO lililoko mkoani Morogoro.

Mwakilishi wa Shirika la Kidini la Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku ya Mwisho (LDSC), Juventus Rubona, alisema wametoa vifaa saidizi 2,800.

Alisema msaada huo umetokana na michango na sadaka na zaka za waumini wenye uendo wa kuwasaidia wahitaji.

Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Ustawi wa Jamii, kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa(TAMISEMI), Amina Mfaki, alisema wanatambua kuwapo kwa makundi maalumu kama vile wazee na walemavu.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Dk. Ukio Kusirye, alisema taarifa zilizoko ni kwamba mtu mmoja kati ya watatu anahitaji vifaa saidizi kimoja au zaidi na kati ya hao ni asilimia 10 ndio wanapata vifaa wanavyohitaji.

Dk. Kusirye alisema hali hiyo inatokana na upatikanaji wa vifaa hivyo kukabiliwa na matatizo mengi ikiwamo upatikanaji usiotosheleza, mipango isiyozingatia mahitaji ya vifaa hivyo pamoja na uhaba wa watumishi waliopewa mafunzo ya kutoa huduma za vifaa saidizi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga jiimarisheni kimataifa dirisha hili dogo

**WIKI** ijayo Desemba 15, dirisha dogo la usajili kwa Klabu za Ligi Kuu, Ligi ya Championship (zamani Ligi Daraja la Kwanza) na First League (zamani Ligi Daraja la Pili) litafunguliwa rasmi kwa ajili ya timu kujiimarisha tayari kwa raundi ya pili ya ligi zao.

Hata hivyo, kuelekea kufunguliwa kwa dirisha hilo ni fursa nzuri pia kwa wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano ya kimataifa kwa ngazi ya klabu, Simba na Yanga.

Wawakilishi hao, Simba wanaipeperusha bendera ya taifa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ambapo kwa sasa wanasubiri kufahamu wapinzani wao watatu watakaopangwa nao hatua ya makundi wiki ijayo.

Kwa upande wa Yanga, yenyewe ina jukumu la kuiwakilisha Tanzania kwenye Kombe la Shirikisho Afrika, pia wiki ijayo itafahamu wapinzani wake watatu katika hatua ya makundi wakati droo hiyo itakapofanyika jijini Cairo, Misri yalipo makao makuu ya CAF.

Hivyo, wakati zikisubiri droo hiyo, kinachotakiwa kwa sasa ni kila moja kuanza kumulika wapi pakujiimarisha zaidi ili kwenda kufanya vizuri katika michuano hiyo ambayo inaingia hatua ya makundi yenye ushindani mkubwa zaidi.

Tunaamini mabenchi ya ufundi ya klabu hizo yameshawasilisha ripoti zao kwa kamati zao za usajili kwa kumulika nafasi ambazo wanahitaji kufanyiwa maboresho zaidi kuelekea usajili wa dirisha dogo wiki ijayo.

Kwa maana hiyo, kilichobaki ni viongozi na kamati zao za usajili kutimiza malengo hayo kwa kusajili nyota wakuja kucheza na kutoa ushindani kuanzia ndani ya vikosi vyao na kuzisaidia timu zao kwenye mashindano husika na si kuongeza wakukaa benchi.

Pamoja na ukweli kwamba tunatambua katika usajili wa dirisha dogo ni vigumu kupata wachezaji wazuri kutokana na wengi mikataba yao kumalizika mwishoni mwa msimu na hata wakipatikana huwa ni kwa gharama kubwa kutokana na klabu zao kuhofia kukosa mbadala wa kuziba nafasi zao, lakini hiyo haiwezi kuwa sababu dhamira ya kweli ikiwekwa.

Licha ya changamoto hizo, tunaamini hakuna namna zaidi ya viongozi wa klabu hizo kukubali 'kuvunja benki' zao ili kusajili wachezaji watakaoweza kuwapa mafanikio katika michuano iliyo mbele yao.


Sisi tunaamini kwa ubora ambao wawakilishi wetu hao wameonyesha hadi kutinga hatua ya makundi, pakifanyika maboresho yenye tija katika usajili wa dirisha dogo, wawakilishi hao wa nchi wanaweza kutinga nusu fainali hata fainali.

Malengo yetu ni kutaka kuona wawakilishi hao wote kwa pamoja wakifika hatua hiyo kubwa na si kuishia hapo tu bali pia kutwaa mataji hayo ili kujenga heshima ya soka la Tanzania.

Lakini hayo hayawezi kutimia kama utafanyika usajili wa mazoea, wakusubiri wachezaji ambao mikataba yao imemalizika na kutupiwa virago na klabu zao za awali.

Tunataka kuona wakisajiliwa watu wa kazi wenye viwango vinavyoeleweka na uzoefu wa michuano ya kimataifa kwani kufika hatua ya nusu fainali ama fainali kunahitaji wachezaji wenye kariba hiyo na uzoefu wa mashindano makubwa ya kimataifa, jambo ambalo tunataka kuliona katika dirisha hili dogo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Makosa ya kibinadamu kwa waamuzi sasa yabaki historia

**KUTOKANA** na malalamiko ya wadau wengi wa michezo nchini, pamoja na kinachoonekana kukua kwa teknolojia hasa kwenye mchezo wa soka, husussan Kombe la Dunia linaloendelea nchini Qatar, Bodi ya Ligi imeonekana kuanzisha juhudi za makusudi ili kuondoka na kutegemea maamuzi ya waamuzi kwa asilimia 100.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi, Almasi Kasongo, amesema eneo la waamuzi ni muhimu sana na kwa sasa wameanza kulifanyia kazi hasa kwenye masuala ya teknolojia.

Ni ukweli usiopingika kuwa kwa soka la sasa duniani, watu wameacha kutegemea macho ya waamuzi, badala yake wametengeneza vyombo vya teknolojia ambavyo vitakuwa vinamsaidia mwamuzi kulirejea tukio kwa uhakika zaidi tofauti na alivyoliangalia hapo awali na baadaye yeye mwenyewe kutoa maamuzi ya mwisho, yawe yale yale au kubadilisha.

"Dunia ilipo waamuzi sasa wanasaidiwa na vyombo vya teknolojia kuliko kutegemea binadamu kwa asilimia 100, kila siku wanabuni vyombo vipya vya kuwarahisishia kazi na kuwafanya watoe maamuzi ya haki zaidi. Tunaona hata huko kwenye Kombe la Dunia masuala ya teknolojia yalivyopiga hatua, ni sisi ndiyo tumebaki kutegemea waamuzi kwa asilimia 100, lakini juhudi zimeshaanza ili kuhakikisha siku za usoni tu inabaki kuwa historia kwa sababu Bodi ya Ligi imeliona hilo, Shirikisho la Soka nchini (TFF) na serikali wote kwa pamoja juhudi za makusudi zimeanza ili siku za usoni tuondokane na changamoto hii.

Nakumbuka Februari mwaka huu, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, aliandika kwenye mtandao wake wa kijamii kuwa atakaa na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa, ili waongee uwezekano wa kutenga bajeti ya kununua chombo cha teknolojia cha kumsaidia mwamuzi, VAR.

Mpaka sasa hatujapewa mrejesho kuwa imefikia wapi, lakini maneno yale yasiwe tu yametamkwa kwa sababu ya timu anayoipenda ilikuwa imenyimwa haki, yawe ya kweli kwani inaonekana kwa sasa VAR ni muhimu zaidi kuliko hata wakati ule aliokuwa akisema.

Kila muda unavyozidi kwenda ambapo wenzetu wanazidi kunufaika na VAR ndiyo hapa nchini waamuzi wanavyozidi kuvurunda na kuonekana kukifanya chombo hicho kionekane kinahitajika zaidi kuliko muda uliowekwa.

Hivi sasa waamuzi kupelekwa kwenye kamati yao siyo jambo la ajabu tena, waamuzi tena wale waliokuwa wanaaminiwa, wakiwa na beji za FIFA wamekuwa wakifanya makosa ambayo wakati mwingine ni ya kawaida sana na yalitakiwa kufanywa na wale ambao ni wageni kwenye fani hiyo.

Ukiiangalia Ligi Kuu Tanzania Bara tangu msimu uliopita, timu zimeonekana kujipanga kisawasawa kwenye usajili, zikileta 'vyuma' kutoka nje ya nchi na wamekuwa wakipambana sana uwanjani, lakini wakati mwingine zinakatishwa tamaa na refa ambaye maamuzi yake yanabadilisha kila kitu, matokeo na hata morali ya wachezaji na makocha.

Waliotengeneza na kukubali teknolojia hii itumike ni watu waliokaa wakafikiri inawezekana vipi makocha wapewe mamilioni ya pesa kuzifundisha timu mifumo mbalimbali ya kwenda kukabiliana na timu pinzani, halafu kila kitu kinakwenda sawa, lakini kosa moja la mwamuzi linabadilisha kila kitu?

Ni kwamba imefika wakati sasa hapa nchini maamuzi yanayofanyika uwanjani yote yawe sahihi, kama lilikuwa bao halali likakataliwa na mwamuzi, watu walio kwenye VAR watamwita kwenda kuangalia na atatoa haki. Iwe hata kinyume chake sawa tu, ili mradi haki imetendeka.

Mfano hapa nchini timu ndogo zimekuwa zikitesema mno. Kwanza wachezaji wake mishahara midogo, kambi duni, chakula cha kuungaunga, usafiri matatizo, halafu zinafika uwanjani zinapambana kwa kadri zinavyoweza, lakini anatokea mwamuzi mmoja tu, anawanyonga na kuwakatisha tamaa.

Ukweli ni kwamba, serikali, TFF na Bodi ya Ligi wanatakiwa kufanya mchakato huo haraka ili haki itendeke na ionekane kweli imetendeka.

Vyovyote iwavyo, kama waamuzi wanafanya hivyo kwa sababu za kibinadamu au kwa makusudi haitakiwi tena. Dunia imeshaanza kutoka huko. Na klabu za Tanzania nazo zianze kujiandaa kisaikolojia, si muda mrefu VAR itaanza kutumika.

Kama kulikuwa na michezo michafu inachezwa, huu ni wakati wa kuacha na kuanza kucheza soka, vinginevyo VAR itawapa tabu sana na kuonekana kama kuna uonevu, kumbe kuna timu zilizoea vya kunyonga na si kuchinja. Siku zote ogopa kwanza Mungu kisha teknolojia.

## Tani 400 nyama ya nguruwe kuzalishwa

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha Ushirika cha Wafugaji Nguruwe Dar es Salaam na Pwani kimepanga kuzalisha tani 400 kwa mwaka ambazo kwa sasa hoteli kubwa nchini zinaziagiza nje ya nchi.

Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Denis Kiwali, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki wakati wa mkutano mkuu wa kujadili mipango na mikakati ambayo bodi ya chama imeiandaa kuendeleza ushirika huo.

Alisema kwa muda mrefu wamekuwa na kikwazo katika upatikanaji wa malighafi za kutengeneza chakula cha mifugo hiyo ambazo huagiza nje ya nchi pamoja na ukosefu wa machinjio ya kisasa inayokidhi viwango vya kimataifa.

"Tumepata mafunzo, kupitia chama tulifanikiwa kumleta mwalimu kutoka Uholanzi ambao ni moja ya nchi zilizopiga hatua katika hili, akatufundisha mbinu mbalimbali. Kwa sasa mashamba ya wafugaji wa nguruwe mengi yamekuwa na matokeo chanya, wanafuga kitaalamu," alisema.

Aliyataja malengo ya kuanzishwa kwa chama hicho ni pamoja na kuanzisha viwanda vya chakula ambavyo vitatumia malighafi za ndani ya nchi na kusaidia wanachama kupata soko na serikali kupata mapato.

"Tunakusudia kuanzisha maghala kuhifadhi chakula, kwa sasa kuna baadhi ya vyakula inatubidi tuagize nje, mfano Uholanzi na gharama ni kubwa na ukizingatia bado ni wajasiriamali wadogo, kwa mtu mmoja mmoja ni vigumu kuagiza na hata wanaojaribu kuagiza kwa kuungana wachache, bado ni ngumu," alisema.

Kiongozi huyo alitaja lengo lingine walilonalo ni kuanzisha machinjio ya kisasa itakayokidhi vigezo vyote ili kuteka soko ambalo kwa sasa hoteli kubwa nchini zimekuwa zikiagiza nyama hiyo nje ya nchi.

"Kwa sasa tunalihudumia soko la ndani lakini bado hatujalitosheleza kwa kuwa na nyama ya kutosha, tunalenga ndani ya miaka miwili ijayo tutazalisha tani 400 za nyama ya nguruwe nchini kwa mwaka, hoteli kubwa huzitaiagiza nje, wataipata kwetu.

"Tunaiomba serikali na mashirika yanayohusika na mifugo watuunge mkono kwa sababu suala la nguruwe bado halijapewa msukumo mkubwa kama ng'ombe na mbuzi, tunaomba serikali iturahisishie kwenye maeneo yanayohusiana na vibali ili tufanikishe malengo yetu," alisema.

Mfugaji wa nguruwe, Praygod Matemba alisema lengo la kuanzisha umoja huo ni kuleta mapinduzi katika sekta ya ufugaji kwa sababu wanapoifanya mtu mmoja mmoja inakuwa na changamoto, hasa ya vyakula.

Mjasiriamali mwingine wa nguruwe, Elinami Swai alisema suala la ufugaji huwa na mambo mengi ikiwamo upatikanaji wa mbegu bora, chakula na dawa.

Ofisa Ushirika wa Halmashauri ya Mji wa Kibaha, Amos Chacha, alisema kupitia mkutano huo, wametoa elimu kwa wanachama kuhakikisha wanasimamia misingi ya uanzishwaji wake ili umoja huo uwe endelevu.



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi, Kata ya Kunduchi, Hashimu Komba (wa pili kushoto), akimkabidhi kadi za kliniki na sabuni Mganga Mfawidhi wa Zahanati ya Tegeta, Rehema Kombo, ikiwa ni siku maalum ya kutoa shukrani kwa wanachama wa tawi la Tegeta la CCM. Wengine ni Katibu wa Jumuiya hiyo, Kata ya Kunduchi, Esther Mande (wa tatu kushoto), Mwenyekiti, Zainabu Semajongo (wa pili kulia) na Katibu, Apendavyo Mwambo. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# 'Mwinyi ameleta mwanga wa maendeleo ajira kwa vijana'

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WAVUVI, wakulima wa mwani na madereva wa bodaboda kisiwani Pemba wamesema mwanga wa maendeleo umeanza kujitokeza tangu walipopewa vifaa vya kisasa zikiwamo pikipiki na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Kwa nyakati tofauti walieleza hayo walipozungumza na waandishi wa habari Micheweni, Shumba Mjini na Chake Chake, Mkoa wa Kusini Pemba, kuhusu maendeleo yanayoendelea chini ya mpango wa uchumi wa buluu.

Rais mstaafu, Dk. Ali Mohamed Shein, anatarajiwa kumkabidhiwa Rais Dk. Mwinyi wadhifa wa Makamu Mwenyekiti wa CCM Zanzibar baada ya Mkutano Mkuu wa Taifa wa chama hicho.

Katibu wa Bandari ya Shumba Mjini, Hussen Kheri Hussen, alisema uamuzi wa Rais Dk. Mwinyi kujenga bandari ya kisasa ambayo itatoa huduma za usafiri na uchukuzi kati ya Pemba na Mombasa, kutaongeza ajira na harakati za kiuchumi kisiwani Pemba.

Alisema katika kipindi cha miaka miwili Rais Mwinyi ametoa boti 1,074 kwa wavuvi na wakulima wa mwani kisiwa cha Pemba, kikipata boti 577 jambo ambalo limesaidia kukuza kipato kwa wavuvi na wakulima wa mwani.

Alisema wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu wananchi wa Shumba Mjini, walimwomba rais awajengee bandari, mradi ambao tayari utekelezaji wake umeanza kufanyika baada ya kupatikana mkandarasi.

"Wakulima wa mwani walikuwa wanatumia vidau kwenda kupanda na kuvuna baharini, lakini sasa wanatumia boti za kisasa zenye usalama zaidi, alisema Hussen. Kiongozi wa Jumuiya ya waendesha Bodaboda Micheweni Pemba, Hassan Haji Hamad alisema vijana wamejiajiri kupitia kazi hiyo baada ya Rais Mwinyi kuwapa vijana pikipiki 250 katika Wilaya ya Micheweni na Wete, Pemba.

Alisema tangu Rais Mwinyi aliposhika wadhifa huo ameonyesha nia ya kuikomboa Zanzibar na kuiletea maendeleo, kuondoa siasa za chuki, ubaguzi na ukabila kutokana na kupeleka maendeleo kwa wananchi bila ya kujali itikadi za vyama.

Naye Mwalimu Kombo Sadi Hamad alisema hatua ya serikali kuamua kujenga kiwanda cha samaki Pemba na kiwanda cha kuchakata mazao ya mwani na karafuu kutasaidia kupunguza tatizo la ajira kwa vijana na kuongeza thamani ya mazao hayo.

Aidha, alisema Wilaya ya Micheweni tatizo la ukosefu wa ajira limepungua kwa vijana baada ya rais kutoa pikipiki 250 kwa vijana.

Nachia Haji Hamad na Bikombo Rashid, walisema mabadiliko ya maendeleo katika kilimo cha mwani yameanza kuonekana tangu kukabidhiwa boti za kisasa.


Naye Omar Musa, mkazi wa Chake Chake, alisema miradi mikubwa kupitia mipango ya uchumi wa buluu ifanyike haraka utekelezaji wake ili kuondoa tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana kutokana na kundi la vijana wakiwamo wasomi wasiokuwa na kazi kuendelea kuongezeka Zanzibar.

Alisema katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wa Dk. Mwinyi, miradi mingi ya maendeleo imejitokeza ikiwamo ya ujenzi wa nyumba za makazi, masoko, hospitali za wilaya bandari ya kisasa ya Magapwani, lakini bado kuna tatizo la ajira kwa vijana.

Kwa mujibu wa takwimu za Mamlaka ya Maendeleo ya Uwekezaji Vitega uchumi Zanzibar (ZIPA), katika kipindi cha miaka miwili wamesajili miradi ya uwekezaji yenye thamani ya Dola za Marekani milioni tatu tangu Rais Mwinyi aliposhika wadhifa huo.

## KABWELA

Fadhili Mohamed



# Asakwa kwa kusambaza video inayohujumu utalii, Rais Samia

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

ALIYESAMBAZA kwenye mitandao ya kijamii video inayodaiwa ya uzushi ikiwaonyesha raia wa kigeni wakilalamika kukaa muda mrefu bila ya kupata huduma kutoka kwa maofisa wa Jeshi la Uhamiaji, anasakwa kwa kuhujumu jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan za kutangaza vivutio vilivyoko nchini.

Tukio hilo lilitokea hivi karibuni kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Kilimanjaro (KIA).

"Sisi tumefanya uchunguzi na kujiridhisha kuwa aliyefanya kitendo hicho cha kurekodi na kusambaza video hiyo iliyoleta taharuki nchini na duniani kote ni raia wa Tanzania ambaye ameonyesha kuwa siyo uzalendo kwa taifa letu na ana nia ovu ya kufifisha jitihada za Rais Samia katika kukuza utalii nchini kupitia filamu ya Tanzania The Royal Tour," alisema Mrakibu wa Uhamiaji na Msemaji wa Uhamiaji, Paul Mselle alipotoa ufafanuzi kuhusu tukio hilo jijini hapo jana.

Alisema uchunguzi na ufuatiliaji walioufanya umejiridhisha abiria anayelalamika aliingia nchini kwa Ndege ya Shirika la Ndege la KLM akitokea Amsterdam Novemba 26, mwaka huu, majira ya usiku.

"Ndege hii ilikuwa na abiria 317 ambapo abiria 226 walishuka KIA majira ya saa 3:06 usiku na kuanza kupata huduma za kuingia nchini. Abiria hawa 226 walihudumiwa kwa dakika 94 sawa na wastani wa dakika mbili na sekunde 40 kwa kila abiria.

"Hivyo, Jeshi la Uhamiaji linapenda kuujulisha umma kuwa kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya Shirika la Usafiri wa Anga Duniani (ICAO) abiria mmoja anastahili kuhudumiwa kwa muda usiozidi dakika tatu," alisema.

Alisema abiria 91 waliokuwa washuke katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) walielekezwa kushuka uwanja wa KIA saa 5:45 usiku baada ya abiria wa awali kuhudumiwa na kuondoka.

"Hawa walielekezwa kushuka uwanja wa KIA kutokana na sababu za kiufundi zilizopelekea ndege ya KLM kutokuelekea Dar es Salaam na katika awamu hii abiria hawa 91 walihudumiwa wastani wa dakika mbili kwa kila abiria ambapo walianza kuhudumiwa mnamo saa 5:50 hadi saa 6:35 usiku," alisema.

Alisema taarifa iliyosambazwa kwenye mitandao ya kijamii siyo sahihi kwa kuwa abiria wote walihudumiwa kwa mujibu wa taratibu na viwango vya kimataifa vya kuhudumia abiria katika viwanja vya ndege.

Alitoa rai kwa Watanzania kuwa wazalendo kwa nchi yao na kusaidia jitihada za kukuza uchumi kupitia sekta ya utalii.




Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, akiwa uwanjani kushuhudia mchezo wa Kombe la Dunia la FIFA kati ya Argentina na Poland ikiwa ni sehemu ya mwaliko rasmi kutoka Visa International ambayo ni mshirika rasmi wa FIFA wa teknolojia ya malipo. Benki ya CRDB imekuwa na uhusiano wa muda mrefu na Visa kupitia mifumo yake ya malipo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## CRDB na Visa wanaleta ubunifu malipo kwenye Kombe la Dunia

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI mashabiki na watazamaji wa michezo duniani kote wakisherehekea Kombe la Dunia la FIFA 2022, Benki ya CRDB na Visa International, mshirika rasmi wa teknolojia ya malipo wa FIFA, wamepata fursa nyingine ya kuonyesha jinsi ushirikiano wao ulivyoleta mapinduzi katika huduma za malipo na ushirikishwaji wa kifedha.

Kombe la Dunia la FIFA linawapa wababe hao wawili nafasi ya kuonyesha suluhisho lao la kisasa la malipo huku pia wakiboresha huduma kwa mashabiki huko Qatar.

Kadi za TemboCard Visa za benki sasa zinatumiwa kwa kiwango kikubwa na Watanzania kufanya ununuzi katika kumbi za Kombe la Dunia, hoteli, migahawa na kwa usafiri wa umma kuzunguka Qatar.

"Benki ya CRDB inajivunia kushirikiana na Visa ili kuwawezesha mashabiki wa soka waliopata fursa ya kupata furaha na msisimko wa Kombe la Dunia, kufanya malipo kwa urahisi kupitia TemboCard Classic, Gold, Platinum na Infinite. Kadi hizo zina thamani mbalimbali na kuongeza huduma kwa wateja," alisema Abdulmajid Nsekela, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB wakati wa mkutano wa kibiashara ulioandaliwa na Visa nchini Qatar.

Ushirikiano kati ya Benki ya CRDB na Visa unachukuliwa kuwa ni moja ya hatua muhimu zaidi katika kuendesha ushirikishwaji wa kifedha na kukuza uchumi Tanzania. Mnamo mwaka 2014, kampuni hizo mbili ziliungana kuzindua kadi ya benki iliyopewa jina la TemboCard Visa, kadi ya kwanza nchini kuwawezesha wateja kupata huduma popote walipo ndani na nje ya nchi.

Nsekela alibainisha kuwa benki imekuwa ikitumia muda mwingi na juhudi nyingi kwa kushirikiana na Visa na kurahisisha huduma za kibenki, pia kupanua ushirikishwaji wa kifedha miongoni mwa watu ambao kijadi hawakuwa na huduma za kibenki au za kifedha.

Alisema watu waliarifiwa jinsi TemboCard Visa inavyotumia ATM, vituo vya mauzo, na majukwaa ya ununuzi mtandaoni kuunganisha watumiaji na akaunti zao popote walipo.

"Tumewaingiza Watanzania wengi katika mfumo rasmi wa benki na shukrani kwa washirika wetu ikiwa ni pamoja na Visa.

"Ushirikiano wetu na Visa pia umeleta mapinduzi makubwa katika mfumo wa malipo wa Tanzania kwa kuwawezesha wateja kulipia huduma na ununuzi kwa kutumia kadi zao kama inavyotokea hapa Qatar," alisema.

Aliongeza kuwa ujumuishaji wa mifumo ya malipo ya kidijitali ni mojawapo ya vipengele vya ushirikiano wa taasisi hizo mbili ambazo zimewezesha kampuni na taasisi nchini kote kukubali malipo kwa kadi na mfumo wa msimbo wa QR.

Alibainisha kuwa teknolojia hiyo imeharakisha malipo na kuimarisha ufanisi wa ukusanyaji wa kodi kwa kuunganisha zaidi ya taasisi 4,000 za mashirika na za umma.

Kama sehemu ya kampeni ambayo Benki ya CRDB iliizindua mwanzoni mwa mwaka huu ya kuhimiza utumiaji wa uchaguzi wa malipo ya kidijitali na kuunga mkono juhudi za serikali za kuanzisha uchumi usio na fedha taslimu, wateja wanne wa TemboCard Visa walipewa fursa ya kuingia kwenye mashindano ya kihistoria ya riadha.

Wateja waliochaguliwa walipata matumizi muhimu na yasiyosahaulika ambayo yalijumuisha safari za ndege, visa, malazi na tiketi za Kombe la Dunia la FIFA pamoja na fursa ya kufurahia mengi zaidi na TemboCard Visa.

Ujumbe wa Benki ya CRDB nchini Qatar umetembelea vituo vya uvumbuzi kama sehemu ya mwaliko wake wa Kombe la Dunia la FIFA 2022 kama mmoja wa washirika wakuu wa Visa.

Pia ulipata nafasi ya kushuhudia mechi za hatua ya makundi kati ya Argentina na Poland na ile ya Japan dhidi ya Hispania.

## Wizara yaja na mkakati wa kukuza, kueneza Kiswahili

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TAKRIBANI watu milioni 250 ulimwenguni wanazungumza Kiswahili. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetaja mikakati yake ya kukuza na kueneza lugha hiyo ikiwamo kupandisha bango maalum la Kiswahili kwenye kilele cha Mlima Kilimanjaro.

Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof. James Mdoe, alitangaza mikakati hiyo jana jijini hapo alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu dhamira ya kukuza lugha hiyo kwenye mataifa mengine kwa kupandisha bango hilo lenye kaulimbiu 'Kiswahili Kileleni' kama sehemu ya maadhimisho ya miaka 61 ya Uhuru.

Alisema wizara inatarajia kuingia mikataba mitano na nchi mbalimbali ili zifundishwe lugha hiyo ili kuieneza zaidi duniani.

"Mwaka huu tutafanya maadhimisho ya miaka 61 ya Uhuru kwa namna tofauti, tutapandisha bango la Kiswahili Mlima Kilimanjaro, lengo ni kueneza Kiswahili kwa mataifa mengi zaidi kuliko ilivyo sasa," alisema.

Alitaja nchi ambazo zinazungumza kwa kiwango kikubwa lugha hiyo kuwa ni Uganda, Kenya, Sudani Kusini, Malawi na Mashariki ya Kongo.

Kiongozi huyo alisema lugha hiyo kwa sasa inapendwa na watu wengi na kuzungumzwa ikiwamo Misri, ikiwa moja ya nchi ambazo lugha hiyo inafundisha tangu mwaka 1964.

Alisema wizara itaendelea kutoa mafunzo mbalimbali yanayolenga kukuza lugha hiyo.

"Kuna vyuo 150 vinafundisha Kiswahili, pia redio na runinga 300 ulimwenguni ambazo zinarusha vipindi kwa lugha hii. Vyuo vya Tanzania vina makubaliano na vyuo vya nje kwa ajili ya kuendelea kufundisha lugha hii na tayari mikataba minne imeingiwa na wizara.

"Tunaendelea na mazungumzo na wizara hizo za nje ya nchi yakikamilika, mikataba mingine mitano itatiwa saini ili kuwezesha uanzishwaji wa madarasa ya kufundishia lugha hiyo nchini," alisema Prof. Mdoe.

Aliwataka wakuu wa taasisi na idara za wizara hiyo kuharakisha maongezi ambayo yanaendelea ili mafunzo hayo yaanze kutolewa.

Kuhusu nafasi ya Kiswahili kikanda na kimataifa, Mwalimu wa Kiswahili Misri, Menna Yasser alisema lugha hiyo inazungumzwa na watu wengi barani Afrika na yeye ameandika kitabu cha Kiswahili.

"Hii ni lugha ambayo mataifa mengi yanaitumia, kuna umuhimu wa kukuza lugha ya Kiswahili, hii lugha imenipa fursa nyingi na nimeisomea," alisema.

Meja Mwinyikombo Ally, mtunzi wa shairi la kueleza umuhimu wa kukuza lugha hiyo, aliipongeza wizara hiyo kwa namna ambavyo inakichukulia Kiswahili kama bidhaa inayouzika nchini na nje ya nchi.

## Sumbawanga yaanzisha operesheni darasa la kwanza

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

MKUU wa Mkoa wa Rukwa, Queen Sendiga, ameanzisha operesheni maalumu kuwatambua watoto wote wenye sifa za kuanza darasa la kwanza na kidato cha kwanza mwakani ili waweze kuripoti shuleni na kuanza masomo kwa wakati.

Agizo hilo alilitoa mwishoni mwa wiki wakati akiwa katika ziara ya kukagua ujenzi wa vyumba vya madarasa 50 unaoendelea katika Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga, mkoani humo.

Alisema kuwa hivi sasa ujenzi wa vyumba vya madarasa 191 utakaotumia Sh. bilioni 3.8 unaendelea katika halmashauri za mkoa huo, lengo ni kuhakikisha wanafunzi watakaofaulu kujiunga kidato cha kwanza pamoja na wanaoanza darasa la kwanza mwakani wanapata nafasi.

Alisema serikali inatimiza wajibu wake kwa kuandaa mazingira bora ya upatikanaji wa elimu, ni jukumu la wazazi kuhakikisha watoto wao wanafika shuleni wakiwa wamewanunulia sare pamoja na vifaa vingine.

"Najua ni lazima tuhakikishe kila mwanafunzi anaripoti shuleni, tutaanzisha operesheni maalumu kwenye kila kijiji ili kuwabaini watoto wenye sifa za kwenda shule na tuwabane wazazi watimize wajibu wao maana tusipofanya hivyo kuna watoto watakosa haki yao ya elimu," alisema.

Meya wa Manispaa ya Sumbawanga, Justine Malisawa, alisema Halmashauri ya Manispaa itawatumia viongozi wa serikali za mitaa, vijiji, vitongoji, watendaji kata pamoja na madiwani kuhakikisha wanawatambua watoto wote wanaopaswa kuanza shule mwakani.

Awali, akitoa taarifa ya maendeleo ya ujenzi wa madarasa 191 mkoani humo, Kaimu Ofisa Elimu mkoa, Matinda Mwinuka alisema utambuzi unaendelea vizuri kimkoa umefikia asilimia 73, huku Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo ikifikia asilimia 68, Nkasi (70), Sumbawanga Vijijini (76) na Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga asilimia 79.

# Wauzaji kuku waomba ushindani wa haki sokoni

**Na Maulid Mmbaga**

WADAU wanaojihusisha na uzalishaji na uuzaji wa vifaranga vya kuku wa kisasa nchini wameiomba serikali kuwawekea utaratibu mzuri utakaowawezesha kuwa na ushindani wa haki katika soko, wakidai kuwapo na uingizaji holela wa vifaranga kutoka nje na kuvuruga soko la ndani.

Siku chache zilizopita Nipashe ilipokea malalamiko kutoka kwa wafugaji na wauzaji wadogo wa kuku wa nyama, wakidai uingizwaji holela wa vifaranga unaowaharibia soko la ndani na kuwafanya wapate hasara katika uendeshaji wa shughuli hizo.

Akizungumza na Nipashe jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Kampuni ya Organia, Albert Momdjian, alisema kampuni hiyo imewekeza zaidi ya Dola milioni 30 katika sekta ya uzalishaji na uuzaji wa kuku nchini, huku akiiomba serikali kuwaruhusu kuuza vifaranga nje ya nchi kama wauzaji wengine wanavyoingiza kuuza nchini.

"Hatutaki kutengeneza uadui, ila tunachokitaka kuwe na ushindani wa haki sokoni tunaomba turuhusiwe kuuza nje pia, tunachotaka ni ubora na kuwe na usawa katika soko," alisema Momdjian.

"Uendeshaji wa shughuli za uzalishaji na ufugaji wa hawa kuku unagharama kubwa, tunalipia vibali na kodi ya serikali hivyo kwa gharama zote hizo sio haki kwenda kushindana na watu ambao wanaingia nchini na kuuza kuku bila kulipa kodi, wala mapato yoyote, jambo pekee tunaloliomba ni kuwe na ushindani wa haki," alisema Momdjian.

Alisema kukiwa na usawa na ushindani wa haki, itakuwa vizuri kwa kuwa itamfanya kila mtu kufanya ubunifu na kuongeza ubora wa bidhaa yake, akisisitiza sheria za uendeshaji wa shughuli hiyo zinapaswa kuheshimiwa na kila mmoja.

"Hapawezi kuwa na ushindani sawa endapo timu moja itakuwa na wachezaji 25 na nyingine kuwa na 12, sio sawa na hicho ndicho kinachotokea katika sekta hii, tunatakiwa kufuata sheria na kumkumbusha kila mmoja juu ya kufuata taratibu, tukiwa na wachezaji 12 kila upande, ambaye yuko vizuri ndio atashinda hatuna shida na ushindani wa haki," alisema Momdjian.

Pia alisema ushindani usiokuwa wa haki ndio tatizo kubwa linalowakabili kwa sasa, akieleza kuwapo uingizaji wa vifaranga na uuzaji unaoendelea usiofuata utaratibu, akilalamika mamlaka husika kutochukua hatua stahiki.

Alisema, uingizaji holela wa vifaranga unaenda kuvunja hali ya usalama nchini, akidai kuwa hiyo inaweza kusababisha kuingizwa kwa magonjwa kutokana na baadhi ya vinavyoingizwa kinyemela havipimwi wala kuangaliwa ubora.

**WAOMBA MNADA MAALUMU**

Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji wa Kuku, Costa Mrema, alisema ombi lao kubwa ni kupatiwa maeneo ya kufanya mnada kama ilivyo kwa wafugaji wa ng'ombe na mbuzi.

Alisema wameomba mnada huo ili waweze kudhibiti bei na kuepusha uuzwaji holela, akidai kuwa changamoto kubwa inayowakabili ni kuwapo kwa uingizwaji holela wa vifaranga jambo linalosababisha soko kuporomoka.

Alibainisha kuwa wafugaji wengi wanazalisha, lakini wanashindwa kupata soko, licha ya kupanda kwa bei ya chakula cha kuku, na kwamba haiendani na uuzaji wa kuku, akiomba serikali kudhibiti uingizaji holela wa vifaranga ili waweze kufanya biashara yenye faida.

"Pia tuliomba tuuze kuku kwa kilo na sio kwa kukadiria na macho, samaki, nyama ya ng'ombe na mbuzi ukienda kununua wanapimwa kwa kilo, lakini kuku hata awe amevimba kiasi gani bado utauza Sh. 5,500 na unakuta ana uzito wa takribani kilo mbili," alisema Mrema.

**UGUMU WA SOKO**

Naye Flora Kabote, mfugaji wa kuku kutoka kampuni ya Organic, alisema soko la kuku kwa sasa limekuwa gumu kwasababu vifaranga vinavyotoka nje vinauzwa Sh. 1,000 huku vya ndani vikiuzwa Sh. 1,700 mpaka 1,800, na kusababisha hasara kwa wazalishaji wa ndani.

"Hawa wanaochukua vifaranga vya nje ndio wanakuja kuuza hadi Sh. 5,000 na wale wanaonunua vya ndani wanauza 6,000 mkapa 6,500, kumkuza kuku hadi afikie kuliwa anagharimu hadi 6,300 sasa ili niweze kukidhi mahitaji yangu ni lazima niuze 6,500 hadi 6,700 ili nipate faida," alisema.



Ofisa Fedha Mkuu wa Benki ya DCB, Costantine Mtumbuka (kushoto), Meneja Fedha, Siriaki Surumbu (katikati) na Ofisa Masoko na Mawasiliano wa benki hiyo, Caroline Gabriel Nnko, wakionyesha tuzo ya mshindi wa kwanza wa uandaaji bora wa hesabu kwa mwaka 2021 katika kundi la benki ndogo na za kati zinatolewa na NBAA, baada ya kukabidhiwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu Zanzibar, Jamali Kassim Ali jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waathirika dawa za kulevya wadai kuchoshwa kutumika kama mitaji

**Na Boniface Gideon,** TANGA

WAATHIRIWA wa dawa za kulevya zaidi ya 2000 jijini hapo wamewatupia lawama baadhi ya wanaharakati na mashirika wanaowapiga picha wengine bila ruhusu katika maskani zao kwa madai ya kuwapelekea misaada.

Waathirika hao walifanya mkutano katika maskani yao kubwa eneo la Deep sea eneo maarufu kama 'Maskani' ambayo hukusanya watu mbalimbali ikiwamo wavuvi, wachuuzi wa samaki na wateja.

Mkutano huo ulilenga kujadili changamoto mbalimbali zinazowakabili waathiriwa wa dawa za kulevya ikiwamo kunyanyapaliwa na jamii, ukosefu wa ajira na mitaji ili wajikwamue kiuchumi.

Mwenyekiti wa waathiriwa hao, Hashim Nuru, alisema waathiriwa wa dawa za kulevya wanatumika kama mitaji kwa kukusanywa na kupigwa picha na kuzituma kwenye mashirika ya kimataifa kwa ajili ya kupata fedha.

"Sisi waathiriwa wa dawa za kulevya tumechoka kutumika kama mitaji ya watu kujipatia fedha kwani wengine, wanakuja hapa maskani kwetu wanatupiga picha halafu wanazituma huko nje ya nchi wanaingiziwa fedha kwa ajili ya kutusaidia, lakini hiyo misaada haitufikii sisi waathiriwa, tunasema hatutaki mwanaharakati yeyote hapa," alisisitiza.

Hashim alisema, wanahitaji usimamizi ili wapate mitaji ya kununua vitendea kazi.

"Wengi wetu kwa hapa Tanga Mjini ni wavuvi, lakini hatuna nyenzo za kutuwezesha kufanya shughuli zetu, tunadandia dandia tu mitumbwi ya watu, lakini nao wanatunyanyapaa na kutunyanyasa kwenye vyombo vyao, sisi tunaomba serikali na mashirika yatusaidie kazi za kufanya sio kutupiga piga picha hapa na kwenda kuzituma nje ya nchi kwa ajili ya kupata fedha," alisisitiza.

Sabina John, alisema ameacha matumizi ya dawa za kulevya na sasa amekuwa mtumishi wa Mungu na anakaa nao waathiriwa hao nakukutana changamoto zinazowakabili nyingi ikiwamo jamii kuwanyanyapaa.

"Mimi mwanzo nilikuwa mwalimu wa shule ya msingi, nilikuwa mtumiaji wa dawa aina nyingi kuzidi hawa, lakini sijaacha matumizi ya dawa za kulevya kwa kutibiwa au kulazimishwa, nimeacha kwa maombi ya watumishi kanisani pamoja na nasaha mbalimbali," alisema.

Alisema kwa muda mfupi aliokaa maskani, ameona changamoto mbalimbali zinazowakabili waathiriwa hao ikiwamo kufanywa mtaji mkubwa wa watu wengine kujipatia fedha, kutengwa na jamii, ukosefu wa ajira na pia viongozi wa dini hawana utaratibu wa kuwatembelea waathiriwa hao kwa ajili ya kuwapa mahubiri.

"Kama mimi niliacha kutumia dawa za kulevya kwa kupitia neno la Mungu basi naamini hata hawa wenzangu nao pia wataacha endapo watapewa neno la Mungu, nawaomba viongozi wa dini waje kuwatembelea waathiriwa," alisisitiza Sabina.

# USAID yatoa msaada vifaa chanjo polio milioni 42/-

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SHIRIKA la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID) kupitia Shirika la JHPIEGO Tanzania katika mradi wake wa MCGL limetoa msaada wa kompyuta mpakato (Laptop) saba na mashine ya 'photocopy' vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 42 kwa waratibu wa chanjo Mkoa wa Singida.

Kaimu Mkurugenzi wa Programu ya MCGL, Dk. Maryrose Giattas, alikabidhi kompyuta hizo kwa Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, wakati wa uzinduzi wa utoaji chanjo ya polio kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano iliyofanyika katika hospitali ya Sokoine Manispaa ya Singida.

Dk. Giattas alisema kompyuta hizo zitawasaidia waratibu wa chanjo Mkoa wa Singida kwa ajili ya kuweka kumbukumbu na kuingiza takwimu za chanjo kwenye mfumo pamoja na shughuli zao zote.

Mkuu wa Mkoa Singida, Serukamba alilishukru shirika hilo kwa msaada na kuwataka waratibu kuzitumia kompyuta hizo kwa malengo yaliyokusudiwa.

Naye Mratibu wa Huduma za Chanjo Mkoa wa Singida, Habibu Mwinory, alisema msaada huo ni muhimu utakaosaidia waratibu kuweka kumbukumbu vizuri kwenye kompyuta na kuongeza ufanidi wa kazi.

Mwinory alisema kwa Mkoa wa Singida, watoto 443,230 wenye umri chini ya miaka mitano wanatarajia kupatiwa chanjo dhidi ya ugonjwa hatari wa kupooza wa polio katika kampeni ya awamu ya nne.

Alisema katika kuhakikisha chanjo hiyo inafanikiwa dozi 478,000 zimesambazwa katika halmashauri zote saba za Mkoa wa Singida kuanzia Oktoba 31, mwaka huu.

Mwinory alisema siku ya kwanza (Desemba 1) ya kampeni hiyo watoto 126,875 walipatiwa chanjo sawa na asilimia 114 kiwango ambacho ni zaidi ya lengo la mkoa ni kutoa chanjo kwa watoto 110,807.5 kwa siku.



Mkuu wa Idara Rasilimali Watu wa Benki ya Exim, Frederick Kanga (katikati), akionyesha tuzo aliyokabidhiwa baada ya benki hiyo kuibuka mshindi kwenye Tuzo za Mwajiri Bora wa Mwaka 2022 (EYA 2022) kipengele cha usimamizi bora wa utendaji kazini zilizoandaliwa na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Benki ya Exim yaibuka mwajiri bora 2022

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Exim Tanzania imepata tuzo za mwajiri bora mwaka 2022 (EYA 2022) baada ya kuibuka kinara kwenye kipengele cha Mwajiri nchini (First Runner - up Local Employer).

Pia benki hiyo ilitangazwa kuwa mshindi kwenye kipengele cha usimamizi bora wa utendaji kazini (Perfomance Management).

Tuzo hizo zimetolewa mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE) na mgeni rasmi alikuwa Makamu wa Rais wa Tanzania, Dk. Phillip Mpango.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) Prof. Joyce Ndalichako.

Dk. Mpango aliwahimiza waajiri wote kuboresha maslahi ya wafanyakazi kulingana na nafasi zao huku akibainisha kuwa serikali imejipanga kuhakikisha sera na sheria za nchi zinakidhi vigezo vya ajira na waajiriwa.

"Natambua pia juhudi za ATE katika kuhakikisha inasimamia vyema majukumu ya pande zote yaani baina ya mwajiri na mwajiriwa katika sehemu za kazi. Hatutaki malalamiko ya wafanyakazi yafike juu kabisa tunataka waajiri mtoe haki na stahiki za wafanyakazi wenu kwa mujibu wa miongozi iliyoko," alisema.

Akizungumza baada ya kupokea tuzo hizo, Mkuu wa Idara wa Rasilimali Watu wa Exim, Frederick Kanga, alisema mfululizo wa tuzo hizo kutoka ATE ni kiashiria tosha mbele ya jamii kuhusu benki hiyo imewekeza kwenye rasilimali watu, hatua ambayo ina umuhimu katika kufanikisha malengo ya benki hiyo.

"Tuzo hizi kwetu ni mwendelezo wa sherehe zetu katika kuadhimisha miaka 25 tangu kuanzishwa kwa benki yetu. Katika maadhimisho hayo agenda ya rasilimali watu ilikuwa ni moja vya vipaumbele vyetu na leo hii tunakamilisha rasmi sherehe hizo kwa tuzo hizi muhimu zinazothibitisha dhamira yetu ya uwekezaji kwa wafanyakazi wetu," alisema Kanga.

Alibainisha kuwa moja ya vipaumbele vya benki hiyo ni pamoja na kuwaandaa watendaji wake kwa kuwaongezea ujuzi unaowawezesha kuwa mbele ya wakati katika utendaji wao ili kuleta matokeo bora na yenye ubunifu mpya kwa wateja.

"Lengo ni kuifanya taasisi yetu iwe sehemu ambayo mfanyakazi anakuwa bora zaidi, mwenye mabadiliko na mwenye utofauti," alisisitiza.

Kwa mujibu wa Kanga benki hiyo imedhamiria kuandaa wafanyakazi wenye ushirikiano katika kuunda timu imara ya pamoja kwa kuandaa mazingira ambayo wafanyakazi hao watajihisi kuwa wanathaminiwa, wanashirikishwa sambamba na kupewa fursa ya kukua na kujiendeleza kitaaluma.

## Ataka kuanzishwa programu wataalamu uuganishaji gesi

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

KATIBU Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Pro. Riziki Shemdoe, amesema ni vyema Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kibaha kikaanzisha programu ya ujuzi kwa wataalamu wa kuunganisha gesi kutokana na uhitaji katika eneo hilo.

Prof. Shemdoe alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki aliposhiriki mahafali ya 50 katika chuo hicho, Kibaha Mkoa wa Pwani na kati ya wahitimu waliotunikiwa vyeti walikuwapo zaidi ya 6,000 waliosoma kwa njia ya mtandao.

Alisema kwa sasa ni ulimwengu wa gesi, inatakiwa kuwa na wataalamu wengi ambao watafanya kazi ya kuunganisha gesi nyumbani pale watakapohitajika.

Alimwelekeza Mkurugenzi wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), Waziri Salum, kupeleka fedha katika chuo hicho ili mafunzo kwa njia ya mtandao yaendelee kutolewa.

"Wahitimu wa leo nendeni mkaunde vikundi muweze kupata mikopo kwenye halmashauri, nitatoa maelekezo kwa wakurugenzi kuwapa kazi zinapotokea kwa kuwa mna ujuzi na vyeti," alisema.

Prof. Shemdoe alisema serikali kwa mwaka imetenga Sh. bilioni 60 kwa ajili ya kutoa mikopo kwenye halmashauri nchini.

Wadau wa elimu wataendelea kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia. Kadhalika, alipongeza kundi la vijana 114 waraibu wa dawa za kulevya waliohitimu mafunzo kwa njia ya mtandao.

Mkurugenzi wa Shirika la Elimu Kibaha alisema Shirika hilo kwa sasa linakabiliwa na kikwazo cha uhaba wa vitendea kazi ikiwamo magari pamoja na uchakavu wa miundombinu na ufinyu wa bajeti ya maendeleo ya kawaida.

Mratibu wa mafunzo ya ufundi stadi kwa njia ya mtandao katika chuo hicho Dk. Rogers Jacob, alisema wanafunzi 6,157 walipata mafunzo hayo na kati yao 221 walitoka Unguja na Pemba na mhitimu mmoja alisoma kutoka Sudan.

Alisema kupitia mafunzo hayo wamebaini uhitaji mkubwa wa wanufaika katika mafunzo hayo na kujipanga kuendeleza utoaji wa elimu ya ubunifu na mtandao kuwezesha wengi kufikiwa na kunufaika.

Mmoja wa wahitimu kutoka kundi la waraibu wa dawa za kulevya, Kondo Rashid, aliishukuru serikali na Chuo cha Maendeleo ya Wananchi kwa kuwezesha kundi hilo kupata mafunzo yatakayowawezesha kuajiriwa na kujiajiri.

Mmoja wa wahitimu wa mafunzo ya ufundi stadi kwa njia ya mtandao, Msafiri Sanjito, alisema wakati wa mafunzo hayo walikuwa wakikumbana na kikwazo cha kushindwa kuingia kwenye mtandao kwa wakati kutokana na mtandao kuwa chini.



## ‘Serikali yanunua vitimwendo 365, vishikwambi 285’

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, amesema serikali imenunua viti mwendo 365 na vishikwambi 285 kwa ajili ya kuwawezesha wanafunzi wenye mahitaji maalum kufikia ndoto zao za kielimu.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki, wakati wa Siku ya Maadhimisho ya Watu wenye Ulemavu Duniani, ambayo kitaifa yalifanyika mkoani Arusha.

Alisema pamoja na kununua visaidizi hivyo, pia katika ajira 9,800 za walimu zilizotoka mwaka 2022, kati yake ajira 264 ya walioajiriwa ni walemavu, ambayo ni sawa na asilimia tatu.

“Hatuwezi kuwaacha watu wenye ulemavu, kwa sababu nao ni Watanzania. Na mengi zaidi mazuri yanakuja kwenu,” alisema Profesa Ndalichako.

Aidha, aliiagiza halmashauri zote kuhakikisha wanatenga na kutoa katika mapato ya ndani asilimia mbili ya fedha kwa walemavu na kuwatengenezea utaratibu rafiki wa kurudisha fedha hizo pale wanapokopeshwa.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela, alisema mkoa huo una watu wenye ulemavu 11,495.

Alisema kutokana na uwezeshwaji kiuchumi mpaka sasa vikundi 27 vya watu wenye ulemavu vimeshapatiwa Sh. milioni 174 na wameanzisha biashara mbalimbali. Mongela alisema: “Wengi wao siyo tegemezi tena kwa sababu fedha hizi zimewasaidia kuwa wajasiriamali na wanaendelea vizuri, hii pia inatoa ujumbe kwa wenzao wenye hali kama zao, kuwa wabunifu na kuachana na utegenezi ili wajikwamue kiuchumi.”

Mbunge wa Arusha, Mrisho Gambo, alisema kwa kuwa watu wenye ulemavu ni wenye matatizo mengi ni muhimu serikali inapoendelea kufanya maboresho ya bima ya afya kwa wote, ikaangalia jinsi ya kuwahudumia watu hao kwa upendeleo maalum.

# Mchungaji ataja siri ndoa nyingi kuvunjika mapema

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MCHUNGAJI wa Kanisa la Infinity Glory, Joel Senny, amesema ndoa nyingi zinazovunjika nchini zinasababishwa na baadhi ya viongozi wa dini kuhusika kuziharibu kwa sababu tu ya tamaa zao za kimwili.

Amesema baadhi ya viongozi hao wa dini wamekuwa wakitekeleza dhamira zao, huku wakijua kwamba vitendo hivyo vinachangia kuharibu taswira ya utumishi wao mbele ya umma na kufanya imani dhidi yao kushuka.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini Arusha wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu wimbi la viongozi wa dini kutumbukia katika dhambi ya kutenda matukio ya ukatili wa kijinsia.

“Tatizo hili la ndoa kuingiliwa na viongozi wa dini na kusababisha kuvunjika linapaswa kukemewa na kila mmoja kwani vitendo hivi vikiachwa viendelee vitakuwa chanzo cha mmomonyoko wa maadili na kuzalisha watoto wa mitaani.

“Baadhi ya viongozi wa dini wamekuwa wakianika uovu wao hadharani wanaoufanya ili kuaminika kuwa wanatoa msaada hasa kwa kundi la wanawake, ambalo limekuwa likiathirika na kujikuta wakibomoa ndoa zao, kwa kudhani viongozi hao wanawapenda zaidi ya waume zao,”alisema.

Kutokana na hali hiyo, Mchungaji Senny alisema iko haja kwa Watanzania kubadili mitazamo yao kwa kuacha unafiki na kuogopana na kisha kushirikiana na Jeshi la Polisi kufichua vitendo viovu vinavyofanywa na baadhi ya viongozi wa dini wasio waaminifu.

Alisema baadhi ya viongozi wa dini wanaingia katika tasnia hiyo kwa lengo la kujipatia maslahi binafsi, badala ya kutumia wito wa kutoa huduma, wao wamekuwa wakitumia kofia hiyo kukiuka maadili ya uongozi wa dini, hivyo kuchangia kuongeza kasi ya matukio ya jinai na ukatili wa kijinsia nchini.

Alisema: “Uwapo wa baadhi ya viongozi wa dini wasio waaminifu hivi sasa, chanzo chake kinatokana na kufuata historia za wakoloni. Jambo hilo limekuwa likichangia kuongezeka kwa maovu baina ya viongozi wa dini na washiriki wao.



Meneja Uhusiano na Elimu kwa Wanachama wa PSSSF, James Mlowe, akizungumza kwenye kikao kazi na wanachama wa Klabu za waandishi wa habari (hawapo pichani) jijini Arusha katika Ukumbi wa Kituo cha Mikutano cha Kimataifa (AICC), kushoto ni Kaimu Meneja wa Klabu za Waandishi wa Habari Kanda ya Kaskazini, Baraka Kitundu. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Ujenzi kisima wanufaisha wakazi 40,000 Simanjiro

**Na Allan Isack,** MANYARA

WANANCHI zaidi ya 40,000 wa Kimasai kutoka vijiji tisa vya Wilaya za Simanjiro na Kiteto, mkoani Manyara, wamenufaika na huduma ya majisafi na salama, baada ya kukamilika kwa ujenzi wa mradi wa kisima kirefu.

Mradi huo uliogharimu zaidi ya Sh. bilioni nne, umetekelezwa na Shirika lisilo la Kiserikali la Maendeleo ya Jamii la nchini Italia la OIKOS, kwa kushirikiana na Shirika la Ujamaa Community Resource Team (UCRT), Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) na Shirika la Maji na Maendeleo Dodoma.

Akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhi na kufunga mradi huo, Mwakili wa Balozi wa Italia nchini, Paolo Razzini, alisema mradi huo ni ishara nzuri ya uhusiano kati ya Tanzania na Italia.

Alisema tangu kuanzishwa kwa mradi huo na kuweka nishati ya umeme wa jua, umesaidia kusukuma mfumo wa kutoa maji, ambayo yatainufaisha jamii.

Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Makongoro Nyerere, akizungumza kabla ya kupokea mradi huo, alieleza kuridhishwa na utekelezaji wa mradi huo, akisema umetekelezwa mafanikio na kwa kiwango bora.


“Kwa niaba ya wananchi wa wilaya za Kiteto na Simanjiro napenda kutoa shukrani kwa uongozi wa Shirika la OIKOS kwa kufanikisha utekelezaji wa mradi huu kwa kushirikiana na washirika wenza kwa kuwa utakuwa mkombozi kwa wananchi,”alisema Makongoro.

Mbunge wa Simanjiro, Christopher Ole Sendeka, akitoa neno la shukrani kwa mfadhili hiyo, aliwashukuru wadau hao kwa kujenga mradi huo akisema kero ya maji ilikuwa kilio cha muda mrefu kwa wananchi wa maeneo hayo.

“Kwa kuwa mmekuwa pia mnashughulika katika miradi ya afya, elimu na mazingira ombi langu baada ya kuukamilisha mradi isiwe njia ya nyie kuondoka bali endeleeni kuwapo kwa kuwa mmeshafahamu hali yetu ilivyokuwa kwa kuwa jamii zetu ni za kifugaji hivyo zinahitaji maji kwa wingi kwa ajili ya kushwesha mifugo na matumizi ya nyumbani.

“Mtu anayekusaidia maji anakupenda sana hasa kwa sisi tunaotoka kwenye nyanda kame hakika mlilenga kwenye sehemu zenye uhitaji wa huduma kwa kiwango kikubwa na uhusiano ulioko kati ya nchi zetu hizi mbili muendelee na msichoke kutusaidia kwa ajili ya kusukuma maendeleo kwa wananchi, aliongeza Ole Sendeka.

Aidha, baadhi ya wananchi, akiwamo Christina Ngoiboi, ambaye ni Mkazi wa Ndedo, Kata ya Makame, Wilaya ya Kiteto, alisema katika kijiji hicho, awali kulikuwa na uhaba wa upatikanaji wa maji na wananchi walikuwa wakitembea umbali mrefu zaidi ya kilomita 14 kwenda na kurudi kufuata huduma hiyo.





# Watanzania takribani 132,000 huambukizwa TB kila mwaka

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

KANZIDATA ya wagonjwa wanaougua kifua kikuu na kifua kikuu sugu (TB), inaonyesha kuwa watu 132,000 kila mwaka huambukizwa ugonjwa huo nchini na kila siku hufariki watu 72.

Mkurugenzi wa Hospitali ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi ya Kibongoto, Dk. Leonard Subi, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa uzinduzi wa kampeni ya upandaji miti katika hospitali hiyo inayotekelezwa na Taasisi ya kimkakati ya Siha Sports Agency.

Alisema ili kukabiliana na tishio la ugonjwa huo iko haja ya kuwahamasisha zaidi Watanzania kupanda miti kwa wingi kwenye maeneo yanayowazunguka kwa ajili ya kuzalisha hewa ya Oxygen inayohitajika kwenye mapafu.

"Miti inayopandwa na Siha Sports Agency, itaenda kuzalisha hewa ya oxygen katika hospitali hii. Nitoe wito kwa wananchi kushiriki kutokomeza kifua kikuu kwa kutambua dalili za kifua kikuu, ambazo ni homa, kupungua uzito, kutokwa na jasho usiku, kukohoa na kuwa na makohozi mengi pamoja na kupoteza uzito kwa haraka.

"Tunayo kila sababu, tunaposema tutokomeze kifua kikuu, tuimarishe sekta zote ikiwamo utunzaji sahihi wa mazingira, ni kwa sababu ni njia mojawapo ya kutokomeza ugonjwa huu hatari. Dawa pekee haiwezi kutokomeza TB, bali ni pamoja na kutunza mazingira, kukaa kwenye nyumba zenye mzunguko wa hewa nzuri, lakini kufanya mazoezi kama Siha Sports Agency, ambavyo imekuwa ikifanya kila Desemba 26, na haya yote ndiyo yatakayofanya TB isiendelee kuwa tishio. Ni lazima tuungane kwa mbinu zozote zile ili kutokomeza ugonjwa wa kifua kikuu," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, aliagiza Halmashauri ya Wilaya ya Siha, kushirikiana na wadau wa mazingira, wakiwamo Siha Sports Agency, kupanda miti katika maeneo yenye ukame mkali, hasa ukanda wa tambarare ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi yanayoendelea kuwatesa binadamu na mifugo kwa sasa.

Katika kampeni hiyo, Babu, aliwakilishwa na Mkuu wa Wilaya ya Siha, Thomas Apson.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Dancan Urassa, alisema wilaya hiyo inatishiwa na tatizo katika baadhi ya maeneo kukosa miti, hasa ukanda wa tambarare kuania West Kilimanjaro, Kata za Ormelili, Donyomurwa, Orkolili, Makiwaru na Karansi, ambazo zinakaliwa na idadi kubwa ya jamii za kifugaji na wakulima.

Alisema: "Kampeni hii ya upandaji miti katika wilaya yetu, inaratibiwa na Taasisi ya Siha Sports Agency, na miti 15,000 tunayoipanda imetolewa na TFS (Wakala wa Misitu Tanzania). Niseme katika wilaya yetu lipo tatizo kwa baadhi ya maeneo, ambayo hayana miti na huko ndiko pia kuna wakulima wengi wanaolima mazao ya mahindi na maharage. "Kukosekana kwa miti katika ukanda huo, kumesababisha tatizo la ukame kuwa mkali zaidi. Wafugaji huko hawana malisho ya mifugo, ndio maana tumesema tunaenda kuweka utaratibu kwa mwaka tutaotesha miti 500,000. Tutaisambaza vijiji vyote vilivyoko vya Siha."

Mwenyekiti wa Siha Sports Agency, Selina Mkonyi, alisema ili kukabiliana na uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi yanayoendelea kwa sasa ni vyema miti yote iliyooteshwa na wananchi au taasisi mbalimbali ifuatiliwe kwa kutumia kifaa hicho.



Ofisa Mkaguzi Msaidizi wa Jeshi la Polisi, Allen Chittunda, kutoka Idara ya Elimu Kikosi cha Usalama Barabarani mkoani Kilimanjaro akitoa elimu ya matumizi sahihi kwa watumiaji barabara ikiwamo wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Lyasikika, mwishoni mwa wiki. **PICHA: JAMES LANKA**

# Wakazi Sanya Juu kupiga kura kuwafichua wauza gongo, bangi

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

KAMPENI ya kupambana na uuzaji wa dawa za kulevya aina ya bangi na pombe ya gongo katika Mji Mdogo wa Sanya Juu ulioko Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro, itaendeshwa kwa kupiga kura za siri baada ya majina ya wafanyabiashara kuorodheshwa.

Uamuzi huo ulitangazwa mwishoni mwa wiki na Diwani wa Sanya Juu, Juma Jani (CCM), baada ya kuitisha kikao cha dharura cha viongozi wa kata hiyo.

Pamoja na mambo mengine, kikao hicho kilichofanyika Ofisi ya Kijiji cha Sanya Juu, kiliketi kujadili madhara yanayoendelea sasa ya idadi kubwa ya vijana kulewa pombe kupindukia nyakati za asubuhi, wengine kugoma kufanya kazi na kukaa vijiweni wakiwa hawajielewi, huku baadhi wakijiingiza kwenye uhalifu. "Jamani tumelazimika kuitana hapa, kwa sababu hali ilivyo sio nzuri kwenye kata yetu. Ndio maana nimewaita viongozi wote pamoja na wajumbe wa halmashauri ya kijiji, kujadili ustawi wetu na hali ya usalama ndani ya kata yetu. Watu wanauza bangi hadharani bila kuwa na hofu yeyote," alisema.

Kutokana na hali hiyo, Diwani Jani, aliagiza watendaji wa vijiji na kata hiyo, kuanza kupita nyumba kwa nyumba kuorodhesha majina ya watu wanaofanya biashara ya kuuza bangi na pombe ya gongo ili waitwe na kupewa onyo la mwisho kabla ya majina hayo kupelekwa kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Siha (OCD) kwa ajili ya hatua nyingine za kisheria.

Kwa mujibu wa Diwani Jani, shule iliyo katika hatari zaidi ya wanafunzi wake kuharibika na kukatisha masomo kutokana na hali hiyo ni Shule ya Sekondari Kilingi, ambayo wanafunzi wake walikamatwa wakitumia dawa hizo za kulevya wakati wa mapumziko shuleni.

Zakaria Materu, Mkazi wa Sanya Juu, akizungumzia tatizo hilo, alisema vitendo hivyo vinafanywa wazi wazi na vijana kwenye jengo moja la serikali liliko Soko la Sanya Juu na maeneo mengine karibu na hapo.

Alipoulizwa Ofisa Polisi Kata ya Sanya Juu, kuhusu tuhuma hizo, Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Juma Hannu, alisema tayari amepokea taarifa hizo na wameanza kutafuta wahusika wanaowauzia vijana hao dawa za kulevya ili wakamatwe na kufikishwa mahakamani kujibu tuhuma zinazowakabili.

# Chuo Kikuu Arusha chaanza kuwapika wahitimu wajiajiri

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Chuo Kikuu cha Arusha, Dk. Mark Malekana, amesema wameanza kuwapika vijana nje ya taaluma yao ili waweze kujiajiri katika sekta ya kilimo.

Amesema wamefikia hatua hiyo kutokana na wahitimu wengi wanaomaliza elimu ya juu nchini kukosa ajira serikalini pamoja na sekta binafsi.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa mahafali ya 16 ya chuo hicho. Katika mahafali hayo zaidi ya wahitimu 300 walihitimu astashada, stashahada na shahada ya uzamivu.

Alisema kwa kuwa kuna fursa kwenye kila tatizo, wameona ni vyema kuwasukuma vijana kuongeza ushiriki wao katika kilimo, kwa kuwapatia mafunzo, kuwafunda njia za kupita ili kupata mitaji na kuwaunganisha na fursa za masoko.

"Vijana wetu fursa ni nyingi nchini kwetu, sekta ya kilimo inabeba fursa zaidi ya asilimia 50, kitendo cha serikali kuzindua mpango mkakati wa vijana kuingia kwenye sekta ya kilimo ni mpango unaolenga kuboresha uchumi wa mtu mmoja mmoja kuanzia umri wa vijana," alisema.

Kabla ya Dk. Malekana kudokeza kuhusu mkakati huo, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Kitojo Wetengere, alisema mikakati ya chuo hicho kwa sasa ni kuhakikisha vijana wanatumia fursa ya kujiajiri, hasa kwenye sekta ya kilimo.

"Vijana wanahitaji kuandaliwa vizuri ili waelewe wanalima nini, mtaji watapata wapi, watauza wapi na hayo yote yanawezekana kukiwa na utashi wa kisiasa. Ninaamini serikali ikiweka mazingira mazuri, vijana wengi watavutika kujiunga kwenye kilimo na nchi itapiga hatua kiuchumi.

"Kingine ni matumizi ya teknolojia katika kilimo. Vijana wa sasa huwezi kutegemea wavutike kulima kwa jembe la mkono na hivyo ni muhimu sana kuwawezesha mitaji kwa kuwaunganisha na benki ili walime kwa teknolojia," alisema.

Mbunge Prof. Shukrani Manya, aliyepewa nafasi ya kutoa neno kuhusu wahitimu hao, aliwapa somo wahitimu hao kutumia maarifa na ujuzi wanaopata vyuoni, kufikia viwango vya ushindani wa soko la ajira katika ukanda wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Alisema: "Kuna umuhimu wa vijana kuendelea kukuza maarifa yao na kusaidia wengine, kwa kuwa wanahitaji kushindana ndani ya nchi na kimataifa. Tunalo tatizo kubwa la ajira kwa vijana wanaohitimu elimu ya juu katika vyuo mbalimbali, na wengi wao hawataki kazi nyingine zaidi ya kusubiri kuajiriwa serikalini.

"Mkimaliza vyuo vikuu msiende kukaa nyumbani kusubiri ajira, hapana! Nendeni mkajitolee kwenye jamii kwa kutatua matatizo yanayowakabili. Na kwa kufanya hivyo mtaongeza ujuzi na maarifa yenu na mwisho wa siku mtajikuta mnamudu ushindani kwenye soko la ajira nchini na kimataifa."

Nipashe

# Spotika



TOFAUTI SABA KATI YA MESSI NA RONALDO UK.16 - 17



## ISIKUPITE

Lionel Messi ametwaa zaidi Tuzo ya Mchezaji Bora wa Mechi kwenye michuano ya Fifa (mara 8) kuliko mchezaji yeyote katika historia ya mashindano hayo. Lakini kwa sasa Messi anashika nafasi ya pili kwa ufungaji bora kwa Argentina kwenye Kombe la Dunia akiwa na mabao tisa moja nyuma ya kinara Gabriel Batistuta, huku Diego Maradona akishika nafasi ya tatu kwa mabao yake nane.

## PATASHIKKA...

Lionel Messi akipata upinzani mkali kwa beki wa Australia, Harry Souttar, wakati wa mechi ya hatua ya 16-bora ya Kombe la Dunia iliyopigwa Qatar juzi na Argentina kutinga robo fainali baada ya kushinda 2-1. **PICHA: MTANDAO**

# VIUNGO KUMI BORA HATUA YA MAKUNDI KOMBE LA DUNIA

**DOHA,** Qatar

HUKU hatua za makundi zikiwa zimekamilika na sasa michuano ya Kombe la Dunia ipo hatua ya mtoano ya timu 16-bora na ilianza rasmi juzi, Jumamosi.

**Tumekuwa na muda mwingi wa kuchanganua msururu wa uchezaji bora wa viungo.**

Kwa hiyo, ni wakati gani mzuri zaidi kuliko sasa, kabla ya mchujo, kuwahukumu wachezaji wa kati wanaofanya vizuri zaidi? Acha tuwaangalie wale waliofanya vizuri zaidi kwenye hatua ya makundi ya michuano hiyo mikubwa zaidi duniani...

**#10. SOFYAN AMRABAT (MOROCCO)**

Kwa pande zote zinazopendekezwa Morocco haikuonekana kuwa na nafasi kubwa kwenye Kombe la Dunia la 2022. Lakini kile ilichofanya kwenye hatua ya makundi kimetoa tafsiri tofauti kabisa.

Sofyan Amrabat amekuwa muhimu kwa hilo, na anawekwa nafasi ya 10 kati ya viungo bora zaidi kwenye hatua ya makundi.

**#9. MATEO KOVACIC (CROATIA)**

Hakuweza kupata bao dhidi ya Ubelgiji, lakini haikuwa kwamba hakujaribu. Mateo Kovacic alikuwa wa kiwango cha juu tena kwa Croatia, na ni muhimu kwao kuingia ndani ya dimba kwa mara nyingine tena.

**#8. GAVI (HISPANIA)**

Gavi alivumilia usiku wao usio sahaulika dhidi ya Japan katika mechi yao ya tatu na walipoteza kwa kufungwa mabao 2-1.

Ingawa hakuwa peke yake, lakini kiwango alichoonyesha kwenye hatua hiyo ya makundi kinamfanya kuwa mmoja wa viungo bora kabisa.

**#7. FRENKIE DE JONG (UHOLANZI)**

Onyesho la kifahari sana kutoka kwa Frenkie de Jong katika mechi tatu za makundi.

Kadiri mashindano yanavyoendelea, unaweza kumuona akiendelea kujiamini na baadaye kuwa na ushawishi mkubwa kwa kikosi hicho cha 'Oranje'.

**#6. PEDRI (HISPANIA)**

Ilikuwa habari sawa na Gavi kwa Pedri dhidi ya Japan. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, hakufurahia mchezo wake bora, lakini ataendelea kuwa tegemeo kwa 'La Roja' katika kipindi chote cha hatua ya mtoano.

**#5. JUDE BELLINGHAM (ENGLAND)**

Kocha Gareth Southgate amegundua kuwa kiungo bora zaidi wa England ni Jude Bellingham na ndio maana ana mpa nafasi ya kucheza.

Katika hatua ya makundi Bellingham ameonyesha kiwango cha kuvutia zaidi na kuwa mmoja wa viungo bora kabisa.

**#4. TYLER ADAMS (MAREKANI)**

Mchezaji huyo wa Leeds United amekuwa na wakati wa kuvutia kama nahodha wa Marekani kwenye michuano hiyo. Kiasi kwamba ikiwa anaweza kurudisha kiwango hiki katika msimu wa ligi, haitashangaza kuiona Leeds ikiwa kwenye wakati bora zaidi.

**#3. BRUNO FERNANDES (URENO)**

Baada ya matokeo mazuri katika mechi mbili za makundi, Fernandes alikaa benchi huku Ureno ikipoteza kwa Korea Kusini.

Nyota huyo wa Manchester United amekuwa nguzo muhimu zaidi kwenye kikosi cha Ureno hadi sasa.

**#2. ALEXIS MAC ALLISTER (ARGENTINA)**

Mchezaji huyu wa Brighton anaendelea kufanya vema na alifunga bao lake la kwanza akiwa na Argentina dhidi ya Poland.

Licha ya golikipa wa Poland, Wojciech Szczesny kuwa kwenye ubora mzuri, lakini Allister alikuwa kwenye kiwango cha kuvutia zaidi na kumfunga.

**#1. CASEMIRO (BRAZIL)**

Kwa ustadi wote ambao Brazil wanao, wanamhitaji Casemiro kufagia ipasavyo na kuongeza ubavu. Anafanya hivyo kwa njia bora kabisa. Mtu huyu ni muhimu zaidi kwa Brazil hasa wakati huu wa mtoano.



CASEMIRO



# CHOMELO: NYOKA ALIVYONIPELEKA SOKA LA WENYE ULEMAVU

Na Saada Akida

MUNGU hakupi kilema akakukosesha mwendo! Msemo huo ndio unaoweza kuutumia pindi tu unapoanza kukizungumzia kipaji cha mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Tanzania kwa Watu wenye Ulemavu (Tembo Warriors), Ramadhan Ally Chomelo, anayecheza soka la kulipwa katika Klabu ya Konyaspor ya Uturuki.

**Hakika unaweza ukapata tatizo kubwa katika maisha yako ikiwamo ulemavu usiotarajiwa na kukukatisha tamaa katika kufanikisha malengo yako uliyojiwekea, lakini ukitia nia kamwe huwezi kushindwa, na hivyo ndivyo ilivyo kwa Chomelo ambaye ni mlemavu wa mguu.**

Katika mazungumzo maalum kwa njia ya simu akiwa Uturuki, Chomelo ambaye ni mzaliwa wa Wilaya ya Handeni mkoani Tanga, anasema safari yake kielimu ilianzia Shule ya Msingi Birikani iliyopo wilayani humo kabla ya kuhitimu na kufaulu na kujiunga na Sekondari ya Pugu iliyoko Ilala jijini Dar es Salaam ambapo alisoma hadi kidato cha nne.

### NYOKA CHANZO CHA ULEMAVU

Chomelo anasema alizaliwa akiwa mzima, lakini hali hiyo ya ulemavu aliipata kutokana na kung'atwa na nyoka wakati huo akiwa na umri wa miaka minne.

"Kipindi hicho nilikuwa na utaratibu wa kuamka asubuhi kumsindikiza baba wakati anaenda kazini, hivyo siku hiyo baba alinidanganya na kunitaka nimsubiri katika kiti ndani, nilifanya hivyo wakati nimekaa kumbe chini kulikuwa na tambara la kufutia miguu na chini yake kulikuwa na nyoka kajificha.

"Yule nyoka alining'ata niliposhusha miguu, lakini sikujua zaidi ya kuona damu zinatoka na kupata maumivu makali, nililia sana. Mama alipofika pale na kuangalia chini ya kiti hakuona kitu na kuhisi ni paka amenikwangua katika mguu wangu.

"Nilipelekwa zahati pale Pangani, kutokana na kucheleweshwa sumu ilizidi kupanda na mguu kuendelea kuharibika, hivyo daktari akashauri nipelekwe hospitali ya mkoa.

"Bahati nzuri nilipofika hospitali hapo na kupokelewa na daktari aliponiona alimuomba baba achangue moja kati ya mwili, nikatwe mguu ama akihofia basi nitakufa maana sumu ilianza kusambaa eneo kubwa, ndipo uamuzi wakukatwa ukafanyika."

### SAFARI KISOKA

Chomelo anasema alipenda soka tangu alipokuwa shule ya msingi, kabla ya hata kujua kama kuna mpira wa watu wenye ulemavu (Amputee), lakini ilikuwa inamuwia vigumu kutokana na shule aliyokuwa akisoma wakati huo hakuwa na mlemavu zaidi yake.

"Nilipokuwa shule ya msingi mlemavu nilikuwa peke yangu, hata nikienda kucheza mpira na wenzangu walikuwa wakiniambia nisicheze kutokana na kuhofia kuniumiza. Lakini sikujali niliwalazimisha, nicheze basi maisha yakaendelea, habari nzuri nilifanikiwa kufanya vizuri na kufaulu, hivyo kuchaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari Pungu.

"Nilichofurahia nilipokuwa Pugu, nilikutana na watu ambao asilimia 35 walikuwa ni wenye ulemavu. Kipindi cha michezo wanafunzi wenye ulemavu walitengwa eneo la uwanja wao kwa ajili ya kucheza michezo mbalimbali na wengi wao walipenda soka.

"Tukiwa kidato cha nne walikuja Wazungu kutoka Ireland na kurasimisha mchezo wa soka kwa watu wenye ulemavu maarufu kwa jina la Amputee. Walipofika nchini wakaanza kusaka vipaji moja kwa moja kutembelea shule mbalimbali ikiwamo Pugu katika mchakato huo uliongozwa na Rais wa Shikikisho la Mchezo huu, Peter Sarungi.

"Kipindi hicho tulikuwa tunaishi shuleni (boarding) nakumbuka tulikuwa na mafunzo ya siku tatu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

"Baada ya hapo, wale waliokuja kutoa mafunzo hayo walisisitiza kuwapo kwa klabu, zilipatikana nne, nilisajiliwa na Klabu ya L.S.L, ambao ni mabigwa watetezi baada ya kutwaa ubingwa mara tatu," anasema.

### JINA LA CHAMA BONGO

"Unajua aina ya uchezaji wangu katika nafasi ya kiungo mshambuliaji, mashabiki wa soka la watu wenye ulemavu, wakanipa jina hili kwa kunifananisha na anavyocheza Clatous Chama, mchezaji wa Simba.

### MECHI ASIYOISAHAU

Anasema msimu uliopita mechi kati ya timu yake ya Kayseri na Basanker ilikuwa ya kuamua nani apande Ligi Kuu kwa sababu zote zilikuwa Ligi Daraja la Kwanza Uturuki kabla ya yeye kujiunga na Klabu ya Konyaspor

"Mechi hiyo ilikuwa fainali, dakika ya tano tukafunga bao la kwanza lililodumu hadi mapumziko tukarudi kipindi cha pili dakika ya 72 wakatufunga la pili, kabla ya mimi kufunga la kwanza dakika ya 77 na dakika tatu baadaye nikatoa pasi ya bao la pili.

"Dakika ya 83 nikafunga bao tatu baada ya hapo tulionyesha ushindani mkubwa na dakika ya 87 nikafunga bao la nne, nikakamisha hat-trick yangu katika mchezo huo, kabla ya timu yake kufunga bao la tano na kisha akasababisha penalti iliyozaa bao la sita na mechi kumalizika kwa ushindi wa 6-2 huku nikiwa nyota wa mchezo na ndipo aliposajiliwa na Konyaspor."

### NDOTO ZAKE KISOKA

"Ni kufika mbali kabisa na niweze kuwa 'super star' (nyota mkubwa) duniani katika mpira huu na ndoto yangu zaidi ni kucheza soka katika Ligi Kuu ya Uingereza kwa Amputee," anasema Chomelo.

---

**NJE YA UWANJA**

KUNA timu nyingi zaidi ambazo zimekabiliwa na kampeni za Kombe la Dunia zenye alama sifuri, ingawa rekodi yao si ya kiufundi kati ya timu mbaya zaidi, Qatar imeingia kwenye orodha hii kwa kuwa taifa mwenyeji lenye rekodi mbaya zaidi katika historia ya mashindano hayo baada ya kumaliza bila pointi yoyote.

FIFA WORLD CUP Qatar2022

# TOFAUTI 7 KATI YA MESSI NA RONALDO

**LONDON,** England

KWA wengine, Lionel Messi ndiye mchezaji bora zaidi kuwahi kutokea na kwa wengine, Cristiano Ronaldo yuko juu. Jambo ambalo haliwezi kukanushwa ni ukweli kwamba wachezaji hawa wote wawili ni bora zaidi kwa kizazi chao, na kwamba hakuna mtu mwingine anayekaribia kiwango walichonacho.

**Kinachofanya ushindani wao kuwa mgumu zaidi ni kwamba licha ya kuwa wafungaji mabao, wote ni tofauti kabisa. Wakati Messi ana ufundi zaidi, Ronaldo anategemea nguvu na mazoezi ya kutosha.**

Takribani kila kipengele cha mchezo wao kinatofautiana kabisa na kile cha wengine, na hapa tunaangalia tofauti hizo, twende sasa...

**#1. KUMALIZA**
**Cristiano Ronaldo**

Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, wawili hawa wamefunga mabao mengi kuliko timu nyingi zikijumlishwa. Na kwa sababu hii kwamba hakuna aliyeshika nafasi mbili za juu za Ballon d'Or katika miaka mitano iliyopita.

Mreno ni mkamilishaji imara - ni nguvu yake kubwa. Iwe kutoka pembeni ngumu zaidi au umbali mrefu zaidi, mtu anaweza kuweka dau la maisha yake kwa Cristiano Ronaldo ili afunge bao kwa dakika moja ya kupata nafasi ya kufunga. Anategemea sana nguvu ili kuhakikisha kwamba mashuti yake yanaishia mwisho.

**Lionel Messi**

Huku Mreno huyo akitumia nguvu kumalizia mikwaju yake, Muargentina huyu anapendelea kuweka mashuti yake kwa usahihi na hufanya hivyo kwa ukamilifu karibu kila mara. Mbinu nzuri na usahihi wa mshindi mara saba wa Ballon d'Or humruhusu kupiga mikwaju yake kutoka katika hali yoyote.

Uimara wake huu umemruhusu kufunga mabao mengi sana na ataendelea kufanya hivyo kwani mbinu huwa hazipungui kadiri umri unavyoendelea, huwa bora kama mvinyo.

**#2. Kupiga chenga**
**Cristiano Ronaldo**

Hapo mwanzo Cristiano Ronaldo alikuwa mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani. Wakati akiwa Sporting na Manchester United, alikuwa akichomoa mpira kutoka kwa kina kirefu na kupiga chenga kuwapita wachezaji wengi na kufunga. Mpira wake wa kimtindo huru uliharibu usiku wa mabeki wengi.

Lakini hayuko sawa kwa sasa kwani ni nadra kupata chenga moja iliyofaulu siku hizi. Shida ni kwamba mtindo wake wa kucheza unatabirika.

**Lionel Messi**

Lionel Messi ndiye mpiga chenga bora zaidi duniani. Udhibiti wake wa karibu wakati wa kupiga chenga unashangaza sana na huwafanya watu washangae jinsi anavyofanya. Mpira unaonekana kushikamana na miguu yake - kana kwamba alizaliwa nao.

Huu ndio uwanja ambao Lionel Messi ni bora kuliko Cristiano Ronaldo - au mchezaji yeyote kwa suala hilo na huacha nafasi ndogo ya mjadala.

**#3. Vichwa**
**Cristiano Ronaldo**

Yeye anajua sana kuruka. Mreno huyo labda ndiye aliye na kiwango kikubwa zaidi katika mchezo kwani anahisi kama anaelea angani akiwa ndani. Mbinu yake nzuri ya kuruka inamruhusu kukaa hewani kwa muda na kichwa chake cha usahihi kinamruhusu kuweka mpira wavuni kwa usahihi.

Katika kipengele hiki, Cristiano Ronaldo ni bora zaidi kuliko Lionel Messi.

**Lionel Messi**

Kipengele pekee cha mchezo wake wa jumla kinachotuacha tukitaka zaidi ni uwezo wake wa angani. Lionel Messi anaweza kufanya kila kitu, isipokuwa kufunga kwa vichwa mara kwa mara. Ingawa amefunga baadhi ya mabao ya vichwa, yuko mbali na kile ambacho mtu anaweza kukiita kama nguvu ya anga. Ufupi wake ndio sababu pekee ya hii kwani kuna shaka kidogo kwamba angekuwa mzuri angani ikiwa angekuwa na urefu wa inchi zaidi.

Ameonyesha kuimarika kwa idadi akifunga mabao machache ya vichwa msimu huu, lakini kwa vyovyote vile ni mahiri hewani.

**#4. Pasi**
**Cristiano Ronaldo**

Nyuma katika siku zake za Manchester United, hii ilikuwa ni kitu ambacho alifanya mara nyingi. Alipendelea kucheza chenga zaidi kuliko kuwapasia wenzake. Akiwa Real Madrid mtindo wake wa uchezaji ulibadilika sana na alikuwa akiwapasia wachezaji wenzake zaidi ya alivyokuwa akifanya hapo awali.

Pasi zake hata hivyo, si ubunifu kama inavyopaswa kuwa kwa mchezaji wa kiwango chake. Ni nadra sana kutoa pasi ya moja kwa moja. Baada ya miaka mingi ya kucheza soka kileleni, inaweza kuhitimishwa kuwa huu ni upungufu mkubwa katika mchezo wake jambo ambalo linamgharimu sana kuthaminiwa.

**Lionel Messi**

Kuna wachezaji wachache sana duniani wanaoweza kupasisha mpira kwa ufasaha kama Lionel Messi anavyoweza katika nafasi ya tatu ya mwisho. Muargentina huyo ni gwiji wa kutengeneza nafasi za wachezaji wenzake kwa kuteleza katika pasi mbaya za ulinzi zinazosambaratisha safu ya ulinzi ya timu nyingi.

Udhibiti wake wa karibu usio wa kweli humruhusu kupiga pasi kutoka kwa nafasi zilizobana zaidi na uwezo wake wa kuona humpa usahihi unaomfanya afaulu.

**#5. Kasi**
**Cristiano Ronaldo**

Moja ya vipengele hatari zaidi vya mchezo wake ni kasi. Anaweza kumshinda karibu kila beki aliyepo katika soka la dunia. Nguvu zake za ajabu za misuli ya paja humruhusu kuwa na kasi kwa hatua ndefu.

Mtindo wake wa kukimbia ni mzuri sana wakati kuna nafasi ya bure ya kukimbia. Lakini kwa sasa nafasi hiyo ni ndogo, mara chache anaweza kufanya hivyo.

**Lionel Messi**

Ingawa Muargentina huyu pia ni mwepesi, mtindo wake wa kukimbia ni tofauti sana. Anakimbia kwa hatua fupi - kama mtu anavyoweza kutarajia kutoka kwa urefu wake na hiyo inamruhusu kujipinda na kugeuka zaidi na kusababisha uharibifu dhidi ya ulinzi.

Mtindo huu wa kukimbia ndio unamruhusu yadi ya ziada na kuonekana karibu kutoweza kushika kasi.

**#6. Mguso wa Kwanza**
**Cristiano Ronaldo**

Mguso wa kwanza ni sehemu muhimu ya ustadi wa mchezaji. Inatofautisha nzuri na bora. Mguso mzuri wa kwanza ni ishara ya mchezaji mwerevu. Mtu yeyote ambaye amecheza mpira kidogo angejua jinsi ilivyo ngumu kudhibiti pasi inayoingia.

Mguso wa kwanza wa Cristiano Ronaldo ni mzuri. Anaweza kupokea mpira na kudhibiti, lakini si mara kwa mara kutengeneza nafasi. Hata hivyo, anapopiga shuti, mchezaji huyo bora anakuwa maarufu kwani amefunga mabao ya kushangaza kwa mguso wake wa kwanza - kitu ambacho ni yeye pekee anayeweza kufanya vyema zaidi.

**Lionel Messi**

Linapokuja suala la mguso wa kwanza, kuna wachache bora kuliko Lionel Messi. Kwa mguso wake wa kwanza, anawapiga mabeki na kutengeneza nafasi kwa ajili yake. Ufahamu wake wakati akipokea mpira katika mazingira ya pasi ni wa ajabu.

Hata hivyo, karibu na goli, mguso wake wa kwanza kufunga si mzuri kama Mreno. Ufahamu wa Cristiano katika matukio haya ni bora zaidi kuliko ule wa Messi.

**#7. Nguvu ya mguu dhaifu**
**Cristiano Ronaldo**

Mguu wa kushoto wa mchezaji huyo wa zamani wa United una nguvu sawa na wa kulia linapokuja suala la upigaji mpira. Nguvu anazopata kutokana na mguu wake unaodhaniwa kuwa dhaifu wakati anapopiga mpira huwaacha wengi wakishangaa.

Lakini haitumii kabisa wakati wa kupiga chenga. Katika suala hilo, mguu wake dhaifu ni dhaifu sana. Ili kumtendea haki, ingawa, si wachezaji wote, ni Santi Cazorla pekee anaweza kutumia miguu yao yote miwili hata wakati wa kucheza chenga.

**Lionel Messi**

Lionel Messi amefunga mabao mazuri kwa mguu wake wa kulia. Ingawa mguu wake dhaifu wa kulia hauna nguvu kama mguu wa kushoto, huwa na ufanisi zaidi unapokuwa karibu na lango.

Hata kwa mguu wake wa kulia, Messi anaonekana kuuweka mpira vizuri, lakini zaidi ya hapo na kwa umbali mrefu haki yake inakaribia kupitwa na wakati na anaitumia tu kwa kukimbia.




RONALDO



MESSI

## Nukuu

"Nimegundua leo [juzi] kuwa ilikuwa mechi yangu ya 1,000. Ninaishi wakati huu, ninafurahia kile tunachopitia, na nina furaha kuchukua hatua moja zaidi, kutinga robo fainali," **Mshambuliaji wa Argentina Lionel Messi baada ya kufunga bao dhidi ya Poland na kuipeleka timu yake robo fainali ya Kombe la Dunia 2022.**




"Kwa sasa, yeye ndiye mchezaji bora wa Ufaransa na hata katika Kombe hili la Dunia. Ni kama (N'Golo) Kante. Haonekani tofauti lakini anapokosekana, inahisiwa," **Mshambuliaji wa Uruguay, Diego Forlan, akieleza kuvutiwa na ubora wa nyota wa Ufaransa, Kylian Mbappe.**



"Tunaposhinda, tunashinda pamoja, tunapopoteza, tunapoteza pamoja. Haibadilishi mawazo yangu. Hili ni kundi, Timu ya Taifa ya Brazil lazima icheze kama kundi moja. Hilo ni muhimu sana kupata kombe," **Kiungo wa Brazil Casemiro baada ya kufunga bao pekee dhidi ya Uswisi wakati wakishinda 1-0 na kutinga hatua ya 16-bora ya Kombe la Dunia nchini Qatar.**



# MAPRO WA SOKA WALIONOGEWA VILIVYO NA BONGO


CHAMA

**Na Adam Fungamwango**

MOJA kati ya vitu ambavyo Tanzania imebarikiwa ni amani, utulivu na ukarimu wa watu wake. Hivi ndivyo vinadaiwa kuwafanya wengi wanaokuja nchini wasitamani kuondoka. Na hata wakiondoka, basi ipo siku watarejea tena ili kuupata ule ukarimu wa watu wake.

**Hata kwenye nyanja ya michezo wachezaji wengi waliofika nchini na kusajiliwa klabu mbalimbali zikiwamo kubwa za Simba na Yanga, wamekuwa wakirejea tena pale wanapoondoka.**

Wachezaji ambao huondoka kwenda kusajiliwa klabu zingine za nje ya nchi, kwa sababu mbalimbali ikiwamo kupata mikataba au kuachwa, baadhi yao wamekuwa wakirejea tena nchini.

Katika hali inayoonyesha kuwa wachezaji hao wanapenda kucheza soka na kuishi nchini, baadhi wamerejea na hata kuzichezea klabu za Championship.

Hawa ni baadhi tu ya wachezaji ambao walikuja, wakaondoka, lakini wamerejea tena kucheza na soka nchini...

**#1. CLATOUS CHAMA - SIMBA**

Huyu ni kiungo mshambuliaji wa Kizambia, kipenzi cha wanachama na mashabiki wa Simba. Si kwa sababu ya uchezaji wake wa kuburudisha na uwezo mkubwa alionao, lakini mara nyingi ndiye anayeamua ushindi wa timu hiyo.

Alijiunga na Simba mwaka 2018 akitokea Lusaka Dyanamos ya Zambia. Aliwahi kuzichezea pia timu za Al Hitihad ya Misri na Zesco ya Zambia. Mwaka jana Simba ilimuuza kwenda RS Berkane. Hakuwa na raha kwenye klabu hiyo ya Morocco, huku timu aliyoiacha ikiwa haifanyi vema, ikatolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika na kuangukia Shirikisho, kwa kiasi kikubwa ilichangia kunyang'anywa ubingwa iliokaa nao kwa misimu minne. Simba ilimhitaji arejee na yeye akakubali kurudi tena nchini kipindi cha dirisha dogo msimu uliopita.

**#2. TUISILA KISINDA - YANGA**

Winga huyu raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, kama ilivyo kwa Chama alijiunga na RS Berkane akitokea Yanga mwaka 2021. Walijiunga pamoja.

Kabla ya hapo alikuwa na klabu ya Yanga aliyokuwa amejiunga nayo tangu 2020. Kabla ya Yanga alikuwa akiichezea Vita Club ya Congo DR mwaka 2019.

Wakati Chama akirejea Simba kipindi cha dirisha dogo msimu uliopita, Tuisila Kisinda amekaa kwa msimu mzima Morocco na kurejea tena nchini mwanzoni mwa msimu huu wa Ligi ya 2022/23 akijiunga tena na Yanga.

**#3. AMISSI TAMBWE - SINGIDA BIG STARS**

Alitamba nchini kuanzia mwaka 2013 hadi 2019 akiwa kwenye klabu kubwa za Simba na Yanga. Straika huyo Mrundi ameshawahi kuwa mfungaji bora akiwa na timu hizo.

Alijiunga na Simba mwaka 2013 akitokea Vital'O ya Burundi na kuitumikia hadi 2014 alipohamia Yanga ambako nayo alikipiga hadi 2019.

Aliondoka nchini kwenda kucheza soka la kulipwa Klabu ya Fanja nchini Oman. Pia na yeye alirejea nchini 2021 akijiunga na DTB, akicheza Ligi ya Championship na kuipandisha daraja. Kwa sasa inaitwa Singida Big Stars akiwa mmoja kati ya wachezaji wanaounda kikosi cha timu hiyo.

**#4. JAMES KOTEI - MTIBWA SUGAR**

Ni mmoja kati ya wachezaji waliorejea tena nchini. Kotei, raia wa Ghana kwa sasa anaichezea Mtibwa Sugar. Alivuma akiwa na klabu ya Simba ambayo alijiunga nayo mwaka 2016 akitokea Al-Orouba ya Oman. Kiungo mkabaji huyo alijizolea mashabiki wengi kutokana na aina yake ya uchezaji na upambanaji. Aliichezea hadi 2019, akaondoka kwenda kuitumikia Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini.

Pamoja na kuzunguka kwenye klabu za Slavia Mozyr ya Beralus na Sohar ya Oman, hivi sasa amerejea tena nchini akiwa na wakatamiwa hao.

**#5. PASCHAL WAWA - SINGIDA BIG STARS**

Ni beki wa kati ambaye awali kabisa aliichezea Azam FC aliyojiunga nayo 2014 akitokea Al Merrikh ya Sudan ambayo alijiunga nayo akitokea Asec Mimosas ya Ivory Coast.

Beki huyu raia wa Ivory Coastal aliondoka nchi kwenda Sudan akirejea tena kwenye klabu yake ya zamani Al Merrikh mwaka 2016 hadi 2017 ambapo Simba ilimrejesha nchini hadi mwaka huu ambapo imeachana naye, lakini bado yupo hapa nchini akiitumikia Singida Big Stars.

**#6. DEO KANDA - MTIBWA SUGAR**

Winga huyo wa kikongomani naye amerejea tena nchini na sasa anaichezea Mtibwa Sugar. Alishawahi kuwa hapa nchini akiichezea Simba ambayo alijiunga nayo mwaka 2019 akitokea TP Mazembe kwa mkopo. Aliondoka na kurudi kwenye timu yake ya TP Mazembe na sasa amejiunga na Mtibwa Sugar. Ni mchezaji ambaye pia ameshawahi kukipiga na Klabu ya Motema Pembe, AS Vita Club, na Raja Casablanca ya Morocco.

**#7. PAPPY TSHISHIMBI - IHEFU**

Alijiunga na Yanga mwaka 2018 akitokea Mbabane Swallow ya Eswatini na kuwa mmoja wa wachezaji mastaa wa klabu hiyo akicheza nafasi ya kiungo mkabaji na wakati mwingine kiungo mshambuliaji. Mkongomani huyo aliachana na Yanga mwaka 2020, akaenda kwao DR Congo kujiunga na AS Vita Club, lakini alirejea nchini akijiunga na DTB ambayo baada ya kuIpandisha daraja akatimkia Ihefu FC kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

**#8. HAMISI KIIZA - KAGERA SUGAR**

Kwa sasa ni straika wa Kagera Sugar. Kiiza, raia wa Uganda ameshawahi kuzichezea Klabu za Simba na Yanga miaka ya nyuma. Alianza kuichezea Yanga mwaka 2011 akitokea URA ya Uganda hadi 2015 ambapo alijiunga na Simba, akiichezea hadi 2016.

Aliondoka nchini kwenda kuzichezea Free State ya Afrika Kusini, akarejea nyumbani kuitumikia URA kisha akaenda El Hilal El Obeid ya Sudan, Fasil Kanema ya Ethiopia, Vipers na Proline FC za Uganda na hatimaye amerejea tena nchini, lakini sasa yupo Kagera Sugar.

**#9. NICOLAUS GYAN - SINGIDA BIG STARS**

Ni mmoja kati ya wachezaji waliolipandisha daraja Singida Big Stars kutoka Championship, wakati huo ikitumia jina la DTB. Kabla ya hapo alishawahi kuwa nchini akiichezea Simba. Gyan, raia wa Ghana alijiunga na Simba mwaka 2017 kama straika akitokea Ebusua Dwarfs ya nchini humo, lakini alibadilishiwa namba, akawa beki wa kulia ambayo aliimudu na anakumbukwa na mashabiki wengi wakati ule Simba ikicheza Ligi ya Mabingwa kwa mara ya kwanza na kutinga makundi. 2019 aliondoka kwenda kuichezea Legon Cities ya nchini kwao, kabla ya kurejea tena nchini.

**#10. SHAFIQ BATAMBUZE - SINGIDA BIG STARS**

Ana uwezo wa kucheza beki zote za pembeni na kiungo wa kati. Ni raia wa Uganda aliyekuwa nchini 2017 akichezea Singida United hadi 2018 alipotimkia Gor Mahira ya Kenya, baadaye Kabwe Warriors ya Zambia, lakini na yeye ameingia kwenye orodha ya wachezaji waliorejea tena nchini, akiichezea Singida Big Stars.

NDANI YA 18



Olivier Giroud, Antoine Griezmann na Hugo Lloris, wamekuwa wachezaji wa kwanza kushinda zaidi ya mechi 10 kwenye Kombe la Dunia wakiwa na Ufaransa.

# SOKA



**REKODI**

* Amevunja rekodi ya Brazil ya kuwa timu ya kwanza katika historia ya Kombe la Dunia kutofungwa katika mechi 17 mfululizo za hatua ya makundi.

* Hii ni baada ya kufunga bao pekee wakati Cameroon iki-ichapa Brazil 1-0 kwenye mechi ya Kundi G ya Kombe la Dunia Qatar 2022.

* Hata hivyo, alitolewa kwa kadi nyekundu kwa kuvua jezi baada ya kuonyeshwa njano ya pili. Pamoja na ushindi huo Cameroon haikufuzu hatua ya 16-bora.

**MKALI WA WIKI**

**JINA KAMILI:** Vincent Aboubakar
**KUZALIWA:** Januari 22, 1992 (miaka 30)
**ALIPOZALIWA:** Yaounde, Cameroon
**KIMO:** 1.76 m (5 ft 9 in)
**NAFASI:** Straika
**KLABU:** Al Nassr
**JEZI NAMBA:** 9/ Taifa 10

Nipashe
# Spotika

KWA wengine, Lionel Messi ndiye mchezaji bora zaidi kuwahi kutokea na kwa wengine, Cristiano Ronaldo yuko juu. Jambo ambalo haliwezi kukanushwa ni ukweli kwamba wachezaji hawa wote wawili ni bora zaidi kwa kizazi chao, na kwamba hakuna mtu mwingine anayekaribia kiwango walichonacho.

Uk. 16-17



Kikosi cha Timu ya Taifa ya Qatar 2022

# REKODI MBAYA ZAIDI KOMBE LA DUNIA

**DOHA,** Qatar

KOMBE la Dunia ni sherehe ya mwezi mzima ya walio bora zaidi, wababe wa soka wakimenyana kwenye jukwaa kubwa la mchezo.

**Mashabiki wa kila ki-zazi wataweza kurudisha mawazo yao nyuma na kukumbuka angalau nchi ambayo huja kwenye sherehe kwa furaha kubwa na hurudi nyumbani mapema.**

Hapa tunaangalia rekodi mbaya zaidi kwa timu kwenye Fainali za Kombe la Dunia, haya sasa...

**#10. INDONESIA - 1938**

Ikiwa inajulikana kama East Indies wakati huo - sasa Indonesia - wana moja ya rekodi mbaya zaidi katika historia ya Kombe la Dunia.

Mwaka 1938, mashindano yalipoingia moja kwa moja katika mfumo wa mtoano, Indonesia walicheza dhidi ya Hungary waliofuzu katika hatua ya 16 bora, ambapo walilazwa mabao 6-0 katika mechi yao moja na pekee ya Kombe la Dunia.

**#9. QATAR - 2022**

Kuna timu nyingi zaidi ambazo zimekabiliwa na kampeni za Kombe la Dunia zenye alama sifuri, ingawa rekodi yao si ya kiufundi kati ya timu mbaya zaidi, Qatar imeingia kwenye orodha hii kwa kuwa taifa mwenyeji lenye rekodi mbaya zaidi katika historia ya mashindano hayo.

Qatar walitolewa kabisa kwa kushindwa kwao na Ecuador, Senegal na Uholanzi.

**#8. MEXICO - 1978**

Mexico wameshiriki fainali za Kombe la Dunia mara 17. Mwaka 978 wanajivunia mojawapo ya rekodi hizo mbaya, wakiondoka kwenye shindano wakiwa wamepoteza mechi zao tatu.

Michuano yao ilianza kwa kuchapwa mabao 3-1 na Tunisia, kabla ya kulazwa 6-0 na Ujerumani Magharibi na kutolewa kwa raha 3-1 na Poland.

**#7. UFARANSA - 2002**

Timu pekee katika orodha hii ambayo imeshinda pointi moja katika kampeni zao za Kombe la Dunia, upande wa Ufaransa mwaka 2002 ndio pekee inaorodhesha orodha hii kwa kuonyesha hali ya kukatisha tamaa waliyoweka, huko Japan na Korea Kusini.

Huenda uchezaji mbaya zaidi wa mabingwa watetezi wa dunia, Ufaransa walianza kwa mshtuko mkubwa zaidi katika historia ya Kombe la Dunia, kwa kupoteza bao 1-0 na Senegal huku marehemu Papa Bouba Diop akifunga bao la ushindi kipindi cha kwanza.

Kikosi cha Roger Lemerre kiliendelea kuhitimisha kampeni zao za Kombe la Dunia 2002 kwa sare ya 0-0 dhidi ya Uruguay na kufungwa 2-0 na Denmark, na hivyo kumaliza kutetea ubingwa wao bila kufunga bao lolote.

**#6. SAUDI ARABIA - 2002**

Mwaka 2002 pia ilishuhudiwa moja ya timu mbaya zaidi za Kombe la Dunia - kitakwimu.

Ingawa Saudi Arabia wanaweza kuwa wamefanya vizuri nchini Qatar mwaka huu, timu yao ya 2002 haikufanya lolote. Hatua ya makundi ambapo walifungwa 8-0 na Ujerumani, 1-0 na Cameroon na 3-0 na Ireland iliimarisha kwa uthabiti nafasi yao kama timu mbaya zaidi ya michuano hiyo.

**#5. KOREA KASKAZINI - 2010**

Korea Kaskazini ilifuzu Kombe la Dunia kwa mara ya pili tu mwaka 2010.

Katika mechi yao ya kwanza ya Kombe la Dunia baada ya miaka 44, Wakorea Kaskazini walichapwa mabao 2-1 na Brazil katika mchezo wao wa ufunguzi. Wakapata kichapo cha 7-0 kutoka kwa Ureno na kupoteza 3-0 kwa Ivory Coast.

**#4. BOLIVIA - 1950**

Kombe la Dunia la mwaka 1950 lilikuwa la kushangaza; kulikuwa na makundi manne - mawili yakiwa na timu nne, moja ikiwa na tatu, na kundi la mwisho la timu mbili tu baada ya Ufaransa kujiondoa kwenye mashindano kabla ya kucheza.

Katika kundi hilo la mwisho, ambao ndio mabingwa Uruguay walichuana na Bolivia - mechi moja na kutinga hatua ya fainali ya michuano hiyo. Uruguay ilimaliza upesi kampeni ya Kombe la Dunia la Bolivia kwa kuishushia kipigo cha mabao 8-0.

**#3. HAITI - 1974**

Mwaka 1974 ilileta timu kadhaa za kusikitisha za Kombe la Dunia, mmoja wao ikiwa Haiti.

Wahaiti hao ambao wamecheza Kombe la Dunia mara moja tu, walimalizika kwa hali ya kukatisha tamaa sana, wakitoka katika hatua ya makundi kufuatia kichapo cha mabao 3-1 kutoka kwa Italia, kipigo cha 7-0 kutoka kwa Poland iliyoshika nafasi ya tatu na kufungwa 4-1 na Argentina.

**#2. EL SALVADOR - 1982**

El Salvador iliifikia rekodi mbaya ya mabao ya Haiti miaka nane baadaye, na kumaliza kampeni yao ya hatua ya makundi kwenye Kombe la Dunia la 1982 kwa vipigo vitatu vya kukatisha tamaa ambapo wakiruhusu mabao 13 na hawakufunga bao lolote.

**#1. ZAIRE (DRC CONGO)- 1974**

Timu mbaya zaidi kuwahi kutokea katika Kombe la Dunia ni Zaire (sasa inajulikana kama Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo).

Wakiwa wamecheza michuano hiyo mara moja pekee hadi sasa, kikosi hicho kilipoteza michezo yao yote mitatu ya kundi - walifungwa 2-0 na Scotland, 9-0 na Yugoslavia na 3-0 na Brazil - wakifungwa jumla mabao 14.

Uchezaji wao utaandikwa milele kwa kiwango cha rekodi mbaya zaidi ya mabao katika kampeni ya hatua ya makundi ya Kombe la Dunia.

**JE, WAJUA?**



KATIKA wachezaji wote wanaoshiriki Kombe la Dunia nchini Qatar, Kipa wa Canada, Milan Borjan, anayecheza soka la kulipwa nchini Serbia (dakika 5,520), ndiye mchezaji pekee anayemzidi beki wa Liverpool na Uholanzi, Virgil van Dijk kwa kucheza dakika nyingi kwa mwaka huu wa 2022. Van Dijk amecheza dakika 5,250, akifuatiwa na Harry Kane wa Spurs na England mwenye dakika 4,830 (kabla ya mchezo wa jana dhdi ya Senegal), kwa mujibu wa CIES.



## Mbeya-WSSA yatahadharisha upungufu wa maji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA), imetangaza upungufu wa maji kwenye baadhi ya maeneo ya miji kutokana na kukosekana kwa umeme kwenye moja ya vyanzo vyake vikuu.

Ofisa Uhusiano wa Mamlaka hiyo, Neema Stanton, alisema tatizo lipo kwenye chanzo cha maji cha Nzovwe ambacho kwa sasa hakina huduma ya umeme na hivyo mitambo inashindwa kusukuma maji kwenda kwa wananchi.

Alisema maeneo ambayo yanakosa huduma hiyo kwa sasa ni Ilomba na Ilomba B ambazo ndizo zinahudumiwa na chanzo hicho.

Alisema wataalamu wa mamlaka hiyo kwa kushirikiana na mafundi wa Shirika la Umeme nchini (TANESCO) wanaendelea kushughulikia tatizo hilo ili kurejesha huduma kwa wananchi.

"Tunaamini huduma itarejea baada ya muda mfupi na wananchi wataendelea kunufaika, tunaomba waendelee kuwa wavumilivu katika kipindi hiki ambacho hali imekuwa tofauti lakini tuwahakikishie kuwa ni tatizo la muda mfupi," alisema Neema.

Alisema kwa sasa Jiji la Mbeya halina tatizo kubwa la maji kutokana na kuwa na vyazo vingi ambavyo vinatumika kuzalisha huduma hiyo na kuisambaza kwa wananchi.

Hata hivyo aliwataka wananchi kutoa taarifa kwa mamlaka hiyo wanapoona mabomba yamepasuka ili kupunguza upotevu wa maji ambayo yanazalishwa kwa gharama kubwa.

# Waziri awa mbogo utoroshaji madini

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

SERIKALI imewaonya wachimbaji na wanunuzi wa dhahabu nchini wanaotorosha madini hayo kuwa watachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani na kufungiwa leseni zao.

Waziri wa Madini, Dk. Dotto Biteko, alitoa onyo hilo mwishoni mwa wiki wilayani Chunya mkoani Mbeya alipowatembelea wanunuzi na wachimbaji wadogo wa dhahabu.

Alisema baadhi ya wachimbaji na wafanyabiashara hao wamekuwa wakiuziana madini hayo nje ya mfumo rasmi wa masoko hali ambayo inachochea uuzwaji holela na kuipotezea serikali mapato.

Hivyo aliwataka kuacha tabia hiyo pamoja kutoa taarifa wanapowabaini wenzao wanaofanya vitendo hivyo ili wachukuliwe hatua za kisheria na kukomesha biashara hiyo.

"Hatuwezi kukubali watu wachache watuharibie biashara ya madini, duniani kote dhahabu inauzwa kwenye mifumo rasmi sasa kwa wale ambao bado wanaendelea kutorosha madini haya tutawachukulia hatua kali ili iwe fundisho kwa wengine," alisema Dk. Biteko.

Alisema kuna baadhi ya wanunuzi wanawafuata wachimbaji kwenye migodi na kuuziana kwa bei ya juu tofauti na elekezi kwa makubaliano ya kutowakata mirabaha ya serikali.

Dk. Biteko alisema kwa sasa wanaendelea kuwafuatilia wanunuzi wote wa madini ili kubaini mienendo yao huku akisisitiza kuwa wakati wa kuhuisha leseni mwezi Julai mwakani watabaki waaminifu pekee na wale wanaotorosha hawataruhusiwa kuhuisha.

Mbunge wa Lupa, Masache Kasaka alisema wachimbaji wadogo wa dhahabu wilayani Chunya wanakabiliwa na kero mbalimbali ambazo zinawafanya washindwe kuinuka kiuchumi liche ya kufanya kazi hiyo kwa muda mrefu.

Aliyataja baadhi ya matatizo hayo kuwa ni pamoja na taasisi nyingi kudai kodi kwa nyakati tofauti hali ambayo alisema inawachanganya wachimbaji hao kutokana na kutokuwa na elimu ya kutosha kuhusu ulipaji wa kodi hizo.

Alizitaja baadhi ya taasisi hizo kuwa ni Mamlaka ya Mapato nchini (TRA), Mifuko ya Hifadhi za Jamii, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Baraza la Taifa la Mazingira (NEMC), Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA).

Alisema Chunya ni miongoni mwa maeneo nchini ambayo yanaongoza kwa uzalishaji wa dhahabu kwa maelezo kuwa unashika nafasi ya pili baada ya Mkoa wa Geita.

Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji Madini Mkoa wa Mbeya (MBEREMA), Leonard Manyesha, alisema baadhi ya wachimbaji wadogo wamefungiwa akaunti zao na TRA kwa sababu ya kudaiwa madeni ya nyuma ambayo baadhi yao walishatumia fedha.



Waziri wa Madini, Dk. Dotto Biteko (wa pili kushoto) na Mbunge wa Jimbo la Lupa wilayani Chunya, Masache Kasaka (katikati), pamoja na baadhi ya wataalamu wa ofisi ya madini ya Mkoa wa Mbeya, wakiangalia ramani ya jengo la maabara ya kuchunguza sampuli za madini linalojengwa wilayani Chunya, mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wanafunzi Shule Mapambano hatarini kudondokewa na ukuta

**Na Nebart Msokwa,** BUSOKELO

WANAFUNZI wa Shule ya Msingi Mapambano iliyoko katika Kata ya Mpombo Halmashauri ya Busokelo mkoani Mbeya, wako hatarini kuangukiwa na kuta za madarasa kutokana na miundombinu hiyo kuchakaa.

Majengo ya shule hiyo yameliwa na fangasi na hata mabati yaliyotumika kuezeka yamechakaa kutokana na kukaa muda mrefu bila kubadilishwa hali ambayo inasababisha baadhi kuvuja.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Benford Mwanjala, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa ziara ya Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete aliyoifanya shuleni hapo. Mwalimu Mwanjala alisema majengo ya shule hiyo yalijengwa kati ya Mwaka 1960 na 1980 lakini hayajawahi kufanyiwa ukarabati hali ambayo imeyafanya yachakae na kuhatarisha maisha ya wanafunzi.

Hivyo aliiomba serikali na wadau wa maendeleo kusaidia kuifanyia ukarabati shule hiyo ili kuwaokoa wanafunzi na hatari hiyo ya kuangukiwa na kuta pamoja kuwafanya wasomee kwenye mazingira rafiki.

Alisema shule hiyo inazaidi ya wanafunzi 529 huku ikiwa na vyumba vya madarasa 11 ambavyo kati yake ni vinne pekee ndio vina hali nzuri na vinavyobaki vyote vimechakaa.

"Tunaiomba serikali itusaidie kukarabati vyumba hivi maana viko katika hali mbaya sana, ikiwezekana inatakiwa vyumba hivi vibomolewe na kujengwa upya, hali iliyopo sasa hivi ni ya mashaka sana," alisema Mwalimu Mwanjala. Mwenyekiti wa Halmashauri ya Busokelo, Anyosisye Njobelo, alisema kutokana na hali ya shule hiyo, wananchi walikubaliana kuanza kufanya ukarabati wa baadhi ya majengo lakini wakaamua kuacha kutokana na kuwa katika hali mbaya.

Alisema walitaka kuanza kwa kupachika milango na madirisha mapya lakini wakabaini kuwa majengo hayo hayastahili kukarabatiwa na bali yanatakiwa kubomolewa na kujengwa upya.

Alisema majengo hayo ni ya miaka mingi na hivyo hayafai kuendelea kutumiwa na wanafunzi pamoja na walimu kutokana na kuhatarisha maisha yao.

Naibu Waziri Mwakibete alisema shule hiyo ni miongoni mwa shule ambazo zipo kwenye mipango ya serikali ya kuzikarabati na kujengwa upya kutokana na miundombinu yake kuwa ya muda mrefu.

Alisema mbali na ukarabati wa shule hiyo, pia serikali ina mpango wa kujenga shule nyingine katika kata hiyo itakayoitwa Kipagika ili kuwapunguzia baadhi ya wanafunzi kutembea umbali mrefu kwenda shuleni.

Alisema shule hiyo mpya itasaidia kupunguza mrundikano wa wanafunzi kwenye shule hiyo ambayo kwa sasa ina wanafunzi wengi.

Mwakibete alisema Sh. milioni 12 zitapelekwa katika shule hiyo kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha ili kuanza ujenzi wa jengo moja kwa awamu ya kwanza wakati nguvu zinakusanywa kwa ajili ya ujenzi wa majengo mengine.



# Wahitimu vyuo vikuu watakiwa kutumia elimu yao kujiajiri

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

MAKAMU Mkuu wa Chuo Kikuu cha St.John's Tanzania, Prof. Yohana Msanjila, amewaasa wahitimu wa elimu ya juu kuitumikia jamii kwa uaminifu na kutumia elimu na maarifa waliyopata kukabiliana na soko la ajira nchini.

Alitoa wito huo mwishoni mwa wiki jijini Dodoma kwenye mahafali ya 13 ya chuo hicho ambayo wahitimu 965 walitunukiwa vyeti na Mkuu wa Chuo, Askofu Mkuu Mstaafu wa Kanisa la Anglikana, Donald Mtetemela.

"Muwe mabalozi wazuri wa chuo chetu huko mnakoenda kumbukeni kwamba popote mtakapokuwapo mmebeba nembo na kauli mbiu ya chuo kwenda kutumika kwa weledi na uaminifu mkubwa, mtumie maarifa mliyopata kujiajiri na kuajiriwa,"alisema.

Askofu Mtetemela alisema elimu waliyoipata itakuwa na thamani endapo itaendana na kasi ya mabadiliko ya sayansi na teknolojia katika kuleta suluhisho la kero zinazoikabili nchi.

Aidha, alisema chuo hicho kimeendelea na uboreshaji wa mitaala ikiwa ni pamoja na kuongeza kozi mpya ambazo mbili zinasubiri kibali kutoka Tume ya Vyuo Vikuu (TCU) kabla ya kuanza kutumika.

"Chuo kinakusudia kuanzisha kozi fupi kwenye maeneo mbalimbali ikiwamo huduma kwa wateja, ujasiriamali na utafutaji wa masoko ya bidhaa, zitatolewa kwa watumishi wa serikali, sekta binafsi, asasi za kiraia na watu binafsi watakaopenda," alisema.

Alisema kufanyika kwa jitahada hizo zinalenga kutoa maarifa na ujuzi kwa jamii.

Askofu Mtetemela alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa utendaji mzuri ambao chuo kina imani naye sambamba na uwekezaji unaofanyika na uimarishaji wa diplomasia ya kiuchumi.

"Tuna matumaini makubwa kupitia serikali yake kwamba shule zetu za msingi na sekondari zitaendelea kuboreshwa ili kutoa wanafunzi wengi bora watakaojiunga na elimu ya juu, tunaimani wanafunzi watakaodahiliwa mwakani watapatiwa mikopo ya kuwawezesha kupata elimu ya juu bila vikwazo vyovyote,"alisema.

Naye Mwenyekiti wa Baraza la Chuo hicho, Prof.Penina Mlama, alisema taasisi za vyuo vikuu huandaa wataalamu mbalimbali ikiwamo afya, kilimo, biashara, uhandisi na kupitia hao nchi inapata mafanikio kadhaa.

Alisema chuo hicho kimejipanga kuongeza udahili, kuboresha taaluma, kufanya mapitio ya mitaala, kuendeleza wafanyakazi kitaaluma, kuanzisha kozi mpya kuendana na mahitaji ya soko, kufanya utafiti na kutekeleza miradi ya kitaaluma.

Mmoja wa wahitimu, Emanuel Kombe, aliwashauri wenzake kutumia elimu na maarifa waliyoyapata kujikwamua kiuchumi kutokana na nchi kukabiliwa na tatizo la ajira.



Kaimu Mkurugenzi wa Programu ya MCGL, Dk. Maryrose Giattas, akimkabidhi kompyuta mpakato Mratibu wa Huduma za Chanjo Mkoa wa Singida, Habibu Mwinory, kati ya saba zilizotolewa na Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID) kupitia Shirika la JHPIEGO Tanzania katika mradi wake wa MCGL. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# DC awaomba wananchi kuripoti matukio ya ndoa za utotoni

**Na Renatha Msungu,** BAHI

MKUU wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamis Munkunda, amewaomba wananchi kutoa taarifa pindi watakapoona matukio ya ndoa za utotoni na ukatili wa kijinsia kwenye maeneo yao.

Alitoa kauli hiyo wakati wa hafla ya siku 16 za kupinga ukatili iliyoandaliwa na Shirika la Msichana Initiative.

Munkunda alisema kuna wasichana wengi ambao wameokolewa kwenye ndoa za utotoni kutokana na jamii kutoa taarifa, hivyo kuna umuhimu wa kutoa taarifa ili kukomesha vitendo hivyo.

"Naomba muwe mstari wa mbele kupiga vita ukatili na ndoa za utotoni, nahitaji kuona watoto wa kike wanasoma, jamii nyingi imekuwa ikiwaficha watoto wao mnapaswa kuacha tabia hii badala yake muwahimize kwenda shule ili watimize ndoto zao,"alisema.

Mkurugenzi wa Msichana Initiative, Rebecca Gyumi alisema lengo lao ni kuona watoto wa kike wanasoma shule na kutimiza ndoto zao kama ilivyo kwa watoto wa kiume.

Alisema wamefanikisha kuokoa watoto wengi wa kike kutoka katika ndoa za utotoni.

"Suala hili la ndoa na mimba za utotoni halikubaliki ndiyo maana tunapambana kuwakomboa watoto wa kike na kila mwaka tumekuwa tukishiriki hafla hizi kwa kushirikiana na serikali,"alisema.

Mmoja wa wanafunzi, Ester Jackson alilishukuru shirika hilo kwa kumsaidia kuendelea na masomo yake baada ya kuepuka ndoa za utotoni.

Hivyo aliiomba serikali kuendelea kukemea ndoa hizo kwa sababu zinakatisha ndoto za watoto wa kike kuendelea na masomo yao.

Alisema wasichana wengi wameolewa bila ridhaa yao hivyo suala hilo linapaswa kupigiwa kelele ili litokomezwe.

## Bunge la Vijana lampongeza Samia uimarishaji diplomasia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE la Vijana mwaka 2022 limeazimia kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa utendaji kazi mzuri ikiwamo kuimarisha mahusiano ya kidiplomasia.

Akitoa azimio la bunge hilo juzi Spika wa Bunge hilo, Antipas Pamba, alisema pia wamempongeza kwa kutunukiwa Shahada ya Udaktari wa Falsafa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), kwamba inaakisi utendaji anaofanya kwa jamii.

"Tunampongeza tunaona wageni wengi wanakuja, sisi kama Bunge tunapongeza hilo na yale mazuri wanayotuletea twende nayo lakini yale yanayokwenda kinyume na tamaduni zetu tuyaache," alisema.

Pamba alifafanua kuwa Bunge limetoa azimio la kumpongeza Rais Samia kwa kazi anayofanya kwenye sekta ya maji ya kuendelea na mikakati ya kumtua mama ndoo kichwani kwenye maeneo mbalimbali.

"Rai yangu kwenye hili serikali itusaidie suala la utoaji wa huduma ya maji lisiwe biashara, serikali ihakikishe wananchi wanapata maji bila kikwazo," alisema.

"Udaktari aliotunukiwa siyo tu wa kupewa kirahisi wamekaa maprofesa kadhaa na kuamua kutoa shahada hiyo kwa Rais kwa sababu amefanya mengi na vijana tunatambua mchango wake kwa mambo anayofanya,"alisema Pamba.

Alisema vijana wa Bunge hilo wamejifunza mambo mbalimbali ikiwamo namna ya uendeshaji wa Bunge.

"Kauli mbiu ya Bunge letu ilikuwa inahusu mabadiliko ya tabia nchi na mchango wa kijana kushiriki kwenye mchakato wa kukabiliana na madhara yanayotokana na mabadiliko ya tabianchi, tumejadili mambo mbalimbali kupitia miswada mbalimbali inayohusu sera za mabadiliko ya tabia nchi," alisema.

Pamba alisema mabadiliko ya tabianchi ni tatizo linaloikabili dunia kwa sasa na ni muhimu vijana kuyajua na kukabiliana nayo.

Waziri Mkuu katika Bunge hilo, David Godian, alishukuru Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutambua uwezo wa vijana na kuitisha mkutano uliolenga vijana wajadili athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwenye Bunge hilo, Lightness Mvungi alisema Rais Samia anapaswa kutunukiwa shahada hiyo kwa kuwa aliivusha nchi kwenye kipindi kigumu kilichokuwa na ugonjwa wa corona.

Akizungumza kwa niaba ya Katibu wa Bunge hilo, Mkurugenzi wa Mawasiliano na Mahusiano ya kimataifa wa Ofisi ya Bunge, Daniel Eliufoo, alisema Bunge hilo la vijana limemaliza shughuli na wameweza kujadili masuala mbalimbali ikiwamo kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

## Dk. Mwinyi: Serikali inafanya mageuzi ya kiuchumi

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema serikali inafanya mageuzi makubwa ya kiuchumi kupitia rasilimali zilizoko za bahari.

Alisema inafanya mageuzi hayo kwa sababu kipaumbele kikubwa kwa Serikali ya Zanzibar ni uchumi wa buluu.

Aliyasema hayo juzi Ikulu Zanzibar alipokutana na Meneja Mkaazi wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Dk.Patricia Laverley.

Dk. Mwinyi alisema serikali inatarajia kutumia vyema rasilimali hizo ili kufikia azma ya mageuzi hayo ya kiuchumi kwamba tayari sera ya uchumi wa buluu imeshatengenezwa.

Aidha, alisema malengo hayo yanategemea sana uwapo wa miundombinu ya barabara, bandari, maji safi na salama pamoja na nishati ya uhakika ya umeme.

Aidha, aliishukuru AfDB kwa kuonyesha utayari wa kuisaidia Zanzibar msaada wa kifedha katika bajeti yake pamoja na eneo la afya.

Meneja wa AfDB, Patricia Laverley, alisema benki hiyo inatambua jitihada kubwa za mageuzi ya kiuchumi zinazofanya na Rais Dk.Mwinyi kupitia mwelekeo wa uchumi wa buluu.

Alisema kupitia mwelekeo huo ambao kwa kiasi kikubwa una rasilimali za kutosha za baharini utawanufaisha Wazanzibari katika eneo la uvuvi, kilimo cha mwani na viwanda.

Alisema AfDB iko tayari kusaidia eneo la afya ambalo Rais Dk.Mwinyi ameliwekea kipaumbele.

**Aliyasema hayo juzi Ikulu Zanzibar alipokutana na Meneja Mkaazi wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Dk.Patricia Laverley.**

# ‘Matukio udhalilishaji watoto wa kiume Zanzibar yashamiri’

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKE wa Rais wa Zanzibar, Mariam Mwinyi, amesema kasi ya matukio ya udhalilishaji wa kijinsia visiwani Zanzibar imeshamiri zaidi kwa watoto wa kiume jambo ambalo litasababisha kuua kizazi kinachokuja.

Aliyasema hayo jana katika sherehe za tunzo kwa vinara wa kupinga vitendo vya udhalilishaji zilizoandaliwa na Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA) ikiwa ni sehemu ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia.

Mariam Mwinyi aliwakilishwa na Mhandisi Zena Ahmed Said.

Alisema ukatili na udhalilishaji wa kijinsia ni jambo la kishetani lisilokubalika sehemu yoyote, hivyo wanaharakati vinara wanakazi ya kuisaidia jamii kuondokana na balaa hilo.

Alisema dhuluma hiyo kwa watoto dhambi yake ni kubwa zaidi hivyo ni lazima kutafuta njia ambazo zinatoa ushahidi wa haraka na usio na shaka ili kutoa adhabu kali kwa washtakiwa.

“Mihimili yote ya nchi yapo pamoja katika kupinga masuala haya. Kama unavyoona sheria imesharekebishwa, Mahakama maalum imeazishwa hivyo hili jambo hatulitaki kabisa na tunalipiga vita kila pembe,” alisema.

Mariam alisema serikali inathamini na kuunga mkono jitihada zinazofanywa na wadau na wanaharakati kwenye mapambano ya udhalilishaji wa kijinsia kwa sababu mapambano hayo yanahitaji nguvu ya pamoja.

“Tuzidi kushikamana kwa nguvu zote kuhakikisha tabia hii ambayo kinyume na misingi ya utu inakoma na kubaki historia katika nchi yetu mapambano haya ya udhalilishaji yanahitaji umakini mkubwa,” alisema.

Mkurugenzi wa ZAFELA, Jamila Mahmoud Juma, alisema kuna wimbi kubwa la udhalilishaji dhidi ya watoto wa kiume akieleza kwamba kwa mujibu wa Hospitali ya Mnazi Mmoja wanapokea kesi mpya 150 kwa mwezi za watoto wa kiume wanaodhalilishwa.

Alisema kwa mujibu wa takwimu kutoka Mtakwimu Mkuu wa Serikali kuanzia Januari hadi Septemba mwaka 2020 matukio 865 yameripotiwa na kwa upande wa ZAFELA imepokea malalamiko 200 yanayohusu kesi za madai na jinai kuhusu udhalilishaji wa kijinsia.

Jamila alisema licha ya jitihada kubwa zinazochukuliwa na serikali na wadau lakini kunatatizo la upatikanaji wa takwimu sahihi wa matukio hayo kutokana na kutokuwapo kwa chombo kimoja ambacho kinakusanya matukio hayo.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Watoto, Riziki Pembe Juma, alishauri adhabu kwa wabakaji ziwe kali angalu kifungo cha miaka 50 au wahasiwe ili kuwa funzo kwa wengine.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar, Riziki Pembe Juma, akimkabidhi zawadi Mke wa Rais wa Zanzibar, Mariam (kushoto), baada ya matembezi ya hiari ikiwa ni sehemu ya harakati za Siku 16 za Kupinga Ukatili Kijinsia, Forodhani mjini Zanzibar jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Makamu wa Rais ataka huduma bora kwa watu wenye ulemavu

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman, amesema upatikanaji wa huduma bora kwa watu wenye ulemavu si hiari bali ni la matakwa ya katiba ambayo yanapaswa kusimamiwa vyema.

Alitoa kauli hiyo juzi katika Uwanja wa Gombani Pemba wakati wa kilele cha Siku ya Watu wenye Ulemavu Duniani ikiwa ni hatua ya kutathmini juhudi zinazofanyika kitaifa na kimataifa katika kulinda haki na utolewaji wa fursa sawa kwa watu wenye ulemavu.

Alisema kutokana na hali hiyo serikali zote mbili zinachukua hatua ya kukabiliana na kero zinazowakabili watu wenye ulemavu.

Othman alisema miongoni mwa kero hizo ni upungufu wa walimu na vifaa katika elimu mjumuisho, uhaba wa huduma na vifaa vya marekebisho, kuwapo na miundombinu isiyorafiki.

Alisema kero zingine ni uhaba wa wataalamu wa lugha ya alama, suala la uwezeshaji wa kiuchumi pamoja na udhalilishaji hasa kwa watu wenye ulemavu wa akili.


Othman alisema serikali inaendelea na jitihada za kupambana na kero hizo ikiwa ni pamoja na kubadili sheria pamoja ujenzi wa hospitali mpya za wilaya zinazozingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu.

Alisema pia serikali imejenga shule mpya za dakhalia zinazozingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu ambazo zipo Pujini kwa upande wa Pemba na Jendele kwa Unguja.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harous Said Suleiman, aliitaka jamii kuacha kuwaficha watoto wenye ulemavu kwa sababu kufanya hivyo ni kuwanyima haki zao.

Mwenyekiti wa Baraza la Watu wenye ulemavu Zanzibar, Salma Saadat, alisema kwamba watu wenye ulemavu wanapaswa kufunzwa na kuibua vipaji vyao vya aina mbalimbali walivyonavyo ili kuendelezwa na kutumika katika shughuli za kimaendeleo.

Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa linalishughulikia Idadi ya Watu Duniani (UNFPA), Amina Kheri, alisema wakati umefika kwa makundi yote yakiwamo ya watu wenye ulemavu kushirikishwa na kushiriki katika sekta zote.





# Sungusungu wapewa jukumu kuzuia ndoa, mimba za utotoni

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

JESHI la Jadi maarufu sungusungu kutoka vijiji sita vya Kata ya Lyamidati Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, limepewa jukumu la kuzuia mimba na ndoa za utotoni kwa kukagua umri wa wahusika.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi ofisini kwake Ofisa Mtendaji wa Kata ya Lyamidati, Joyce Mahina, alisema ili kufanikisha adhma ya kutokomeza ndoa za utotoni wameamua kuwakabidhi sungusungu jukumu hilo kwa sababu wao wako karibu na wananchi.

Mahima alieleza hayo wakati wa utekelezaji wa mradi wa sauti za kaya na vyombo vya habari katika kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto, unaotekelezwa na Shirika la SPC kupitia Mfuko wa Wanawake Tanzania (WFT).

Alisema kuanzia sasa hakuna ndoa yoyote itakayofungwa katika kata hiyo bila kujiridhisha umri, kwamba hilo limekuwa likifanywa na Jeshi la Jadi lililoko katika kila Kijiji kwa kushirikiana na wenyeviti wa vitongoji.

Mahina alisema kwa wale watakaobainika watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Alieleza kuwa ulinzi huo unafanywa hadi siku ya magulio na minada kwani kuna wakati wanafunzi wanatendewa vitendo vya ukatili na wanapohojiwa kujua mhusika ni nani wanadai walikutana minadani.

Diwani wa Kata ya Lyamidati, Veronica Nduta, alisema kila ndoa ambayo huwa inafungwa viongozi wa kata huwa wanaalikwa, endapo ni ndoa ya watoto waliochini ya miaka 18 wahusika hawatoa mwaliko kwa viongozi.

Alisema ndoa za kimila zinaongoza katika kuozesha watoto wadogo kulinganisha na zile za kanisani na misikitini ambazo viongozi hujiridhisha kabla ya kufungisha ndoa.

Kamanda wa sungusungu, Salu Bunga alisema, ndoa za utotoni zimepungua baada ya kufanyika ukaguzi, kwamba kwa sasa kuna matukio ya wanaume kutelekeza wake zao na kwenda kuoa wanawake wengine na watoto kukosa mahitaji yao.




Baadhi ya wakazi wa Kitongoji cha Bugarama wilayani Msalala wakipatiwa elimu ya afya na kupima afya zao wakati wa maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani yaliyoandaliwa na Mgodi wa Barrick Bulyanhulu na kufanyika kwenye kitongoji hicho. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wasiojulikana waiba mtoto wa mwezi mmoja

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

MTOTO Benitha Benedict mwenye umri wa mwezi mmoja mkazi wa Migera Kata ya Nshambya Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera ameibwa na watu wasiojulikana wakati mama yake akiwasindikiza wageni.

Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Kagera, William Mwampaghale, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kwamba tukio hilo lilitokea Desemba Mosi mwaka huu majira ya saa sita mchana nyumbani kwa mama wa mtoto huyo aitwaye, Joanitha Agustina.

Kamanda Mwampaghale alisema mama huyo akiwa nyumbani anaendelea na shughuli mtoto wake alikuwa chumbani huku yeye akipokea wageni waliofika kumpongeza.

"Akiwa anawasindikiza wageni hao walikuja wageni wengine watatu na kwamba wakati anarudi nyumbani akitoka kusindikiza wageni wa awali aliingia ndani na kutomkuta mtoto," alisema Kamanda Mwampaghale.

Kamanda Mwampaghale alisema Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi wa kubaini waliohusika na wizi wa mtoto huyo na kuwataka wananchi kutoa taarifa kituo cha polisi kilicho jirani kwa mtu yoyote watakeyemtilia mashaka juu ya wizi huo.

**Kamanda Mwampaghale alisema mama huyo akiwa nyumbani anaendelea na shughuli mtoto wake alikuwa chumbani huku yeye akipokea wageni waliofika kumpongeza.**

# 'Wakazi Kanda ya Ziwa tunzeni vyanzo vya maji'

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WANANCHI wa mikoa ya Kanda ya Ziwa wamepewa jukumu la kushiriki kikamilifu katika kulinda na kutunza vyanzo vya maji ikiwa ni pamoja na kuacha shughuli za kibinadamu katika vyanzo hivyo.

Rai hiyo ilitolewa juzi na Mkurugenzi wa Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria, Renatus Shinhu, wakati wa uzinduzi wa mfumo wa kidijitali wa ukusanyaji wa takwimu za maji ulioambatana na kuwajengea uwezo wasomaji wa ankara za maji kutoka mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Shinhu aliwataka wasomaji wa ankara za maji kuwa mabalozi katika maeneo yao kwa kuwaelimisha wananchi na watumiaji wa maji, kuhakikisha wanatunza vyanzo hivyo ili viendelee kuongeza ujazo ambao utasaidia katika shughuli za usambazaji wa huduma hiyo. Alibainisha kuwa Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria itahakikisha inashirikiana kikamilifu na wananchi katika kusimamia, kutunza, kuboresha pamoja na kuongeza miundombinu rafiki itakayosaidia kutoa huduma za maji.

Akizindua mfumo huo Katibu Tawala Msaidizi kutoka Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza, Daniel Machunda amewataka wasoma ankara za maji kutekeleza majukumu yao kwa wakati ili kuisaidia serikali katika utoaji huduma kwa jamii ikiwa ni pamoja na usanifu wa vyanzo vya maji.

Alisema serikali kupitia Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria inaendelea kuimarisha utunzaji wa vyanzo vya maji ili kuendelea kuvilinda kwa ajili ya kujikinga na maambukizi ya magonjwa.

Mkuu wa Kitengo cha Maji Juu ya Ardhi na Usalama wa Mabwawa, Rosemary Masikini, alisema bodi hiyo imeamua kutoa vifaa janja pamoja na kuendesha mafunzo ya matumizi mazuri ya mfumo mpya wa usomaji wa takwimu za maji uitwao 'ziwa letu app' ili kuharakisha usomaji wa maji kwa haraka na kuepusha ucheleweshwaji wa taarifa.

Alisema kupitia mfumo huo wataweza kuwasilisha taarifa zao kila siku baada ya kumaliza kupima maji, kwamba zitaisaidia bodi kuweka mazingira rafiki katika utekelezaji wa miradi ya usambazaji wa huduma ya maji kwa jamii. Wakizungumza baada ya kupokea vifaa vya kidigitali baadhi ya wasomaji wa ankara za maji akiwamo Mwidini Juma alisema vifaa hivyo vitawapunguzia usumbufu wa kuandaa taarifa ya muda mrefu kwani taarifa hizo zitatumwa kila siku kupitia simu.

HABARI KIMATAIFA

# Rais Cyril Ramaphosa asisitiza kuendelea kutetea wadhifa wake

**CAPE TOWN,** Afrika Kusini

RAIS wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, amesema hana nia ya kujiuzulu na kwamba ataendelea kupambania mamlaka yake na ataipinga ripoti ya bunge mahakamani.

Kwa mujibu wa msemaji wa rais huyo anayekabiliwa na kashfa na kitisho cha kuondolewa madarakani hana nia ya kujiuzulu na kwamba ataendelea kupambana kisiasa na kwa njia za kisheria.

Ramaphosa amekuwa akikabiliwa na shutuma tangu mwezi Juni, baada ya mkuu wa zamani wa idara ya ujasusi alipowasilisha malalamiko kwa polisi akidai kuwa rais huyo hakuripoti polisi wizi uliotokea mwezi Februari mwaka 2020 katika shamba lake kaskazini mashariki mwa nchi.

Katika malalamiko hayo Ramaphosa pia alidaiwa kuwa alipanga juu ya kutekwa nyara wezi hao na kisha kuwahonga ili wanyamaze.

**Chama cha ANC cha shujaa wa taifa la Afrika Kusini, Nelson Mandela, kimo madarakani kwa miaka 28 tangu kumalizika kwa ubaguzi wa rangi nchini humo, na kwamba kinaendelea kupoteza uungwaji mkono.**

Pia ilielezwa kuwa Rais huyo alikana kufanya makosa yoyote lakini kashfa dhidi yake na taarifa za kupatikana zaidi ya dola nusu milioni zilizofichwa kwenye mito ya makochi, zimetolewa wakati mbaya kwake kutokana na kwamba Desemba 16, Ramaphosa atagombea kwenye uchaguzi wa rais wa chama tawala cha ANC nafasi ambayo ni muhimu katika kumwezesha kuendelea kusalia kama rais wa taifa la Afrika Kusini.

Msemaji wa Rais Vincent Mangwenya alieleza kwamba Rais Ramaphosa anatilia maanani ujumbe kutoka kwenye matawi ya chama tawala ambayo yamemteua kugombea muhula wa pili wa uongozi wa Chama cha ANC, na kwamba anaelewa kuwa ujumbe huo unamaanisha kwamba unamtaka aendelee kuongoza ili afanikishe mageuzi ya serikali na kiuchumi.

Mangwenya aliongeza kwamba Ramaphosa kwa unyenyekevu na kwa uangalifu mkubwa na kujitolea kwake amekubali wito huo wa kuendelea kukihudumia chama chake cha ANC na watu wa Afrika Kusini.

Viongozi wa kamati ya chama tawala nchini Afrika Kusini wanatarajiwa kuamua siku ya iwapo wataendelea kumuunga mkono Rais huyo.

Ijumaa kamati hiyo kuu ya ANC ilifanya mazungumzo baada ya jopo la bunge kutoa ripoti iliyoashiria kupatikana ushahidi wa awali kuhusu kutendeka utovu wa nidhamu na kwamba huenda Rais Ramaphosa alikiuka sheria za nchi.

Aidha, ilibainishwa kwamba ripoti hiyo itapelekwa bungeni kesho Jumanne na hoja inaweza kuwasilishwa ya kupigwa kura ya kumwondoa madarakani Ramaphosa.

**MAAMUZI YA KIKAO**

Mweka Hazina Mkuu wa ANC, Paul Mashatile, aliviambia vyombo vya habari kuwa katika kikao hicho kifupi iliamuliwa kuwa ripoti hiyo ishughulikiwe kwanza na viongozi wakuu wa chama kabla ya kamati kuu kukutana tena.

Vyombo vya habari vya Afrika Kusini vimeendelea kuonesha imani kwamba Ramaphosa atasalia madarakani kwa kuwa anapendwa na umma.

Chama cha ANC cha shujaa wa taifa la Afrika Kusini, Nelson Mandela, kimo madarakani kwa miaka 28 tangu kumalizika kwa ubaguzi wa rangi nchini humo, na kwamba kinaendelea kupoteza uungwaji mkono.

Ramaphosa alichukua wadhifa wa kuliongoza taifa lililoendelea zaidi kiuchumi barani Afrika mwaka 2018, akiahidi kukomesha rushwa katika taasisi za serikali. **DW**



Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, akizungumza katika mahakama ya juu nchini humo, kuhusu tuhuma zinazomkabili. **PICHA: RFI**

# Urusi yapinga ukomo wa bei ya mafuta

**MOSCOW,** Urusi

NCHI ya Urusi imekosoa hatua ya mataifa ya magharibi ya kuweka ukomo wa bei kwa mafuta yake na kutishia kutopeleka nishati hiyo kwenye mataifa yatakayoridhia uamuzi huo.

Australia, Uingereza, Canada, Japan, Marekani na mataifa 27 ya Umoja wa Ulaya (EU) yalitangaza wiki iliyopita kuweka ukomo wa bei kwa mafuta ya Urusi wakisema watalipa dola 60 pekee kwa kila pipa.

Ukomo huo wa bei unatarajiwa kuanza kufanya kazi leo pamoja na marufuku ya EU dhidi ya kununua mafuta yanayosafirishwa kwa njia ya bahari kutokea Urusi.

Mataifa hayo ambayo ni washirika wa Ukraine yanatumai ukomo kwa bei ya mafuta ya Urusi utaongeza ugumu kwa mapato ya Moscow yatokanayo na mauzo ya nje ya nishati hiyo na hatimaye kupunguza uwezo wa Urusi kuendelea na vita.

Msemaji wa Ikulu ya Urusi, Kremlin, Dmitry Peskov (pichani), alisema Urusi inahitaji muda kufanya tathmini ya hatua hiyo ya mataifa ya magharibi kabla ya kutangaza vipi itajibu suala hilo. Hata hivyo imesisitiza kwamba kamwe haitokubali mafuta yake kuwekewa ukomo wa bei.



Mwakilishi wa kudumu wa Urusi kwenye mashirika kadhaa ya kimataifa huko mjini Vienna, Mikhail Ulyanov, alionya kwamba mataifa ya Ulaya yatakayounga mkono uamuzi huo yatajutia uamuzi wake.

"Kuanzia mwaka huu, Ulaya itaishi bila mafuta ya Urusi," alindika Ulyanov kupitia mtandao wake wa Twitter.

"Moscow imekwishaweka wazi kwamba haitouza mafuta yake kwa nchi zitakazounga mkono ukomo wa bei ambao ni kinyume na bei inayokubalika na soko. Subirini, hivi karibuni EU itaituhumu Urusi kutumia mafuta kama silaha," alisema.

Wakati Moscow ikitoa msimamo huo, ofisi ya Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelenskyy, iliyataarifu mataifa ya magharibi kuweka ukomo wa bei ya chini kabisa, ikisema ule uliofikiwa na mataifa ya EU na kundi la nchi tajiri la G7 hautoshelezi.

"Itakuwa muhimu kupunguza bei ya pipa hadi dola 30 ili kuuharibu uchumi wa adui haraka," aliandika Andriy Yermak, mkuu wa ofisi ya Rais Zelenskyy kupitia ukurasa wa mtandao wa Telegram.

Mtizamo huo wa Ukraine ni sawa na ule uliotolewa na Poland iliyotaka bei ya chini zaidi kwa mafuta ya Urusi. Poland ni miongoni mwa wakosoaji wa mstari wa mbele wa vita vya Urusi nchini Ukraine.

Chini ya makubaliano ya siku ya Ijumaa, kampuni za bima na nyinginezo zinazohitaji kusafirisha mafuta ya Urusi zitapaswa kuchukua yale yanayouzwa kwa bei ya dola 60 kwa pipa au chini ya kiwango hicho.

Sehemu kubwa ya kampuni za bima na usafirishaji mafuta zinaendesha shughuli zake ndani ya EU au Uingereza na zitalazimika kutii ukomo uliowekwa. **DW**

# Walimu wachangia choo na wanafunzi

## • Watawa wawasitiri walimu wa kike

**Na Waandishi Wetu,**
waliokuwa HAI

NI safari ya saa moja kwa daladala kutoka mji mdogo wa Bomang'ombe hadi eneo la Mferejini, njiapanda ya Narumu wilayani Hai, panapotikana shule mbili zenye taarifa ya ukakasi, walimu wanachangia choo na wanafunzi wao.

Unapofika Mferejini, safari inaunganishwa na bodaboda hadi kijijini Usari, Kata ya Machame-Narumu, penye ushuhuda huo wa shule za msingi jirani, Usari na Narumu.

Faragha hiyo walimu wa kike wanalazimika kwenda kwa majirani watawa wa Kanisa Katoliki Parokia ya Narumu, wakati walimu wa kiume wanachangia choo na wanafunzi.

Ikirejewa madarasani, kuna uhaba, pia uchakavu mkubwa, huku walimu hawana makazi. Kimsingi, Nipashe imeshuhudia nyufa, kuta zilizochakaa, sakafu iliyobanduka, milango na madirisha hali ni mbaya.

### MKUU ANENA

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Narumu, Anna Minja, anaeleza shule hiyo ina miaka 79, yaani ilianzishwa mwaka 1943 na sasa ina jumla ya wanafunzi 322 na walimu sita.

Anayataja matatizo hayo ya miundombinu na kitaalamu yamedumu kuwa kikwazo kikubwa kwa tija ya shule, akiainisha kuna upungufu wa madarasa mawili.

"Kwa hiyo, tunaomba serikali itusaidie kwa hili. Upungufu wa vyumba vya madarasa ni kwa darasa la kwanza na chekechea (darasa la awali). Hivi sasa darasa la kwanza wanapokezana na darasa la chekechea," anafafanua.

Jirani yake, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Usari, Mwombeki Rwegoshora, anasema shule yake ina wanafunzi 450 na walimu sita.

"Choo kilichokuwapo awali kilijengwa kati ya mwaka 1950 na 1953. Ni dhaifu na hakifai kabisa kwa matumizi ya binadamu," anasema.

Ni hoja inayoungwa mkono na Mwenyekiti wa Kijiji cha Usari, Ismail Urassa anayesema: "Wanafunzi walikuwa hawana choo maana kilibomoka, tukakikarabati. Sasa tumebaki na tatizo hili la kukosekana choo cha walimu.

"Tumeshatoa taarifa kwenye mikutano ya hadhara kuhusu suala hili la kukosekana choo cha walimu shuleni. Shida tuliyonayo ni ukosefu wa fedha, tumefikiria tutengeneza choo cha walimu kwa kuelekeza majitaka kwenda shimo la choo cha wanafunzi ili kupunguza bajeti. Itapendeza kama kila shule itakuwa na choo kwa ajili ya walimu wake."

Fadhila Omari mkazi wa Kijiji cha Usari ana angalizo kuhusu kinachojiri shuleni, kwamba kunawaweka hatarini walimu na wanafunzi kukumbwa na magonjwa ya mlipuko, akitoa mfano wa kipindupindu na kuhara.

"Kukitokea mlipuko huo, kwa hali iliyoko kwenye vyoo vya shule, ni wazi wanafunzi hawatohudhuria darasani na hivyo kufanya vibaya kwenye masomo yao," anatahadharisha.



Wanafunzi wa darasa la kwanza katika Shule ya Msingi Narumu wakiendelea na vipindi wakiwa wamekaa kwenye mti kutokana na kukosa darasa. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**



Choo kinachotumiwa na walimu na wanafunzi wa Shule ya Msingi Usari.

Mwenyekiti wa Kamati ya Shule ya Msingi Narumu, Evarist Gasper, anawasilisha hatua zilizoanza kukabili madhila hayo, wamepokea mifuko 50 ya saruji kutoka Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo.

"Tulipanga tuielekeze moja kwa moja katika ujenzi wa choo cha walimu katika Shule ya Msingi Narumu, lakini baadaye tukaona ni vyema tufanye kwanza ukarabati wa madarasa, kwa sababu wanafunzi wanatumia madarasa ambayo yamejaa vumbi.

"Tukishamalizana na ukarabati wa madarasa, tuhamie kwenye suala la choo na tumeanza vikao vya mchakato," anasema.

Mtazamo mpana wa hatari uliyoko sasa ambayo Nipashe imebaini, pia ikijiri katika Shule ya Msingi Roo iliyoko Kata jirani ya Romu, ikigusa ustawi wa elimu na afya ya jamii shuleni.

### SERIKALI WILAYANI

Diwani wa Machame-Narumu (CCM), John Lengai anakiri tatizo kwenye kata hiyo, shule zake mbili za msingi na moja ya sekondari hazina vyoo kwa ajili ya walimu.

"Shule ya Sekondari Tumo ni miongoni mwa shule ambazo walimu hawana vyoo kabisa. Kuna shule zingine za msingi, Narumu na Usari nazo zimesahaulika katika hilo. Kwenye hizo shule, walimu hawana vyoo kabisa na wanalazimika kujisaidia kwenye vyoo vya wanafunzi.

"Shule hizi, walimu wanapata shida sana. Kwa mfano, katika Shule ya Msingi Usari walimu wa kike wanajisaidia kwenye choo cha masista wa Roman Catholic (watawa wa Kanisa Katoliki).

"Walimu wa Shule ya Msingi Narumu wanajisaidia katika vyoo vya wanafunzi. Yaani mwanafunzi yupo nje anamsubiri mwalimu atoke. Hili si jambo nzuri kwenye jamii yetu, tutafute namna bora wajisitiri," anasema.

Kutokana na dharura hiyo, Diwani Lengai anaiomba Halmashauri ya Wilaya ya Hai iupe uzito wa kipekee kwenye bajeti zake zijazo ujenzi wa vyoo vya Sekondari ya Tumo, pia Shule za Msingi Usari na Narumu.

Mkuu wa Wilaya ya Hai, Juma Irando anakiri hali mbaya inayoshuhudiwa, akitamka: "Nimezitembelea hizo shule za Tumo na Roo, ni aibu na inasikitisha sana! Nimemwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri na Mwenyekiti wa Halmashauri, watenge fedha kupitia mapato ya ndani kwa ajili ujenzi wa vyoo vya walimu.

"Nimeagiza waanze na shule hizi mbili za Roo na Tumo ambazo binafsi nimeziona, ili walimu wafanye shughuli zao bila kuwa na wasiwasi au fedheha."

Nipashe inabisha hodi ofisini kwa Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Hai, David Lekei anayekiri kupokea maelekezo ya Mkuu wa Wilaya na anaahidi kuyatekeleza.

Mbunge wa Hai (CCM), Saashisha Mafuwe anakumbusha historia ya shule za msingi na sekondari zilizoko Hai, kwamba nyingi zilijengwa kati ya miaka 1920 na1950, hivyo zimechakaa.

"Hivi ninavyozungumza (Novemba 3 mwaka huu), kuna shule 13 ni chakavu sana. Ni za kuvunja na kujenga upya! Miundombinu ya madarasa ni chakavu, miundombinu ya vyoo pia ni chakavu.

"Kimsingi, tatizo hili la miundombinu chakavu ni shida kubwa ndani ya Jimbo la Hai, na nilishazungumza mbele ya Mheshimiwa Rais (Samia Suluhu Hassan) alipotutembelea.

"Nilimwomba atupe upendeleo maalum kwa ajili ya hizi shule chakavu. Alitukubalia na tulishawaandikia TAMISEMI (Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa), fedha zinakuja lakini haziji kwa ukamilifu, hivyo tatizo hili bado lipo, tunaendelea kusubiri ahadi ya Mheshimiwa Rais Samia kutuletea fedha.

"Ninachukua nafasi hii kuwakumbusha watu wa Hai kurudi nyumbani kusaidia maendeleo ya kwao. Unajua hizi shule zilijengwa na wazee wetu na kuna wana Hai wako Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza, Mbeya na wana maisha mazuri. Serikali haiwezi kufanya kila kitu. Utamaduni wetu watu wa Hai ni kushirikiana na serikali, na ndicho kilichotusaidia shule nyingi zikajengwa," anashauri.

### KUTOKA NGO

Mkurugenzi wa taasisi binafsi, Voice of Empowered Women Foundation, Asifiwe Mallya ana angalizo lake: "Shule inapokuwa na miundombinu duni, ujifunzaji kwa wanafunzi na ufundishaji kwa walimu unakuwa duni, kunakuwa na utoro kwa walimu na kushuka kwa umahiri katika ufundishaji.

"Niiombe serikali itafute fungu mahali popote ili iwajengee vyoo walimu hawa wa shule za msingi Narumu na Usari ili waondokane na aibu wanayoipata kwa sasa."

### SERA NA CAG

Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 inaelekeza uwiano sahihi shuleni kwamba tundu moja la choo litumiwe na wanafunzi 20 wa kike na wa kiume 25. Pia kila shule iwe na choo cha walimu.

Kwa mantiki hiyo, kunahitajika walau matundu 20 shuleni Usari kwa ajili ya wanafunzi 420 walioko; pia matundu 12 kukidhi mahitaji ya wanafunzi 322 wa shuleni Narumu.

Sera hiyo pia inaelekeza kila mwalimu awe na nyumba yake inayojitegemea, mambo ambayo hayapo shuleni Narumu na Usari.

Katika ripoti yake ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Mitaa kwa Mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni jijini Dodoma Aprili 12, mwaka huu, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, anabainisha halmashauri 77 zina uhaba wa vyumba vya madarasa 74,735, nyumba za walimu 73,135, ofisi za walimu 5,112, viti 65,889, meza 185,840 na matundu ya vyoo 111,931, akipendekeza serikali ichukue hatua za haraka kuboresha miundombinu iliyoko na kujenga mipya.

BURUDANI

# Whozu afunguka mimba ya Wema

Na Mwandishi Wetu

NYOTA wa muziki wa Bongo Fleva, Whozu, amethibitisha kuwa ni kweli alimpa ujauzito mpenzi wake, Wema Sepetu ila uliharibika.

Katika mahojiano na waandishi wa habari, Whozu alibainisha kuwa kuharibika kwa ujauzito wa Wema ilikuwa ni bahati mbaya.

Mwanamuziki huyo alieleza kusikitishwa kwake na watu waliotilia shaka habari za yeye kumpa ujauzito mpenzi wake huyo.

"Iliniuma. Halafu watu wanafikiria ni uwongo! Mnanionaje kuwa mimi siwezi kumpa mtu mimba? Mnanichukuliaje?" Alisema.

Alidokeza kuwa anapanga kumpa tena Wema ujauzito kwa mara nyingine baada ya ule wa kwanza kutofikia hatua ya kujifungua.

Whozu alisema kuwa yeye na mpenzi wake wanatamani kupata mtoto wa kiume pamoja.


Mwimbaji huyo alisema kuwa bado anafanya juhudi nyingi na pia anamwombea sana mpenzi wake apate ujauzito tena.

Haya yalijiri baada ya Wema kueleza hamu yake ya kupata mtoto wa kwake na kumwomba Mungu amjalie.

Ijumaa, aliandika ombi la mtoto chini ya picha yake akiwa amemshika mtoto mchanga ambayo aliiweka kwenye Instagram.

"Eh Mungu tafadhali nibariki na wangu siku moja," aliandika.





# WIZKID AIPONDA HIP HOP

**London,** England

MWANAMUZIKI wa Nigeria, Wizkid ameviteka vichwa vya habari vya mitandao yote ya burudani, baada ya kauli yake kwamba muziki wa Hip Hop umekufa.

Kwenye mahojiano na 10 Magazine ambayo yametoka juzi, Wizkid alikaririwa akisifia ukuaji wa muziki wa Afrobeats kimataifa huku akiukandia muziki wa rap.

Wizkid alisema mbali na Afrobeats, huwa hasikilizi aina nyingine ya muziki hasa wa rap kwa sababu nyimbo nyingi zinazotengenezwa zinaboa.

"Nikiwa mkweli tu, sisikilizi aina nyingine yoyote ya muziki tena. Sisikilizi rap, huo upuuzi unaniboa.

"Tayari umekufa, umechoka mbaya. Hawa jamaa wanafanya kitu kile kile cha kipuuzi kwenye midundo ile ile na miondoko ile ile," alikaririwa Wizkid.

Hata hivyo, hakuishia hapo, aliendelea na mashambulizi yake juu ya rap ambapo alihamia kwenye mtandao wa Snapchat na kuandika madongo kwamba, angalau anawakubali Nasty C, Sarkodie na Black Sherif kwa hapa Afrika, ila wengine wote ni ovyo tu na ni watu waliofulia.

# *Wolper atoa la moyoni*

Na Mwandishi Wetu

MREMBO wa Bongo Muvi, Jacquline Wolper, amesema kupitia tukio la harusi yake, limemfanya ajifunze mambo mengi na kujua watu wake wa kushikana nao na wasio wa kwake.

Wolper amesema, yeye si mnafiki hivyo, ila amegundua watu ambao sio marafiki zake, anawaacha waende na maisha yao, lakini wale ambao amewaona ni wake, ataendelea kushikana nao kwenye shida na raha.

"Eeeh kama mtu sio wangu pita huku na mimi napita kule, mimi sio mnafiki. Nikiona huendani na mimi basi unapita njia yako na mimi yangu.

"Nimejifunza si tu kwamba kwa kutokuja kwenye harusi yangu ila kuna vitu vingi," alisema.



# SIMBA QUEENS, JKT QUEENS KUKATA UTEPE WA LIGI KESHO

**Na Saada Akida**

LIGI Kuu ya Wanawake Tanzania Bara inatarajiwa kuanza kutimua vumbi kesho, Jumanne kwa mabingwa watetezi, Simba Queens, kukata utepe wa msimu mpya wa 2022/23 dhidi ya JKT Queens katika mechi itakayopigwa Uwanja wa Mo Simba Arena ulioko Bunju nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam.

**Kesho kutakuwa ni mchezo huo mmoja tu wa ufunguzi huku ligi hiyo ikitarajiwa kuendelea kesho kutwa, Jumatano ambapo itapigwa michezo minne kwa Yanga Princess kuikaribisha Fountain Gate Princess katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.**

Michezo mingine itakayopigwa siku hiyo ni kati ya The Tiger Queens na Mkwawa Queens utakaochezwa Uwanja wa Black Rhino jijini Arusha, huku Alliance Girls wakiwa nyumbani dhidi ya Ceasiaa Queens katika Dimba la Nyamagana jijini Mwanza na Amani Queens ikiwakaribisha Baobab Queens katika Uwanja wa Ilulu mkoani Lindi.

Kocha Mkuu wa Simba Queens, Charles Lukulu, raia wa Uganda, amesema amefanya maandalizi mazuri kuelekea msimu huo na anaamini timu yake itatetea taji lao la ubingwa msimu huu.

Alisema kwa mujibu wa taarifa alizozipata kutoka kwa wasaidizi wake, wapinzani wao wamefanya usajili mzuri, hivyo anatarajia kuona ligi yenye ushindani mkubwa, lakini watapambana kuhakikisha wanatetea taji lao.

"Ligi itakuwa ngumu kwa sababu timu zimejiandaa vizuri, zimefanya usajili kuboresha vikosi vyao kwa lengo la kutoa ushindani mkubwa, kwangu nimeandaa kikosi changu kwa ajili ya kwenda kupigania taji ambalo tunalo sasa, kuhakikisha halitunyang'anywi kuchukuwa kwa mara nyingine," alisema Lukulu.

Kocha wa Yanga Princess, Edna Lema, kwa upande wake alisema wameandaa timu yenye ushindani mkubwa kwa sababu wanatambua msimu huu ligi itakuwa ngumu, hivyo wamejipanga na kufanya usajili kuboresha vikosi vyao.

"Msimu huu itakuwa ligi ya kuvutia na ngumu kwa sababu kila timu imefanyia kazi madhaifu yao hasa kwa tuliokuwapo msimu uliopita na kushindwa kufikia malengo yetu, tayari tumeandaa timu kwa ajili ya kutorudia makosa yaliyopita na kuhakikisha tunakuwa bora," alisema kocha huyo.

Naye Kocha wa JKT Queens, Haule Grayson, alisema anaimani msimu huu utakuwa wa ushindani kwa sababu ya maandalizi ya timu shiriki pamoja na ujio wa timu mpya ambazo zimepanda daraja msimu huu.

"Tumejipanga vizuri hatutaki kuwa wanyonge hasa kwa hizi klabu mbili za Kariakoo Simba na Yanga, JKT Queens tumefanya usajili mzuri na msimu huu tunahitaji kurejesha heshima yetu ambayo tuliipoteza misimu ya nyuma," alisema Haule.

## LA KWANZA HILO...



Moses Phiri akiifungia Simba bao la kwanza wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Coastal Union kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Mkwakwani juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Biashara United yapiga mtu mkono

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Biashara United juzi ilizinduka kutoka usingizini kwenye Ligi ya Championship na kuachia kipigo kizito cha mabao 5-0 dhidi ya Green Warriors, mechi ikipigwa Uwanja wa Karume, Musoma mkoani Mara.

Ushindi huo umeipeleka timu hiyo hadi nafasi ya tisa kwenye msimamo wa ligi hiyo ambayo ipo kwenye raundi ya 12, ikiwa na pointi 17.

Vinara wa ligi hiyo, JKT Tanzania waliendelea kujiweka kwenye mazingira mazuri ya kupanda Ligi Kuu msimu huu moja kwa moja bila zengwe, baada ya kuwachapa wapinzani wakubwa kwenye msimamo huo Kitayosce kwa mabao 3-1 kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Dar es Salaam na kuzidi kujikita kileleni mwa msimamo wa Ligi ya Championship.

Kwa ushindi huo, maafande hao wanaongoza ligi hiyo kwa tofauti ya pointi tano, ikifisha jumla ya pointi 31, na kuiacha Kitayosce kwenye nafasi ya pili, lakini ikibaki na pointi zake 26.

Timu ya Pamba imepanda kwenye msimamo wa ligi hadi nafasi ya tatu ikifikisha pointi 25, baada ya kuidungua Mbuni bao 1-0, mechi ikipigwa Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza. Mbuni imezidi kuporomoka na sasa ipo nafasi ya sita na pointi zake 18.

Mbeya Kwanza ambayo msimu uliopita ilikuwa Ligi Kuu, imezidi kujitutumua kutaka nayo kurejea hata kwa 'play off' kwa kuisulubu Transit Camp mabao 2-0, mechi ikichezwa kwenye uwanja ambao tangu ilipokuwa Ligi Kuu iliufanya wa nyumbani, Majimaji, Songea mkoani Ruvuma.

Ni ushindi ulioipeleka hadi nafasi ya tano ya msimamo ikiwa na pointi 21, ikiwaacha maafande hao wa JWTZ wakiwa nafasi ya 12 na pointi zao 12.

KenGold nayo iliachia kipigo cha mabao 5-2 dhidi ya Pan African, mechi iliyochezwa Uwanja wa Sokoine Mbeya, huku Ndanda ikifa kwao, Uwanja wa Nangwanda Sijaona kwa bao 1-0 dhidi ya Copco.

# Mabondia wanawake wafundwa

**Na Shufaa Lyimo**

MWAMUZI wa Kimataifa wa mchezo wa Ngumi za Kulipwa nchini, Pendo Njau, amewataka wanawake kujitokeze kushiriki semina mbalimbali zinazoandaliwa na Chama cha Ngumi za Kulipwa Tanzania (TPBC), ili kujiongezea maarifa katika masumbwi.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, alisema kama wanawake watakuwa na utamaduni wakuhudhuria semina hizo mara kwa mara, watajifunza mambo mengi ambayo hawayafahamu.

"Ninawashauri wanawake wenzangu kupenda kushiriki semina mbalimbali zinapotokea, watapata vitu vingi vinavyohusiana na mchezo huu," alisema Njau ambaye amejizolea sifa nyingi kwa uchezeshaji bora wa mapambano makubwa nchini.

"Ngumi zinazidi kukua siku hadi siku, tunaona vipaji vipya vinazaliwa kila muda, naamini ndani ya miaka miwili ijayo Tanzania itafika mbali kupitia mchezo wa ngumi," alisema.

Alisema alifurahishwa na mabondia wanawake ambao walijitokeza kushiriki semina ya mchezo huo ambayo ilifanyika mwezi uliopita katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

# Black Sailor FC yainyoa Kipanga

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Black Sailor imefanikiwa kupata ushindi wake wa pili kati ya michezo 15 aliyocheza katika Ligi Kuu Zanzibar.

Black Sailor hapo juzi iliifunga timu ya Kipanga FC 2-1 katika mwendelezo wa ligi hiyo ikiwa ni mchezo wa mwisho wa kukamilisha mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Zanzibar, ambao uliochezwa Dimba la Amaan majira ya Saa 11 jioni shukrani kwa mabao ya Mustafa Hamadi dakika ya tisa na Mazuya Simba dakika ya 27 wakati bao la Kipanga likipachikwa nyavuni na Neva Kaboma dakika ya 90.

Kwa matokeo hayo, Black Sailor imepaa kwa nafasi mbili kutokea mkiani mwa msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar hadi nafasi ya 14 ikiwa na alama 10 mkononi.

Awali akizungumza na gazeti hili, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Saleh Machupa alisema malengo ya timu hiyo ni kuhakikisha inakwenda dirisha dogo ikiwa na alama 10 ili kujipanga vema kuelekea mzunguko wa lala salama.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### CITY KUMUUZA GREALISH

KLABU ya Manchester City itakuwa tayari kumuuza mchezaji wao aliyevunja rekodi ya usajili, Jack Grealish, 27, ili kufadhili usajili wa kiungo wa kati wa England, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 19, kutoka Borussia Dortmund. ***(Football Insider)***

### CODY HAFIKIRII HATIMA

BAADA ya kuisaidia Uholanzi kufika robo fainali ya Kombe la Dunia, Cody Gakpo hafikirii kuhusu mustakabali wake hadi "labda tutakapokuwa mabingwa". ***(Sport)***

### RONALDO BADO HAJAAMUA

NYOTA wa Ureno, Cristiano Ronaldo, 37, bado hajaamua kama atakubali ofa ya pauni milioni 173 kwa mwaka kutoka kwa Klabu ya Al-Nassr ya Saudi Arabia. Mshambuliaji huyo wa zamani wa Manchester United ataamua tu mustakabali wake baada ya Kombe la Dunia. ***(Sunday Mirror)***

### GVARDIOL AWINDWA EPL

NIA ya Tottenham Hotspur na Chelsea kumnunua beki wa kati wa RB Leipzig na Croatia, Josko Gvardiol, 20, inaongezeka kabla ya dirisha la uhamisho la Januari. ***(Corriere dello Sport)***

### MEUNIER KUTAFUTA TIMU

KAMA Barcelona haitamtafuta Thomas Meunier, 31, wa Borussia Dortmund basi beki huyo wa kulia wa Ubelgiji atasikiliza ofa kutoka kwa klabu nyingine zikiwamo AC Milan, Juventus, Manchester United. ***(Mundo Deportivo)***

### ASENSIO ATAKIWA ARSENAL

ARSENAL ina nia ya kumsajili winga wa Real Madrid na Hispania, Marco Asensio, 26, katika dirisha la Januari. ***(Calciomercato)***

### CUNHA KUTUA WOLVES

MSHAMBULIAJI wa Atletico Madrid na Brazil, Matheus Cunha, 23, anatazamiwa kujiunga na Wolves katika dirisha la uhamisho la Januari. ***(Cadena Ser)***

### GAKPO ATAJWA LEEDS

KOCHA wa Leeds United, Jesse Marsch, amesema klabu hiyo "ilikuwa karibu sana" kumsajili Cody Gakpo, 23, kutoka PSV Eindhoven Agosti mwaka huu na Manchester United sasa iko tayari kufuatilia nia yao ya kumnunua mshambuliaji huyo wa Uholanzi katika dirisha laJanuari. ***(90 Min)***

### ZUBIMENDI AMULIKWA UNITED

KLABU ya Manchester United iko tayari kulipa kitita cha pauni milioni 51.4 kumnunua kiungo wa kati wa Real Sociedad na Hispania, Martin Zubimendi, 23. ***(AS)***

### LUKAKU KUONGEZWA INTER

INTER Milan inataka kumsajili mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku, 29, kwa mkopo kwa msimu mwingine kutoka Chelsea. ***(Gazzetta dello Sport)***

### MOURA BADO FLAMENGO

KLABU ya Flamengo inafuatilia hali ya Lucas Moura, 30, wa Tottenham Hotspur baada ya klabu yake ya zamani ya Sao Paulo kushindwa kumnunua. ***(Bolavip)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA



# MESSI AKATAA KUSHEREHEKEA KUFIKISHA MECHI YA 1,000

**AL RAYYAN,** Qatar

LIONEL Messi amesema hatasherehekea hatua yake kibinafsi ya kufikisha mechi 1,000 tangu aanze kucheza soka, baada ya kuisaidia Argentina kushinda 2-1 dhidi ya Australia katika hatua ya 16-bora ya Kombe la Dunia 2022.

**Messi mwenye umri wa miaka 35, aliifungia Argentina bao la kwanza kabla ya Julian Alvarez kufunga la pili katika kipindi cha pili na kuwawezesha kuondoka na ushindi huo.**

Mechi hiyo ilikuja siku mbili tu baada ya kuifunga Poland katika mchezo wao wa mwisho wa hatua ya makundi na kujihakikishia nafasi ya kufuzu.

> ●●● Nina furaha sana kwa kupiga hatua nyingine mbele, kufikia lengo...

Messi alikuwa katika hali nzuri tena na alitangazwa kuwa mchezaji bora wa mchezo huo.

Lakini licha ya kufikia hatua nyingine ya maisha na kuvuka alama ya Diego Maradona ya mabao nane ya Kombe la Dunia, Messi hatambui mafanikio hayo binafsi.

"Nina furaha sana kwa kupiga hatua nyingine mbele, kufikia lengo lingine," alisema Messi alisema baada ya mechi hiyo.

"Ilikuwa mechi kali na ngumu tulijua itakuwa hivi. Hatukuwa na muda mwingi wa kupumzika na tulikuwa na wasiwasi kwani tulijua itakuwa mechi ya kimwili na walikuwa na nguvu sana."

Alipoulizwa kwenye TV ya Argentina kama atasherehekea mechi yake ya 1,000, Messi alijibu: "Hapana, hapana. Huu ulikuwa mchezo mgumu, hatukuwa na mapumziko mengi, hatukuwa tumepona vizuri, ulikuwa mchezo wa kimwili sana.

"Tulipogundua tutalazimika kucheza tena baada ya siku tatu, tulisema ni wazimu na si kupumzika vya kutosha, lakini wakati huo huo tulitaka kuwa hapa kwa jinsi tunavyojisikia na kwa nini hii inawakilisha kwa mashabiki wetu."

Argentina sasa inaelekea kwenye robo fainali ya Kombe la Dunia dhidi ya Uholanzi hapo Ijumaa wiki hii.

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
POLISI TANZANIA
VERSUS
AZAM
1 | 4.18
X | 3.06
2 | 1.87

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# VAN GAAL AUONA UBINGWA UHOLANZI KOMBE LA DUNIA

**DOHA,** Qatar

LOUIS van Gaal anajua kuna safari ndefu, lakini alitangaza kwamba, Uholanzi inaweza kubeba Kombe la Dunia nchini Qatar.

Kikosi cha Van Gaal kimetinga robo-fainali ya Kombe la Dunia, ambapo kitacheza na Argentina ya Lionel Messi baada ya kupata ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Marekani kwenye Uwanja wa Kimataifa wa Khalifa, Jumamosi.

Memphis Depay na Daley Blind walifunga kipindi cha kwanza, huku Denzel Dumfries ambaye aliisaidia Uholanzi mabao mawili ya kwanza - akifunga la tatu baada ya Haji Wright kurudisha bao moja kwa Marekani.

Mtazamo wa kimantiki wa Van Gaal ni kwamba timu yake sasa imeimarika zaidi na inaweza kuwa mabingwa wa dunia.

“Napata shukrani za kutosha kutoka kwa watu wanaonizunguka,” alisema Van Gaal katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi hiyo alipoulizwa kama anaamini alihitaji kushinda shindano hilo ili kupata heshima kutoka kwa baadhi ya wakosoaji wake.

“Najua vyombo vya habari huwa haviripoti kwa njia chanya, ni suala la soka, lakini bado tuna mechi tatu mbele yetu. “Tunaweza kuwa mabingwa wa dunia. Sisemi kwamba tutaweza, lakini tunaweza.”

Uholanzi imefuzu kutoka mechi tano kati ya sita za mwisho za raundi ya 16-bora kwenye Kombe la Dunia, ikiwa ni pamoja na kusonga mbele kutoka kwa mechi tatu za mwisho katika hatua hii.



# Afya ya Pele sasa yaimarika

**RIO DE JANEIRO,** Brazil

GWIJI wa soka wa Brazil, Pele, anaendelea vizuri na matibabu ya ugonjwa wa kupumua na hali yake ya afya haijazidi kuwa mbaya zaidi ya saa 24 zilizopita, katika Hospitali ya Albert Einstein anapotibiwa.

“Edson Arantes do Nascimento alilazwa katika Hospitali ya Israelite Albert Einstein Jumanne iliyopita kwa ajili ya kufanyiwa tathmini ya matibabu yake ya uvimbe kwenye utumbo mpana, ambao uligunduliwa Septemba 2021. Bado anaendelea na matibabu na hali yake ya kiafya bado inaendelea vizuri,” ilisema taarifa ya hospitali hiyo.

Pele mwenye umri wa miaka 82, amekuwa hospitalini tangu Jumanne na Jumamosi, aliandika ujumbe kwenye ukurasa wake wa Instagram uliosomeka: “Marafiki zangu, nataka kuweka wazi. Nina nguvu, na matumaini mengi na ninafuata matibabu yangu kama kawaida. Nataka kuwashukuru timu nzima ya matibabu na uuguzi kwa huduma zote ambazo nimepata.

“Nina imani nyingi kwa Mungu na kila ujumbe wa upendo ninaopokea

kutoka ulimwenguni kot
hunifanya nipate nguvu
Ujumbe wa kumtaki
heri umemiminika ku
toka duniani kote kw
mshindi huyo mara tat
wa Kombe la Dunia, am
baye anaendelea na ma
ibabu ya saratani.
Kely Nascimento, bin
tiye Pele, alichapish
picha kadhaa kweny
Instagram kutoka kw
mashabiki wa Brazil nch
ni Qatar wakimtakia he
babake kwa bendera n
mabango.
Majengo katika tai
hilo la Mashariki ya Ka
pia yalionyesha jumbe z
kumuunga mkono nyot
huyo wa soka.

CHEZA USHINDE KASINO

# 'YANGA IMEIPONZA IHEFU'

Na Adam Fungamwango

KOCHA Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Mexime, amesema Ihefu ilitumia nguvu sana ilipocheza mechi dhidi ya Yanga, hivyo wachezaji wake walikuwa wachovu na hiyo ndiyo mbinu aliyoitumia kuiangamiza kwa mabao 2-0 Ijumaa katika Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Mexime amesema siri ya ushindi kwa timu yake ni maelekezo aliyoyatoa kwa wachezaji wake akiwaambia wasicheze kwa nguvu kipindi cha kwanza, badala yake wazitunze mkapa kipindi cha pili kwa sababu Ihefu watakuwa wamechoka kutokana na kutumia nguvu kubwa kwenye mechi dhidi ya Yanga, pamoja na uchovu wa safari.

"Nilijua watachoka, walitumia nguvu kubwa kipindi cha kwanza na wametoka kucheza mechi ngumu ambao walitumia nguvu nyingi dhidi ya Yanga, pamoja na usafiri kutoka Mbeya hadi Mwanza, kipindi cha pili nikawaambia wachezaji wake sasa wafunguke na kushambulia sana kwa sababu watakuwa na fatiki na kweli tukapata mabao mawili," alisema kocha hiyo.

**Yalikuwa ni mabao mawili ya Erick Mwijage dakika ya 67 na mkongwe Hamisi Kiiza dakika ya 84.**

Kocha huyo aliwapongeza wachezaji wake kwani alichowaagiza kufanya ndicho walichokwenda kukitekeleza.

Kocha msaidizi wa Ihefu, Themi Felix, alikiri uchovu ndiyo uliowaangusha kwenye mechi hiyo.

"Tunashukuru kwa yote, tumecheza na Geita Gold Novemba 25 na Novemba 29 tukacheza na Yanga mechi kubwa, ambayo wachezaji wetu walipambana sana pamoja na Kagera Sugar leo (Desemba 2), tulitegemea 'fatiki' kwa wachezaji wetu. Nguvu iliyotumika kwenye mechi zilizopita hasa na Yanga ni kubwa, hivyo umakini umepotea kwa sababu ya uchovu wa mwili, tumefungwa mabao 2-0 tumekubali, tumemaliza mzunguko wa kwanza sasa tunarudi nyumbani kujipanga, kwenye msimamo wa ligi hii wenzetu hawapo mbali, tutapambana kwenye mzunguko wa pili," alisema straika huyo wa zamani wa timu iliyowafunga, Kagera Sugar.

Wakati Kagera Sugar ilimaliza mzunguko wa kwanza ikiwa na pointi 21, Ihefu ina pointi 11, nafasi zao kwenye msimamo zitategemea matokeo ya mechi za timu zingine za kumalizia mzunguko huo.

## Mgunda na ushindi Simba

INATOKA UKURASA 32

Mgunda alisema ilikuwa ngumu kwa sababu anaifahamu, hivyo haijalishi matokeo au nafasi waliyokuwa nayo.

"Nilisema tangu mwanzo kuwa Coastal Union ni ngumu, haijalishi matokeo ya mechi zake, haijalishi nafasi waliyokuwa nayo, mimi ni mmoja kati ya watu ambao wameshiriki kuwatengeneza wale vijana kwa hiyo nilikuwa najua uzito na nguvu iliyopo, hivyo tumeshinda katika mchezo mgumu. Mwisho wa yote tumepata pointi tatu, tunajipanga na mechi inayokuja na sisi," alisema.

Kuhusu kipa Aishi Manula, kutorejea dimbani kipindi pili, alisema alicheza huku akiwa anaumwa malaria na tumbo, lakini aliwahakikishia kuwa anaweza kukaa langoni na kama akizidiwa basi atawaambia, na ndivyo ilivyotokea, kwani kipindi cha pili akaomba kufanyiwa mabadiliko.

Kocha Yusup Chipo wa Coastal Union, alisema wachezaji wake walicheza kwa tahadhari sana kipindi cha kwanza, lakini kipindi cha pili walifanya makosa kadhaa ambayo Simba wameyatumia kuwaadhibu.

"Tumefungwa mabao mepesi sana, inafaa tukomae kidogo sisi Coastal Union hasa kwenye mechi za mzunguko wa pili, tusiwe tunafanya makosa kama haya," alisema kocha huyo raia wa Kenya.



Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Mexime.

## *Mayele, Phiri wapishana*

INATOKA UKURASA 32

pointi nne wakati Azam nayo ikimaliza mzunguko wa kwanza kwa ushindi itapaa hadi nafasi ya pili kwa kufikisha alama 35 moja zaidi ya Wekundu wa Msimbazi hao.

Katika mbio za kuwania Kiatu cha Dhahabu cha Ligi Kuu Bara, mbali na Phiri na Mayele, pia wamo Sixtus Sabilo wa Mbeya City mwenye mabao saba, huku Idris Mbombo na Reliants Lusajo wa Namungo kila mmoja akiwa na mabao sita, wakati Moubarack Amza wa Coastal Union akiwa amecheka na nyavu mara matano.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" – NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" – NI TIMU KUTOKA SARE
"2" – NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 05/12/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 3483 | CS Maritimo U23 vs Rio Ave U23 | 2.29 | 3.51 | 2.64 |
| 14:00 | 2466 | Ethiopia Electricity vs Arba Minch Kenema | 3.26 | 2.92 | 2.22 |
| 14:00 | 2945 | Tianjin Teda vs Guangzhou Evergrande | 1.84 | 3.55 | 3.65 |
| 14:00 | 4756 | Hebei Zhongji vs Meizhou Kejia | 27.20 | 13.60 | 1.01 |
| 14:30 | 1248 | Shanghai Shenhua vs Hangzhou NG | 3.90 | 3.70 | 1.74 |
| 14:30 | 5987 | Henan Jianye vs Chengdu Qianbao | 2.37 | 3.30 | 2.67 |
| 15:00 | 3786 | Millwall U23 vs Ipswich U23 | 1.50 | 4.87 | 4.38 |
| 15:00 | 4465 | Legia Warszawa vs GKS Tychy | 1.29 | 5.84 | 6.42 |
| 15:40 | 4553 | Ahli Al-Fujirah vs Hatta Club | 3.31 | 3.36 | 2.00 |
| 15:40 | 5137 | AL Bataeh (UAE) vs AL Jazira AL Hamra | 1.27 | 5.05 | 8.55 |
| 16:00 | 1275 | Busoga United vs Bright Stars | 3.03 | 2.79 | 2.43 |
| 16:00 | 3156 | Apollon 1926 vs Apollon Larisas | 1.53 | 3.74 | 5.64 |
| 16:00 | 3896 | Polisi Tanzania vs Azam | 4.18 | 3.06 | 1.87 |
| 16:00 | 4875 | Crewe U23 vs Barnsley U23 | 2.15 | 4.07 | 2.57 |
| 16:15 | 3942 | Kallithea FC vs AEK Athens B | 1.38 | 4.01 | 8.01 |
| 18:00 | 1108 | Ararat Armenia vs Pyunik Yerevan | 2.14 | 3.02 | 3.32 |
| 18:00 | 2335 | Malkiya Club vs Bouri | 1.67 | 3.49 | 4.66 |
| 18:00 | 2402 | Al-Tadamun Buri vs Najma Manama | 7.01 | 4.38 | 1.37 |
| 18:00 | 2675 | Etehad Alreef vs Busaiteen | 6.81 | 4.18 | 1.40 |
| 18:00 | 4476 | Japan vs Croatia | 3.69 | 3.19 | 2.06 |
| 18:30 | 2350 | Club Omnisports de Korhogo vs Societe Omnisport | 4.18 | 2.87 | 1.95 |
| 20:00 | 4113 | FC Versailles 78 vs Sedan | 1.78 | 3.55 | 4.15 |
| 20:00 | 5326 | Omonia Nicosia vs Karmiotissa | 1.53 | 4.22 | 5.62 |
| 20:00 | 5533 | Steaua Bucuresti vs CS Mioveni | 1.33 | 4.66 | 8.92 |
| 20:00 | 5622 | Caykur Rizespor vs Pendikspor | 2.23 | 3.12 | 3.02 |
| 21:00 | 3135 | Hapoel Katamon Jerusalem W vs MS Kiryat Gat W | 3.30 | 3.54 | 1.94 |
| 21:00 | 3323 | Asi D Abengourou vs AF Amadou Diallo | 3.55 | 2.82 | 2.16 |
| 21:30 | 3999 | St Truiden U21 vs FCV Dender EH U21 | 1.36 | 4.77 | 6.42 |
| 21:30 | 4749 | Waasland Beveren U21 vs Lierse SK U21 | 1.90 | 3.84 | 3.21 |
| 22:00 | 2825 | RWD Molenbeek U21 vs AS Eupen U21 | 3.40 | 4.38 | 1.73 |
| 22:00 | 3270 | Brazil vs South Korea | 1.26 | 5.40 | 11.00 |
| 22:00 | 4140 | Excelsior Virton U21 vs Oostende U21 | 7.81 | 6.05 | 1.24 |
| 22:00 | 4501 | Westerlo U21 vs Lommel U21 | 1.96 | 3.71 | 3.12 |
| 22:00 | 4922 | Kmsk Deinze U21 vs Kortrijk U21 | 3.36 | 3.75 | 1.87 |
| 22:30 | 1378 | Pescara Calcio vs Taranto Sport | 1.51 | 4.09 | 6.18 |
| 22:45 | 4807 | Bradford PA vs Telford | 2.53 | 3.16 | 2.58 |
| 23:00 | 4598 | Ponferradina vs Burgos | 2.57 | 2.97 | 2.82 |
| 23:45 | 3177 | Mafra vs FC Vizela | 3.10 | 3.40 | 2.21 |

JUMANNE - 06/12/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 03:30 | 5402 | Arnett Gardens FC vs Molynes | 2.06 | 3.25 | 3.25 |
| 11:30 | 2719 | Real Kashmir vs Sreenidi Deccan FC | 2.32 | 3.07 | 2.92 |
| 14:00 | 2040 | Fuenlabrada vs Merida UD | 2.16 | 3.07 | 3.21 |
| 15:45 | 5462 | Al Masry Club vs National Bank | 2.05 | 3.09 | 3.79 |
| 16:00 | 4544 | ND Gorica vs ASK Bravo | 3.22 | 3.12 | 2.13 |
| 18:00 | 1502 | Morocco vs Spain | 6.00 | 3.55 | 1.61 |
| 20:00 | 2202 | Unirea Slobozia vs Dinamo Bucuresti | 2.55 | 3.10 | 2.80 |
| 20:00 | 4644 | Petrolul Ploiesti vs U Craiova SA | 2.77 | 3.06 | 2.43 |
| 20:00 | 4803 | Maribor vs NK Radomlje | 1.46 | 4.19 | 5.65 |
| 22:00 | 2095 | Portugal vs Switzerland | 1.89 | 3.30 | 4.20 |
| 22:45 | 5435 | Braintree vs Oxford City | 2.87 | 3.41 | 2.18 |
| 22:45 | 5483 | Farsley Celtic vs Kings Lynn | 3.80 | 3.55 | 1.80 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumatatu Desemba 5, 2022
Nipashe



Afya ya Pele yaimarika

UKURASA 30

# Mayele, Phiri wapishana kwa rekodi Ligi Kuu

## ●●● Ni wakati wakigongana kwa vita vya ufungaji bora kila mmoja akiwa na mabao 10, lakini...

**Na Adam Fungamwango**

MASTAIKA Moses Phiri wa Simba na Fiston Mayele Yanga, tayari wamefunga mabao 10 kila mmoja kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo inamaliza mzunguko wake wa kwanza, huku kila mmoja akimzidi mwenzake kwenye maeneo tofauti kitakwimu.

**Wakati Mzambia Phiri akimzidi Mayele kwa kuzifunga timu nyingi zaidi kuliko mwenzake, Mayele amecheza mechi moja pungufu kuliko mwenzake, huku nyingine akiingia kipindi cha pili.**

Phiri amecheza mechi zote 15 za mzunguko wa kwanza, huku Mayele akicheza 14, hakucheza mechi dhidi ya KMC pia akiingia kipindi cha pili kwenye mechi moja dhidi ya Geita Gold, lakini hakufunga bao lolote.

Takwimu zinaonyesha kuwa katika mechi hizo, Mayele amefunga mabao matatu 'hat-trick' kwenye mechi moja dhidi ya Singida Big Stars, lakini hana bao lolote la penalti kwenye 10 aliyotupia hadi sasa kabla ya mchezo wao wa jana usiku dhidi ya Tanzania Prisons.

Takwimu zinaonyesha kuwa Phiri amezifunga timu nane kwenye Ligi Kuu mpaka sasa ambazo ni Geita Gold, Kegara Sugar, KMC, Dodoma Jiji, Mtibwa Sugar, Namungo, Polisi Tanzania ambayo ameifunga mabao mawili, pia akifunga idadi kama hiyo dhidi ya Coastal Union Jumamosi iliyopita wakati wakishinda 3-0, moja likiwa la penalti.

Timu ambazo hajazifunga ni sita, Azam, Yanga, Ihefu, Prisons, Ruvu Shooting na Mbeya City.

Kwa upande wa Mayele amezifunga timu sita tu, ambazo ni Polisi Tanzania, Coastal Union, Mtibwa Siugar, Singida United akifunga mabao matatu, Dodoma Jiji akifunga mawili na akifunga tena mawili kwenye mechi dhidi ya Mbeya City.

Amekosa kuzifunga timu sita kwenye mechi alizocheza ambazo ni Simba, Azam, Ruvu Shooting, Geita Gold ambayo aliingia kipindi cha pili, Kagera Sugar na Ihefu, huku akiwa hajacheza kwenye mechi dhidi ya KMC.

Mabao hayo yamezisaidia timu zao kukaa katika nafasi nzuri za mbio ya ubingwa, kwani hadi sasa kabla ya mchezo wa jana wa Yanga dhidi ya Tanzania Prisons, timu hiyo ya Mayele ilikuwa nafasi ya pili kwa alama mbili nyuma ya Simba iliyokuwa kileleni kwa pointi 34, lakini ikicheza michezo miwili zaidi.

Yanga hadi sasa imecheza mechi 13 huku Simba yenyewe ikiwa imekamilisha raundi ya kwanza kwa kushuka dimbani mechi zote 15.

Kwenye mbio hizo za ubingwa pia miamba hiyo inakabiliwa na vita vikali kutoka kwa Azam FC iliyopo nafasi ya tatu kwa alama zake 32 yenyewe ikicheza mechi 14 hadi sasa.

Hivyo, kama Yanga imeshinda mchezo wake wa jana itakaa kileleni kwa alama moja zaidi na endapo ikishinda wa kukamilisha raundi ya kwanza, inamaana itaizidi Simba kwa

INAENDELEA UK. 31

## ROBO HIYOOO...



Lionel Messi, akishangilia baada ya kuipeleka Argentina Robo Fainali ya Kombe la Dunia kwa kufunga moja wakishinda 2-1 dhidi ya Australia nchini Qatar juzi.

**HABARI UK. 29**

# Mgunda na ushindi Simba SC

**Na Adam Fungamwango**

KAIMU Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, amesema amefurahi timu yake ya Simba kupata ushindi wa pointi tatu na mabao matatu, lakini hapo hapo ameumia kuona klabu yake ya zamani, Coastal Union ikipoteza na ndiyo maana hakushangilia mabao hayo kama ilivyo kawaida yake.

Amesema kwa heshima ya timu yake hiyo ambayo ameichezea kwa miaka mingi, iliyomfanya hata kuchaguliwa Timu ya Taifa, Taifa Stars, kwenda kucheza soka la kulipwa nje ya nchi na hata kumfanya kuwa kocha, hakuweza kushangilia, lakini ana imani kuwa watajipanga na kushinda kwenye mechi zinazokuja.

Alisema hayo juzi baada ya kumalizika kwa mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya timu yake ya Simba na Coastal Union ambapo Wekundu wa Msimbazi walitoka kifua mbele kwa mabao 3-0 kwenye Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga, shukrani kwa Wazambia Moses Phiri na Clatous Chama walioipa ushindi.

"Nimefurahi kwa timu yangu ninayoifundisha imeshinda, tumepata pointi tatu na mabao matatu, lakini nimesikitika kwa timu yangu ya zamani, Coastal Union kupoteza, sikuweza kushangilia, hii ni mara ya kwanza mimi kuwa mpinzani wa timu hii, kuna kitu nimejifunza, nimecheza, nimechaguliwa kwenye timu ya taifa, nimekwenda kucheza soka la kulipwa nje ya nchi na nimefundisha nikiwa Coastal, lakini leo niko sehemu nyingine, haya ni maisha, na hii ni kazi, nadhani wanajipanga tena ili kushinda mechi ijayo na sisi tunasonga mbele," alisema kocha huyo.

Alizungumzia mechi hiyo,

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >